**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 25 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mhe. Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI.**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha, 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 76

**Nyumba za Wananchi Kubomolewa**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na mkanganyiko wa mawazo miongoni mwa Wakazi wa Jiji la Mwanza wanaokaa na waliojenga katika miinuko kama nyumba zao zitabomolewa na Serikali na wao kuhamishwa kwa nguvu, na kwa kuwa wananchi hao walipokuwa wakijenga sehemu hizo Serikali ilikuwepo na haikuwazuia katika ujenzi huo:-

(a) Je, ni kweli Serikali haioni ina mpango wa kubomoa nyumba hizo?

(b) Kama ni kweli. Je, Serikali haioni kuwa hilo ni zoezi la hatari kwa usalama wa wananchi na vyomnbo vitakavyosimamia zoezi hilo?

(c) Je, huu si wakati muafaka kwa Serikali kuwapimia na kuwahakikishia wananchi maeneo hayo ili wananchi hao waishi kwa amani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti maalum, yenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, Jiji la Mwanza kama ilivyo miji mingine mikubwa ya Tanzania, asilimia ipatayo sabini (70%) ya wakazi wake wanaishi katika maeneo yasiyopimwa *(squatter).* Makazi holela mengi katika Jiji hili yako kwenye vilima. Baadhi ya vilima vilivyojengwa kiholelea katika Jiji la Mwanza ni vile vya Igogo, Bugando, Mabatini, Isamilo, Ibungilo, Kitangiri na Kilimahewa. Katika Jiji la Mwanza kuna nyumba zipatazo 40,000 zilizojengwa katika maeneo yasiyopimwa. Ujenzi huu umekuwa ukifanyika kinyume cha taratibu na sheria za ujenzi Mjini ambazo humtaka mwananchi kujenga baada ya kupata kibali cha ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sheria zilizokiukwa ni zile za Mipango Miji sura ya 355 ya mwaka 2002) kifungu cha 35 ambacho kinaeleza kuwa ujenzi mjini hauruhusiwi bila kuwa na kibali *(Planning consent).* Sheria nyingine iliyokiukwa ni ile ya Ujenzi Mjini Sura ya 101 *(Township Building rules)* kifungu cha 4(a) ya mwaka 1942. Sheria hii inasema wazi kabisa kuwa hakuna ujenzi wowote unaoruhusiwa mijini bila kuwa na kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuliona hilo tatizo, Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilifanya zoezi maalum kwa mwaka 2003 la kubaini idadi ya nyumba zilizojengwa kinyume na taratibu na sheria za ujenzi Mjini ili kuzuia ongezeko kwa kuzipa nyumba hizo namba. Halmashauri iliwekeana mikataba na wananchi kwa kushirikisha uongozi wa mitaa iliyokuwa imejenga ukingoni mwa vilima ili kuhakikisha kuwa hakuna zinazojengwa zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti ujenzi holela katika Jiji la Mwanza, Serikali ina mipango ifuatayo:-

- § Kuboresha na kupima maeneo yanayowezekana. Kazi hii imefanyika katika vilima, mfano Ibungilo la Isamilo na vilima ambavyo viko kwenye miinuko mikali na nyumba zimebanana ambavyo uboreshaji hautawezekana.

- § Halmashauri ina mradi wa kupima viwanja vingi ambavyo vitapatikana kwa wananchi.

- § Halmashauri inaandaa viwanja vidogo vya gharama nafuu eneo la Kiseke na Buswelu ambapo wananchi waliojenga kwenye vilima vikali wanashauriwa kuhamia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wataelimishwa hakutakuwa na nguvu zitakazotumika, bali wale waliojenga baada ya mwaka 2003 watatakiwa kuondoka kwa hiari.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, viwanja vinapimwa vya bei zote ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa hali zote ili wajenge kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na maelezo hayo hapo juu Serikali katika jiji la Mwanza imekuwa ikichukua hatua za kuzuia ujenzi holela na itaendelea kupiga vita ujenzi holela katika vilima vyake. Hatua za kisheria zitaendela kuchukuliwa pale wananchi wanapoendelea kujenga kiholela hivyo kuharibu miji yetu. Kwa vile Serikali haina mpango wa kutumia nguvu, hatutegemei tatizo lolote kutokea. Serikali katika Jiji la Mwanza inaendelea na mkakati wake wa kupima viwanja vidogo vidogo vitakavyofaa kwa wananchi walijenga kwenye vilima. Wananchi watashauriwa kwenda kwenye viwanja hivyo.

**SPIKA:** Kabla hujauliza sijui na wewe na umejenga kwenye miinuko hiyo? (*Kicheko*)

**MHE. ADAM MKIWA KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, sijajenga, ahsante nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema wale waliojenga baada ya 2003 watatakiwa kuondoka, Je, Serikali iko tayari kuwalazimisha wale waliojenga kabla ya 2003 katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba mwaka 2003 baada ya lile zoezi zile nyumba zote zilizojengwa kiholela 40,000 zimepatiwa namba. Kwa hiyo, nyumba zote zile zilizopatiwa namba hakuna mpango wa kuzibomoa, lakini kwa wale ambao wamejenga baada ya hapo nyumba zao zitabomolewa na watashariwa kuhamia sehemu nyingine.

Na. 77

**Kukamilisha Ujenzi wa Madaraja na Barabara**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa ujengaji wa madaraja huendana na utengenezaji wa barabara ili kupunguza hasara na upotevu wa fedha za umma na kwa kuwa tatizo limejitokeza kwenye daraja la Korintho, Ilembula ambako barabara haijatengenezwa.

Je, Serikali haioni kwamba inapoteza fedha za umma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba daraja la Korintho, Ilembula lililopo katika mto Halali ni Miundombinu muhimu sana. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 daraja hili lilikamilika kwa kujengwa kwa kiwango cha zege kwa jumla ya shilingi milioni 35 ni kweli pia kwamba mwaka huo wa fedha Serikali haikuwa na fedha ya kujenga barabara ya km.9 ambayo inapita katika daraja hili kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Nina amini kuwa hatua hiyo ya ujenzi wa daraja imara ilikuwa ni muhimu katika uchumi wa eneo hilo, lakini vile vile kwa maana ya kutoa huduma kwa wananchi. Kwa kufanya hivyo siyo kupoteza fedha bali ni hatua muhimu katika kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi. Kwa kufanya hivyo siyo kupoteza fedha bali ni hatua muhimu katika kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya ujenzi wa daraja hilo kwa kiwango cha zege ukarabati wa barabara ulifanyika kwa mwaka wa fedha 2005/2006 na ukarabati huu ulitengewa fedha kiasi shilingi 26,336,000/= kutokana ruzuku ya maendeleo ya kuzisaidia Serikali za Mitaa yaani. Kazi ya ukarabati ilifanywa na mkandarasi *Santona General Enterprises* na ilikamilika rasmi mwezi Januari mwaka 2007. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuchonga kwa greda barabara kiasi cha kilometa 9, kumwaga changarawe sehemu korofi kilomita 1, na kuchimba mifereji na kuweka kalvati za mistari zipatazo saba.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Njombe wanategemea sana hospitali iliyo Ikonda Makete kwa kupata matibabu na uchumi; na kwa kuwa barabara ya Njombe kupitia Igosi Kipengele kwenda Makete imekuwa na mbovu ina mashimo sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara hii ili iweze kupitika kwa ajili ya wagonjwa hao hasa wamama wajawazito?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ubovu wa barabara

nyingi nchini na kwa mwaka huu kama ilivyoonyeshwa kwenye Bajeti, kwamba fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge akienda kwenye Halmashauri yake washauriane waone umuhimu wa barabara ya Ikonda Makete ili waitengee fedha nyingi ili iweze kupitika kwa mwaka mzima.

Na. 78

**Hadhi ya Soko la Koboriloni**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara pamoja na wananchi wengi wa nchi jirani hutumia soko la Koboriloni ambalo kwa umaarufu wake limekuwa kama soko la kimataifa, ingawa halina hadhi hiyo?

Je, Serikali ina mpango gani wa kulifanya soko hilo kuwa na hadhi ya kimataifa badala ya kutumika kama gulio?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, soko la Kiboriloni lilianzishwa kwa ajili ya kuuza aina mbalimbali za mboga na ndizi, ila baadaye likawa ni maarufu kwa kuuza nguo, kuuza mitumba na mahitaji mengine ya kawaida. Soko hilo lilikuwa la kawaida lakini lenye wachuuzi wengi, baadhi wakitumia mabanda yaliyojengwa kwa muda.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hivi karibuni Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imeamua kujifunga soko hilo la Kiboriloni lilikuwa linawapa huduma wananchi wa Mikoa ya Kilimanjaro. Arusha, Manyara na hata nchi jirani. Wale wote waliokuwa na biashara eneo hilo wamehamishiwa uwanja wa *Memorial (memorial grounds)* ulio katika barabara ya kwenda Arusha *(Arusha Road*). Kwa kuzingatia hali hiyo namshauri Mheshimiwa Mbunge iwapo bado anayo azma ya ujenzi wa soko la kimataifa katika eneo la Kiboriloni aliwasilishe ombi hilo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ili waweze kuamua.

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata majibu ambayo yanatia moyo kama bado nia kweli ya kuliendeleza lile soko litakuwa ipo. Lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza, ni sababu zipi zilizoifanya Halmashauri hapa ikahamisha hilo soko?

Je, huko lilikohamishiwa kuna miundombinu ya kukidhi mahitaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, majibu hapa tumesema kwamba uamuzi wa kulihamisha soko hilo ulifanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ambapo Mheshimiwa Mbunge ni mmoja wa uongozi pia. Lakini nilitegemea kabisa kwamba katika hali hiyo yeye angekuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuelewa sababu zilizofanya soko likahamishiwa huko.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo swali la pili suala la miundombinu iliyoko katika eneo hilo, mimi nahakika kabisa kwamba uamuzi unapofanywa wa kurekebisha masoko hayo na kupeleka maeneo mbalimbali ni hatua ambazo zinafanywa na Halmashauri za mamlaka husika ili kuhakikisha kwamba wanaendesha biashara zao kwa ufanisi zaidi.

Na. 79

**Uchumi wa Mkoa wa Mara**

**MHE. VEDASTUS MATHAYO MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Mara ni Mkoa wenye rasilimali nyingi kama vile ardhi nzuri kwa kilimo, madini, mifugo na samaki na kwa kuwa ili kuinua uchumi wa Mkoa rasilimali kama mifugo, samaki na mazao ya kilimo havina budi kusafirishwa nje ya nchi katika masoko mbalimbali.

Je, Serikali ina mpango gani katika kusaidia Mkoa huo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua rasilimali nyingi za Mkoa wa Mara zinazojumuisha mazao ya kilimo, madini, mifugo na samaki ambavyo ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa Mkoa huo kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge. Katika kusaidia upatikanaji wa masoko wa mazao ya rasilimali za Mkoani Mara Wizara yangu inayo mipango kadhaa kama ifuatavyo:-

(i) Wizara yangu kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* na Halmashauri ya Biashara ya nje *(BET)* huandaa maonyesho na mafunzo kwa wajasiriamali wadogo ili kuwajengea uwezo wa kufanya biashara kitaalamu pamoja na kuwapatia mbinu za kukabiliana na changamoto mbalimbali za kibiashara.

(ii) Mpango wa kuanzisha vituo vya biashara sehemu za mipakani imeandaliwa ambapo Wilaya ya Tarime itashirikishwa.

(iii) Utaratibu wa kutoa mafunzo ya usindikaji wa vyakula kwa kuzingatia mazao mazao asilimia ya Mkoa wa Mara umekwishaanza kwa zao la ndizi huko Tarime.

(iv) Tayari Viwanda viwili vya kusindika samaki wa Ziwa Victoria vimeanzishwa na vinafanya kazi. Na kwa kutumia mabaki ya samaki kutoka viwanda hivyo viwanda vingine vidogo vitano vya usindikaji wa chakula cha mifugo vimeanzishwa.

(v) Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mara tumebainisha eneo la uwekezaji kwa mpango wa *EPZ* lenye hekta 2,200 eneo Tairo, Wilayani Bunda ambalo litakuwa mahsusi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zitakazouzwa nje ya nchi kutokana na malighafi ya Mkoa huo.

(vi) Aidha, upo mkakati wa kufufua kiwanda cha maziwa Mkoani Mara ili kupanua soko la maziwa na hivyo kuinua kipato kwa wananchi wa Musoma.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaupongeza Mkoa wa Mara kwa kuandaa Mkutano wa Wawekezaji mapema mwaka huu Mkoa Mara kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake na kwa kutambua kwamba kwa kweli kwa Mara ni kati ya mikoa ambayo ina rasilimali nyingi na huku ikiwa na matatizo makubwa ya usafiri maana zile rasilimali lazima zisafirishwe nje ili tuweze kujipatia kipato. Sasa swali langu kulikuwa, kulikuwa na mkakati na mpango mkubwa wa kutengeneza reli ya kutoka Tanga hadi Musoma ambayo ilikuwa ni mkakati wa muda mrefu. Lakini vilevile kwa kuwa uwanja wa ndege wa Musoma upo katikati ya mji na mdogo na hauwezi kupanuliwa kukawa na mpango mwingine wa kuuhamishia eneo la Musoma Vijijini kuelekea kule Mgango, Je, mipango hiyo yote, imefikia wapi kuhakikisha kwamba zile rasilimali za Mara zinaweza kusafirishwa nje na wananchi waweze kujipatia kipato?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru tu kwamba Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba huu mpango wa ujenzi wa ujenzi wa reli kutoka Tanga hadi Musoma upo na huo mpango wa ujenzi wa uwanja wa pia upo. Kwa hiyo, hii yote ni sehemu ya mipango ambayo nimeieleza kwamba imedhamiria kusaidia wananchi wa mkoa wa Mara kuweza kusafirisha mazao yao nje. Sasa hatua ambayo mipango hii imefikia, mimi nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba awe na subira muda si mrefu Wizara ya Miundombinu itawasilisha makadirio yake hapa Bungeni, bila shaka yatapatiwa majibu.

**MHE. ELIATA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa Musoma ina mazao sawa na yale yanayopatikana Rukwa. Je, Serikali ina mipango gani ya makusudi ya kusaidia Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatambua rasilimali na mazao mengi yaliyoko katika mkoa wa Rukwa na mipango tuliyonayo haitofautiani sana na ile niliyoieleza katika jibu langu la msingi hapa, kwamba shirika letu la *SIDO* pamoja na *BET* wanaandaa mafunzo haya ni nchi nzima kusema kweli si kwa ajili ya mkoa wa Mara ni nchi nzima ni pamoja na

Rukwa. Kwa hiyo, baadhi ya mikakati niliyoitaja katika jibu la msingi inahusisha mkoa wa Rukwa pia.

Na. 80

**Malipo ya Kutunza Watoto kwa Wanandoa Walioachana**

**MHE. RAMADHAN A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa, inapotokea wanandoa wameachana wakiwa na watoto na shauri lao likafikishwa kwenye Vyombo vya Sheria kuna utaratibu kwa mzazi wa kiume kupeleka matumizi ya watoto kupitia Ofisi ya Ustawi wa Jamii:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kisheria kinapaswa kulipwa kwa mwezi kama matumizi ya kutunza familia?

(b) Je, kiasi kinacholipwa kinakidhi matakwa ya hali halisi ya maisha kwa sasa?

(c) Kama kiasi hicho hakilingani na hali halisi ya maisha ya sasa kwa Mtanzania. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya marekebisho. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya marekebisho katika Sheria husika ili kuweka viwango vinavyokidhi au vinavyokaribia hali halisi ya maisha kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa Namba 5, ya mwaka 1971, ndio inayotumika katika mashauri yanayohusu matunzo ya watoto (*duty to maintain children*). Kimsingi sheria hii inampa mlezi wa kiume jukumu la kumtunza mtoto. Hata hivyo, ikibainika kwamba mlezi huyo wa kiume amefariki, hajulikani alipo au hana uwezo wa kumtunza mtoto basi jukumu hilo litapaswa kufanywa na mzazi wa kike.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna kiasi maalum cha fedha kilichowekwa kwa mujibu wa sheria kinachopaswa kulipwa kwa mwezi kama matumizi ya kutunza familia. Kiwango kinachopaswa kulipwa hutamkwa na Mahakama.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kutamka kiwango cha matunzo kinachotakiwa kutolewa Mahakama huangalia vigezo vingi vikiwemo kipato cha mlezo wa kiume wa kiume na kipato cha mama wa mtoto. Mahakama kiasi cha matunzo ya mtoto mzazi

huyo aweze kumsaidia mtoto lakini na yeye mwenyewe aweze kujikimu. Kama mama wa mtoto ana uwezo kuliko baba wa mtoto, Mahakama pia huzingatia jambo hilo. Kwa kuwa Mahakama inatumia uzoefu, busara na mamlaka yake na vilevile inaangalia hali halisi ya maisha, kiwango kinachotolewa mara nyingi kinakidhi matakwa yaliyokusudiwa kisheria.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa, kutungwa Sheria ya Watoto na kutungwa kwa Sheria ya Urithi na mirathi ambazo pamoja na mambo mengine zitazingatia vigezo vinavyohusu gharama za matunzo ya watoto ili kuboresha maisha ya watoto pindi linapotokea jambo lolote kwa mzazi au wazazi.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa sheria hiyo inataka kufanyiwa marekebisho baada ya miaka thelathini iliyopita, wakati Wizara husika ikiwepo, Je Serikali inafahamu kwamba wapo watoto wamekosa haki za msingi kama kupata elimu kwa sababu sheria imechelewa kufanyiwa marekebisho?

Je, Serikali ina mpango gani kuwapa fidia watoto waliothirika na sheria hasa kwa kukosa elimu na wengine wako mitaani wakati watoto hao hawana kosa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, si rahisi kusema kwamba watoto waliokosa haki wamezikosa kwa sababu tu sheria haikubadilishwa, inawezekana kabisa watoto hawa wamekosa haki na uwezo huo wa kusoma kwa sababu zingine nyingi tu zinazotokana na hali ya familia na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, si rahisi kusema pia kwamba kwa sababu hiyo basi watoto hawa watapata fidia Serikali inao utaratibu wa kusaidia kusomesha watoto ambao hawana wazazi ama ambao wazazi wao wameshindwa kuwasomesha watoto hao, lakini si sababu ya sheria ndio iliyosababisha tatizo hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Chalinze.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Sheria ni kubana wale walio wahalifu. Pili ni jukumu la wazazi kuona kwamba ni kazi yao kuwalea watoto wao.
Kwa hivyo naomba Wazazi wote wakiwemo wa kiume na wa kike wasingoje kubanwa na sheria bali waone umuhimu wa kulea watoto wao ipasavyo. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya watoto wa mitaani na watoto wanaoishi mazingira magumu yamekuwa mengi na hasa ukizingatia watoto wa kike wanaopata

mimba wengi wao chanzo kinatokana na hali ngumu ya maisha. Aidha sheria ya ndoa ya mwaka 1971 kuna kipengele kinachosema kwamba mtoto anatunzwa kwa shilingi mia.

Je, Wizara inasemaje kuhusu hilo? Je, ni lini Wizara itutamkie hapa leo Sheria hiyo itakuwa tayari?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kweli yapo matatizo ya watoto wa mitaani na lipo tatizo kubwa tu la watoto wetu kupata mimba, lakini hili ni tatizo la kijamii na halitokani na kuwapo ama kutokuwapo na sheria. Sheria anayoizungumzia Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu ni sheria ya *affiliation act* ambayo inaweka kiwango hicho cha shilingi mia na siyo sheria ya ndoa. *(Makofi)*

Sheria hii haiwahusu wanandoa bali inawahusu watu ambao wamepata mtoto lakini hawapo katika ndoa, wako nje ya ndoa.

Sheria ya Ndoa ni Sheria namba 5 ya mwaka 1971 na viwango vinavyotamkwa vinategemea Mahakama baada ya kufanya upembuzi mzuri wa hali ya halisi basi itaweka kiwango kulingana na uwezo wa Baba au Mama katika hali ilivyo.

Kuhusu lini Sheria hii italetwa hapa ninapenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa Sheria ya Watoto, Ndoa na Mabadiliko ya Sheria ya *Affiliation* kupitia *current Act* zitaletwa hapa mwezi Januari au Februari mwaka ujao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tuendelee Waheshimiwa Wabunge, sijui kwa nini suala hili linavuta hisia zenu sana lakini naona tuendelee Wizara hiyo hiyo swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Bujibu Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba.

Na. 81

**Hati za Kuzaliwa**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:

Kwa kuwa, Haki za Kuzaliwa ni haki kwa kila mwananchi na kwa kuwa vyeti hivyo vinahitajika sana kwa vijana wetu kwa shughuli mbalimbali hususan kujiunga na Vyuo na ajira na kwa kuwa wazazi wengi huwa hawafuatilii vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wao kwa kukosa elimu ya kuona umuhimu wa vyeti hivyo na utaratibu mrefu wa kuvipata vyeti hivyo pamoja na kuwa siku za karibuni utaratibu umerahisishwa na kuwekwa chini ya katibu Tawala wa Wilaya.

(a) Je, Serikali inatoa maelezo ya athari zipo zitakazoweza kujitokeza iwapo utaratibu bora utaandaliwa ili vyeti hivyo viwe vinatolewa kwenye zahanati, kliniki na hospitali ambako watoto hao wanazaliwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa iwapo utaratibu huo utabadilika utaweza kuwa kichocheo kwa akina mama wengi kwenda kujifungulia kwenye zahanati, kliniki, vituo vya afya na hospitalini na hivyo kupunguza kwa kiwango fulani vifo vya akina mama vinavyotokea wakati wa kujifungua na watoto wengi wanaweza kupata vyeti vyao mapema na bila usumbufu mkubwa.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katibu na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua kuwa ukosefu wa elimu juu ya umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa ni chanzo cha wazazi wengi kutosajili vizazi vya watoto wao na kupata vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kama athari zozote zinazoweza kutokea iwapo vyeti vya kuzaliwa vitatolewa kwenye hospitali, zahanati na kliniki hakuna utafiti uliofanyika kuhusu hili. Hata hivyo kuzipa hospitali, vituo vya afya na zahanati jukumu hilo itakuwa ni kwenda kinyume cha Sheria ya uandikishaji vizazi na vifo inayotamka kuwa Msajili wa Vizazi na Vifo wa Wilaya atakuwa Katibu Tawala wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kutoa vyeti hospitali kuwa kichocheo cha akina Mama kujifungulia hospitalini, hakuna utafiti unaoonyesha kuwa hiki ni kichocheo. Yako mambo mengi yanayofanya akina mama kujifungulia majumbani yakiwemo uwezo mdogo wa kumudu gharama za hospitali, umbali wa huduma za hospitali na kadhalika. Sidhani kama kutolewa cheti cha kizazi hospitali kama kitakuwa kichocheo cha akina mama wengi kujifungulia hospitali.

Hata hivyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, vifo vingi vya akina mama na watoto vinaweza kuepukwa kama akina mama watajifungulia katika zahanati, vituo vya afya, kliniki na hospitali.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Bujibu P. Sakila.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali vizuri lakini moja ya lengo la msingi katika swali hili ni kuiomba Serikali kwamba iangalie uwezekano wa kuwasaidia wananchi wanaokaa mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya kama wale wa Chilima, Igematu, Imanai ambayo wanakaa umbali wa kilomita 100

kutoka Ndugu na ninachoomba ni Serikali kangalia uwezekano wa kuwasaidia watu kama hao.

Je, sasa Serikali haioni kwamba itakuwa vizuri zaidi mara baada ya mtoto kuzaliwa fomu muafaka ijazwe hapo hapo katika *dispensary,* zahanati au kituo cha afya zitumwe kwenye ofisi husika na hatimaye vyeti vitakapokuwa tayari vitumwe katika *dispensary,* zanahati na katika vituo vya afya ili mwananchi aweze kupata vyeti vyake kwa urahisi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kajibu swali la Mheshimiwa Bujibu P. Sakila, kama ifuatavyo:

Ni kweli kwa sasa vyeti vya kuzaliwa vinatolewa katika Wilaya ambapo kwa vijiji kama vile alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vinaweza kuwa ni mbali sana na Wilaya hiyo. Kwa kulizingatia hilo na kutambua ukweli huo Serikali kwa sasa imekipata chombo hicho kinashughulika na uandikishaji kinachoita *RITA* yaani *Registration Insolvency and Trusteeship Agency* kimeanza kufanya utaratibu wa kuandikishwa katika Tarafa.

Hivi ninavyozungumza katika Mkoa wa Dodoma hiyo shughuli imeanza na ni jana tu Wataalam walikuwa Chamwino, juzi walikuwa katika Wilaya nyingine katika mkoa huu wa Dodoma, Makatibu Tarafa wote wa Mkoa huu wamekwishapata mafunzo katika suala hili. Utaratibu wa kuandikisha katika Tarafa utaendelea kwa nchi nzima na baadaye tutashuka kidogokidogo mpaka tutafika vijijini jinsi tutakavyoweza kuimarisha hii *agency* yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunahamia sasa Wizara ya Nishati na Madini, Swali linaulizwa na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 82

**Matumizi ya Gesi ya Songo Songo Majumbani**

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI** aliuliza:

Kwa kuwa Serikali katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliahidi kwamba katika awamu hii gesi ya Songo Songo itaanza kutumika majumbani ili kuwapunguzia wananchi adha ya kutumia mkaa au kuni:-

(a) Je, ni lini mpango huo utaanza na ni wapi na kati ya sehemu hizo, sehemu za Kilwa na hasa Kijiji cha Songo Songo kitakuwepo?

(b) Kwa kuzingatia kipindi hiki ambapo mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira kinaendelea. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha

matumizi ya Nishati hiyo kwa haraka nchini kote ili kunusuru nchi yetu na balaa la ukosefu wa mvua na njaa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu;

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum, naomba nitumie fursa hii kuwapa pole familia na jamaa wa marehemu kwa ajali ambayo imetokea jana Mkoani Singida na Marehemu watatu, niitumie fursa hii kumwomba Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu Mahali Pema Peponi, Amin! Lakini pia nitumie fursa hii kuwaombea majeruhi katika ajali hiyo na kwamba Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia waweze kupona haraka.

Baada ya kusema maneno hayo ya utanguli na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikilihimiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* linaloshirikiana na kampuni ya *Pan African Energy* kukamilisha miradi ya kutumia gesi asilia kwa kupikia majumbani, kwenye taasisi mbalimbali na mahotelini kwa njia ya kusambazwa na mabomba yaani (*Piped Natural Gas (PNG*); na pia matumizi ya gesi asilia katika kuendeshea mitambo na hasa magari.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo la Serikali, mwezi Agosti, 2006 *TPDC* iliingia mkataba na mshauri mwelekezi ambaye ni Kampuni ya *Ultimate Petroleum Technology* ya China ili kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya kutumia gesi asilia kama Nishati ya kupikia na pia kama Nishati ya kuendeshea magari katika nchi yetu kwa kuanzia na Jiji la Dar es Salaam. Ukamilishaji wa taarifa ya mwisho unaoendelea. Upembuzi huo utakapokamilika utatoa mwelekeo halisi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam lilionekana liwe sehemu ya kuanzia utekelezaji wa mradi huo kutokana na kwepo mahitaji makubwa na soko la kutosha na kuwa na maeneo yaliyopimwa na kuancha nafasi ya kuweza kupitisha mabomba kwa ajili ya mradi huo. Hata hivyo, kwa mantiki ya kuanza utekelezaji wa mradi wa upelekaji wa gesi majumbani kwa njia ya mabomba licha ya kuanzia kwenye Jiji la Dar es salaam ambako mahitaji yake ni makubwa vilevile utajumuisha Mkoa wa Lindi inakotoka gesi hiyo. Baadaye itafuatia Mikoa mingine itakayoonyesha mahitaji makubwa ya gesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa matumizi ya gesi asilia (*Compressed Natural Gas (CNG*) kama nishati ya kuendeshea magari, utaanzia kwenye Jiji la Dar es salaam na baadaye Mikoa mingine kulingana na mahitaji na kiasi cha gesi na kuthibitika kuwepo kwa gesi ya kutosha ya kukidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upembuzi unaoendelea ukikamilika utatoa mwelekeo halisi wa mradi wa matumizi ya gesi asilia majumbani. Kama nilivyosema katika maelezo yangu ya awali, utekelezaji wa miradi huo utaanzia Jijini Dar es Salaam. Vilevile utajumuisha sehemu za Mkoa wa Lindi, hususan Songosongo inapotoka gesi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali na *TPDC* zimeweka jitihada za dhati kutafuta maeneo zaidi hapa nchini yenye raslimali ya gesi zaidi ya maeneo yaliyogunduliwa kabla. Kupatikana kwa maeneo mengi zaidi yenye gesi asilia yatasaidia kupatikana kwa raslimali zaidi ya gesi hiyo na hivyo kufanikisha upelekaji wake katika maeneo mengine ya nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi swali la nyongeza.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, gesi ni nyenzo muhimu katika kuleta umeme na kwa kuwa umeme ni nyenzo muhimu pia katika kuleta maendeleo na kwa kuwa umeme ni nyenzo muhimu pia katika kuleta maendeleo na kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Kilwa wanatumia umeme wa *generator* ili kupata mahitaji yao na umeme huo hautoshelezi kwa kuwa watumiaji wameongezeka. Je, Serikali ni lini itawahakikishia wananchi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya Kilwa kupata umeme wa uhakika kwa kutumia umeme wa gesi ili kuondokana na adha hii ya umeme wa mgao ambao tunaupata Kilwa na Mkoa wa Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, tunarudia tena kwa mara nyingine kuendelea kulithibitishia Bunge hili tukufu na Taifa kwa ujumla kwamba ule mpango wa usambazaji wa umeme kwenye Mikoa ya Kusini hasa kutokana na raslimali ambayo imezidi kuzinduliwa kila wakati na sasa hivi kuna Kampuni inayofahamika kama *ATMAS* inayoendelea na usambazaji wa umeme katika Mikoa ya Kusini. Tunatumia nafasi hii kuwakumbusha wananchi na Wabunge kwa ujumla kwamba huduma ya umeme itakuwa ya uhakika hivi karibuni, mpango upo na unaendelea wa kusambaza kupitia Nishati ya kutumia gesi kama ambavyo imekuwa ikifanywa na kampuni ya *ATMAS.* Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo wakati mambo ya kitaalamu yanaendelea kukamilishwa kuhakikisha kwamba Mikoa ya Kusini na Mikoa mingine ambapo raslimali hii ya Nishati inahitajika itakuwa inatekelezwa na kufanikishwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, Wizara hiyo hiyo swali linaulizwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi.

Na. 83

**Uhakiki wa Mikataba ya Madini**

**MHE. HAMADI RASHID MOHAMED** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikihakiki mikataba mbalimbali hasa ya uwekezaji katika Sekta ya Madini.

(a) Je, Serikali ilipanga kupitia mikataba mingapi na ipi kwa majina?

(b) Je, ni mikataba mingapi imekwishapitiwa na kasoro zake ni zipi?

(c) Je, kazi hiyo inategemewa kumalizika lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamadi Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko kutoka kwa wananchi, Waheshimiwa Wabunge na Wadau mbalimbli kuwa Sekta ya Madini haichangii ipasavyo katika uchumi wa nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliagiza Wizara ya Nishati iunde Kamati Maalum ya kupitia mikataba ya Madini na kutoa ushauri utakaowezesha Sekta ya Madini kupongeza mchango wake kwenye uchumi. Kamati hiyo iliundwa na Wizara yangu ikishirikisha Wajumbe wengine kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira; Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; Wizara ya Fedha; TAMISEMI; Wizara ya Sheria na Katiba, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA);* Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST);* Benki ya Tanzania *(BOT)* na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO).* Kazi ya kupitia mikataba ya Madini ilianza rasmi tarehe 10 Mei, 2006 na kukamilika tarehe 8 Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa kazi ya kupitia mikataba kulifungua milango ya kuanza kwa majadiliano baina ya Serikali na kampuni zenye leseni cha uchimbaji mkubwa wa dhahabu ambazo zina mikakata na Serikali. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Hamadi Rashid Mohamed, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kupitia mikataba yote mitano ambayo Serikali iliingia na makampuni makubwa ya uchimbaji wa dhahabu. Mikataba hiyo ni kati ya Serkali na kampuni ya *Bulyanhulu Gold Mine Limited* inayomiliki mgodi wa Bulyanhulu ulioko katika Wilaya ya Kahama, *Pangea Minerals Limited* inayomiliki mgodi wa Tulawaka ulioko Wilayani Biharamulo, *North Mara Gold Mine Limited* inayomiliki Mgodi wa *North Mara Mine* Wilayani Tarime, *Geita Gold Mine Limited*

inayomiliki Mgodi wa Geita katika Wilaya ya Geita na *Resolute Tanzania Limited* inayomiliki mgodi wa *Golden Pride* Wilayani Nzega.

(b) Mheshimiwa Spika, mikataba yote mitano ambayo Serikali iliingia na makampuni makubwa ya uchimbaji wa dhahabu ilipitiwa. Zoezi hilo limebainisha kuwa kuna haja ya kurekebisha baadhi ya vivutio vitolewavyo kwa wawekezaji. Lengo ni kuharakisha makampuni ya Madini kulipa kodi haraka.

(c) Mheshimiwa Spika, kazi ya kupitia mikataba yote ilikamilika mwezi Julai, 2006. Majadiliano kati ya Serikali na Kampuni moja moja yanaendelea ili kuhakikisha Taifa linanufaika ipasavyo na maliasili yake. Aidha, Serikali inakusudia kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi katika sekta ya Madini.

**SPIKA:** Swali la Nyongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Katiba Kifungu cha 63(2) na Sheria Namba 3 ya mwaka 1988 ya *Immunities and Privileges Act* inampa madaraka Mbunge au Bunge kupata nyaraka zozote za Serikali. Je, Serikali inatumia kifungu gani cha Katiba na Sheria gani kulikatalia Bunge kupata nyaraka wanazozihitaji ikiwa ni pamoja na mikataba inayohusiana nayo?

Pili, kwa kuwa, Serikali katika kupitia Mikataba hii imeona mapungufu na kazi hii imefanyika katika kipindi kisichopungua sasa mwaka mmoja kuna sababu gani za Serikali kushindwa kuonyesha katika Bajeti ya mwaka huu unafuu au mapato yaliyopatikana kutokana na *negotiations* hizo?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo;

Serikali hata siku moja haijakatalia Mbunge yeyote kupata nyaraka za kutoka Serikalini, mikataba si nyaraka za Serikali ni kati ya watu wawili walioingia mkataba. Sasa hiyo mikataba ni ya kibiashara kwa hiyo katika kufuatilia mikataba ya kibiashara ikiiweka wazi na ukiileta Bungeni ambayo inakuwa ni hadharani ina maana ile mikakati ya kibiashara iliyowekwa na mshindani mmoja na mwingine unaitangaza kwa dunia nzima jambo ambalo halikubaliki katika vipengele vile ambavyo vinaambatana na *confidentiality*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Serikali kila wakati katika Wizara mbalimbali ilikuwa ikitoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati mbalimbali zinapotaka kupitia sheria hizo na jinsi tulivyozungumza kwamba hizi sheria tunataka kuzidurusu kufuatana na hayo mapungufu tuliyoyaona na pindi pale itakapofikia wakati

ule kwamba ziletwe Bungeni zitakuwa hapa tutazijadili na kuzipitisha kama tutaona inafaa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima J. Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na kwa kuwa Serikali inaingia mkataba kwa niaba ya wananchi nikimaanisha raslimali zozote zinazoingizwa kwenye mkataba ni kwa niaba ya wananchi. Je, kitendo cha Waziri kutaka kusita kuleta hizo *documents* anataka kuliambia hili Bunge kwamba kuna maovu ambayo yanakuwepo humo ndani ambayo hataki sisi tuyaone? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima J. Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Suala la mkataba wa kibiashara ni tofauti na suala la maovu, nataka kuliambia Bunge lako tukufu kwamba huwezi ukaleta mkataba wote na vipengele vyote, kama kuna kipengele fulani ambacho mtu anauliza hicho kinaweza kuzungumziwa kama kipengele lakini siyo mkataba wote unavyoeleza kwamba yupo nani, kiasi gani anapewa na kadhalika. Sasa hicho ni kitu tofauti, ni tofauti kama kuleta mkataba kama ulivyo mzima na kutafuta kipengele ambacho Mbunge ana wasiwasi nacho ambacho kinaweza kujadiliwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tuendelee suala hili ni pana litaendelea kujadiliwa. Tunahamia Wizara ya Miundombinu swali linaulizwa na Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Na. 84

**Fidia kwa Wananchi Watakaohamishwa kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Makongorosi**

**MHE. BENSON MWAILUGULA MPESYA** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuwalipa fidia wakazi wa Isanga, Mwangekwa na Iganzo ili kupitisha ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongorosi, kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa, mali zao zilithaminishwa:-

(a) Je, Wananchi hao wategemee kulipwa lini ili kupitisha barabara hiyo muhimu?

(b) Kwa kukwa, barabara hiyo ndiyo itokayo Capetown kwenda Cairo. Je, Serikali haioni kuwa ni vyema iharakishwe kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu;

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, usanifu wa barabara ya Mbeya – Makongosi umezingatia na kupitia ndani ya hifadhi ya barabara husika hivyo barabara yote inatarajiwa kujengwa katika eneo la miliki ya barabara.

Aidha, katika maeneo ambayo shughuli za ujenzi ama upanuzi wa barabara utafanywa nje ya mipaka ya eneo la miliki ya barabara, Wizara yangu italipa fidia kwa mujibu wa Sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara itokayo *Cape Town* kwenda *Cairo:- The Great North Road* kulingana na nyaraka za Sheria ya Barabara inaingilia Tunduma kutokea Zambia na kupita katika Mikoa ya Mbeya na Iringa ikifahamika kama *Tanzam Highway*. Aidha, kutokea Iringa imefuata barabara kuu ya Iringa – Mtera – Dodoma – Babati hadi Arusha na kuingia Kenya kupitia Namanga.

Hata hivyo, kwa umuhimu wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi, Serikali iliamua kuijenga kwa kiwango cha lami. Ili kurahisisha utekelezaji na kwa kuzingatia uwezo wa fedha, Wizara kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) iliamua kuigawa Barabara hii katika sehemu tatu. Sehemu ya Kwanza yenye urefu wa kilomita 36 inaanzia Mbeya hadi Lwanjilo. Uchambuzi wa zauni kwa ajili ya ujenzi wa sehemu hii uko katika hatua za mwisho. Aidha, ujenzi wa sehemu mbili zilizobaki kati ya Lwanjilo na Makongorosi utatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mpesya.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa uthaminishaji wa mali katika barabara hii ulishafanyika. Je, uchambuzi wa wale wanaostahili kulipwa utafanyika lini ili ikiwezekana wahame kabla ya msimu wa mvua?

Pili, kwa wale ambao ni wazee sana na wajane ambao wengi wao wapo ndani ya mipaka ya barabara na wameishi katika maeneo hayo zaidi ya miaka 50 Serikali inatoa tamko gani katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Benson Mpesya, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza barabara hii kwa kweli inapitia katika eneo au milki ya barabara yenyewe kwa maana hiyo Sheria ya Barabara hapa itatumika na kama ilivyo ni kwamba wale ambao walikuwa kwenye hiyo *reserve* kwa mujibu wa Sheria hawatalipwa. Lakini kama barabara hiyo kutakuwa na haja ya kuipanua au kubadilisha ile *alignment* yake ili ipite nje ya mipaka au kwenye *road reserve* basi wale watalipwa na kwa kuwa kazi hiyo karibu itaanza itajulikana hivi karibuni ni nani anastahili kulipwa ni nani anastahili kulipwa kwa maana kwamba aliyekuwa nje ya *road reserve* lakini Barabara imemfuata huko au imepinda kumfuata, kumfuata atalipwa na hiyo shughuli itafanyika haraka iwezekanavyo kwa sababu kazi hiyo ya Barabara karibu inaanza. *(Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Msindai swali la nyongeza.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Barabara ya Mbeya – Chunya – Rungwa inakwenda mpaka Itigi na mpaka Mokiwa. Serikali inasemaje juu ya kuendeleza hiyo Barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msindai kama ifuatavyo;

Ni kweli kama alivyoeleza kwamba Barabara hiyo ikitokewa Mbeya – Chunya – Makongorosi inakwenda mpaka Rungwa hadi Itigi Mkiwa. Lakini katika mipango ya Serikali ni kutekeleza kwa awamu, kilichoamuliwa kwa sasa ni kujenga Barabara ya lami kutoka Mbeya hadi Makongorosi lakini kwa kipindi hiki tumeahidi na iko kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba tutaboresha eneo la kutoka Makongorosi hadi Rungwa, Itigi hadi Mokiwa kwa kiwango cha changarawe kwa sasa ili Barabara hiyo iendelee kupitika lakini kwa maana ya kujenga kwa kiwango cha lami bado uwezo wa fedha hatuna.

**SPIKA:** Swali la mwisho bado Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi.

Na. 85

**Ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Mongoyo**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, umebainika kwamba ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Mingoyo haitaweza kukamilika kwa kiwango cha lami kama Serikali ilivyoahidi katika kipindi cha

mwaka wa fedha 2007/2008 hivyo kufifisha matumaini ya wananchi wa Mikoa ya Kusini kwamba, kama ingekamilika ingerahisisha usafiri wa uhakika kwenda Dar es Salaam.

(a) Je, Serikali ina matarajio gani na lini ya kukamilishwa kwa Barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

(b) Je, kwa nini Serikali inaruhusu ng'ombe toka nje ya Mikoa ya Lindi, Mtwara kupita kwa wingi kwenye Barabara hiyo mpya kwa kisingizio cha kutafuta maeneo ya malisho mapya kusini?

(c) Je, Serikali imejifunza nini katika kujenga Barabara kwa kutumia fedha zake yenyewe, kama ilivyo kwa Barabara hiyo, ikilinganishwa na ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Mwanza ambayo imetumia fedha za Wafadhili kwa sehemu kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfonce Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Kibiti – Nangulukulu - Lindi – Mingoyo, yenye urefu wa jumla ya kilometa 347, na ambayo ilikuwa na miradi mitano tofauti, umechelewa kukamilika kutokana na sababu mbalimbali ambazo zimekuwa zikielezwa humu Bungeni. Hata hivyo, miradi hii yote, ukiacha sehemu ya Ndundu – Somanga (km 60), sasa inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka kesho (2008).

Kuhusu kipande cha Ndundu – Somanga, inayofadhiliwa na *KUWAIT FUND /OPEC,* baada ya matatizo yaliyojitoleza kwenye zabuni ya kwanza, kama tulivyokwisha jibu humu Bungeni, zabuni ya pili iliyotangazwa upya imefunguliwa tarehe 19/06/2007 aambapo makandarasi watano wamejitokeza. Uchambuzi wa zabuni hizo utakamilika tarehe 9/7/07 na mkataba wa ujenzi kusainiwa mwezi Agosti, 2007. ujenzi unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2010.

Kwa maana hiyo, kabla ya mwisho wa mwaka 2010, barabara yote ya Kibiti – Lindi - Mingoyo itakuwa imakamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haijaruhusu ng'ombe kupita kwenye Barabara hii au barabara nyingine kwa kisingizio chochote. Kupitisha mifugo hususan ng'ombe kwenye barabara kunaathiri uwezo wa barabara kudumu kutokana na kingo za barabara kubomolewa na kwato za mifugo hiyo na kusababisha mmomonyoko wa tuta la barabara.

Aidha, mifugo huangusha nguzo za alama barabarani na kusababisha kufifia kwa alama za juu ya Barabara hususani mistari ya rangi kutokana na kinyesi kinachoachwa na mifugo hiyo.

Tunaomba ushirikiano wa viongozi, wananchi na vyombo vya dola katika kudhibiti tabia hii ya wafugaji kupitisha mifugo yao kwenye barabara popote nchini. Ng'ombe wanaruhusiwa tu kusafirishwa kwa barabara wakiwa ndani ya magari. Pale ambapo ni lazima ng'ombe wakatishe barabara, kuna maeneo maalum yanayoonyeshwa kukatishia ng'ombe.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kutumia fedha zake za ndani kujenga kwa kiwango cha lami baadhi ya miradi mikubwa ya barabara, badala ya kutegemea fedha toka nje, Serikali imejifunza kupata faida zifuatazo:-

(i) Hatua za maandalizi ya miradi inayofadhiliwa kutoka nje zinachukua muda mrefu na wakati mwingine miradi hiyo kufutwa kabisa ikilinganishwa na miradi inayogharamiwa na fedha zetu.

(ii) Kupunguza hali ya baadhi ya wafadhili kuchagua maeneo ya nchi wanayotaka wao kutoa fedha za miradi hivyo kuondoa dhana ya Serikali kuonekana inapendelea baadhi ya maeneo katika nchi yetu.

(iii) Kiasi cha fedha akinachoahidiwa na nchi wahisani ndicho kinachokuwa kigezo cha kiwango cha ubora wa kazi na si hali ya halisi ya mahitaji ya mradi husika.

(iv) Kutokana na masharti ya ufadhili, ni vigumu kujenga uwezo wa ndani na utaalam katika maandalizi na usimamizi wa miradi mikubwa. Aidha, ni vigumu kujenga uwezo wa ushiriki wa makandarasi wa ndani.

(v) Dhana ya kujitegemea inaweza kutafsiriwa kwa vitendo vya kuandaa, kugharamia na kusimamia miradi mikubwa sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara kwa kutumia mtindo wa kusanifu na kujenga (*Design and Build*) tuliyotumia kwenye baadhi ya miradi, umetupa changamoto inayohitaji kuzingatiwa na kufikiriwa kwa undani na kwa utaalam zaidi kabla ya kuendelea kutumia dhana hii katika miradi mingine ijayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrope swali la nyongeza.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ninapenda kuuliza kwamba kwa kuwa lengo langu katika kumwuliza swali ilikuwa kuiomba Serikali ione kwamba imechelewa kwa muda wa miaka mitano katika utekelezaji wa mradi huu yaani sasa kama wakimaliza 2010 ambapo mara ya kwanza waliahidi kwamba mradi ungekamilika 2005 ni miaka mitano hiyo.

Sasa Je, haiwezekani kwa kipande hiki cha Ndundu mpaka Somanga wakaweka wakandarasi wawili. Mmoja aanzie Somanga na mwingine aanzie Ndundu ili kazi hiyo iweze kufanyika kwa mapema zaidi?

Halafu la pili, ni kwamba niliwahi kuuliza katika Bunge hili kuhusu ubora wa lami inayowekwa hasa katika eneo la Chibite ambalo Mheshimiwa Waziri analifahamu sana. Nataka kumwarifu kwamba eneo lile sasa hivi hiyo lami imekwishaharibika kabisa. Je, Waziri atachukua hatua gani kwa mkandarasi yule na pia kwa viongozi wa *TANROADS* ambao udhaifu wao umesababisha wananchi watumie fedha zaidi kwa ajili ya kuwekeza pale na mpaka sasa hivi barabara hiyo kwa kweli inasikitisha wakati ukipita.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba tuweke wakandarasi wawili kati ya Ndundu na Somanga ili barabara ile ikamilike kwa haraka. Napenda ijulikane kwamba fedha hizo ni za ufadhili, na kwa maana hiyo zina kiwango ambacho tumefadhiliwa.

Kama mnavyojua wakandarasi wawili *items of mobilization* itakuwa ni gharama kubwa sana kuweka wakandarasi kwa kilomita zenye kilomita 60 gharama itapanda zaidi. Ndiyo maana tuliamua toka awali kwamba tuchukue mkandarasi mmoja na ndiyo utaratibu ambao hata mfadhili ameishaidhinishwa; na kwa kuwa kazi hii karibu inaanza, mimi niseme tu kwamba pamoja na kuchelewa tuwe na uhakika kwamba Serikali imedhamiria kukamilika barabara yote hiyo kama kilomita zaidi 350 zimebaki kilomita 60; na hizo kilomita 60 karibu zinaanza kujengwa tuwe na imani kwamba zitakamilika. Ni afadhali kuchelewa lakini tukamilishe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa lami. Kama ambavyo tuliwahi kujibu tatizo la ubora wa lami linaweza kweli likatokea kutokana na mkandarasi kutozingatia utaalam. Lakini vilevile inategemea uwezo uliokuwepo kwa maana ya fedha na hali halisi ya eneo ambalo linajengwa. Hata hivyo, suala hili liko kwa wataalam na tumewambia wajaribu kufanya kwa undani waone tatizo ni nini? Inawezekana kabisa si tatizo la mtu, lakini ni tatizo tu ambalo linatokana na hali halisi ya eneo lile na fedha iliyokuwepo kwa ajili ya kujenga. Baada ya kupata utafiti kamili tutaleta jibu ili Mheshimiwa Mbunge aweze kuelewa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Kuna matangazo. Nitaanza kwanza na wageni na mnivumilie kidogo kwa sababu wageni waliopo ni wengi kidogo na ni muhimu niweze kuwatumbulisha. Kwanza, mgeni wetu wa leo ni Mheshimiwa Regina Lowassa, Mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namwomba asimame. Ahsante sana. Karibu sana Mama Regina Lowassa. Unaendelea kuonyesha mfano mzuri, naomba na Mawaziri wengine wafuate mfano huu kwa sababu nyumba ni wawili. Sasa msiwe na mambo makubwa mnatoa hotuba wenzenu hawapo na hii ni kwa Mawaziri wote Wanawake na Wanaume. Mama Regina Lowassa amefuatana na wafuatao: - Kuna kijana Richard Lowassa, rafiki yangu sana huyo, ni mtoto wa Waziri Mkuu na ni mtoto mdogo tu, lakini anapenda sana kuhudhuria Bunge, na siku moja alininong'oneza kwamba lengo lake ni kuja kuwa Spika

wa Bunge. Karibu sana Richard, tunazidi kukuombea, hayo ni matarajio mema. Yupo pia Mama Beatrice Mumba mdogo wake Mama Regina Lowassa yuko pale, karibu sana na pia amesindikizwa na Mama Cecilia Mosha na Costa Moho wale pale, ahsante sana. Karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hao kuna familia ya Mheshimiwa Rita Mlaki. Yupo Mchalo Mlaki, Lawrence Mlaki, Joseph Mlaki, naomba wasimame ni watoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri Rita Mlaki. Wako kwenye *Press Gallery* na mmoja anasomea *Engineering* Mchalo, Lawrence anakwenda Chuo Kikuu na Joseph Mlaki yupo *University* India, sina uhakika kama kuna hata mmoja anayesomea taaluma ya Uandishi wa Habari, lakini wako kwenye *Press Gallery. (Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni kutoka nchi jirani na rafiki ya Malawi, wakiongozwa na Katibu wa Bunge la Malawi Mama M.M. Katapola ningemwomba asimame *Please madam*! *Thank you very much*. Ana mila kama zile za Kisukuma amepiga goti kidogo. *We welcome you madam, it is really pleasure to receive colleagues from Neighbouring Parliaments, it is greater honour. We wish you well in* Malawi *thank you*; *You and your delegation. Thank you*. Amefuatana na *delegation* ndefu kidogo ambao ni Mkurungezi wa Majengo wa Serikali ya Malawi, Mchoraji *Chief Architect*, Kampuni ya ABC *Designs.* Fununu nilizonazo ni kwamba wamevutia na ukumbi wetu na kwa hiyo wamekuja kuutazama ili kuona kama wanaweza kufanya kitu bora zaidi. Tunawatakia kila la kheri.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo tuna bahati ya kuwa na Wakuu wetu wa Mikoa wa Tanzania Bara na ninaona ni heshima kutokana na kazi kubwa sana wanayoifanya hapa nchini niwatambulishe mmoja mmoja. Nitaanza na Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Abbas Kandoro asimame tafadhali. Anashughuli kubwa kule za kupambana na wapiga debe. Mkoa wa Arusha Mheshimiwa Lt. Kanali Samuel Ndomba. Karibu sana. Mkoa wa Iringa Mheshimiwa Hajjat Amina Mrisho Said. Karibu sana na hongera sana kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mkuu wa Mkoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, utakuta katika baadhi ya vitabu pale sahihi yangu na mimi niliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa mwaka 1987. Mkoa wa Kagera Mheshimiwa Kanali Enos Mfuru. Mkoa wa Kigoma Mheshimiwa Kanali Joseph Simbakalia, Mkoa wa Lindi Mheshimiwa Said Mecky Sadiki yule pale. Mkoa wa Manyara Mheshimiwa Henry Shekiffu. Nadhani ana dharura.

Mkoa wa Mara Mheshimiwa Isidori Shirima. Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa John Mwakipesile. Wasilimie wote hadi Kyela kule. Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa *Major General* Said Kalembo. Mkoa wa Mtwara Mheshimiwa Kanali Mstaafu Anatory Tarimo. Mkoa wa Pwani Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma.

Mkoa Rukwa Mheshimiwa Daniel Ole Njolai. Mkoa wa Shinyanga Brigedia. General Mstaafu Dr. Johannes Balele. Mkoa wa Singida Mheshimiwa Parseko Ole Kone. Mkoa wa Tabora Abeid Mwin

Waheshimiwa Wabunge, Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Mohamed Babu. Sasa nyie mnataka na Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wakuu wa Mikoa. Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Dr. James Msekela. Mkoa wa Tanga, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz. Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa Monica Mbega na Mkoa wa Dodoma mwenyeji wetu Mheshimiwa William Lukuvi. Naona wamekamilika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao hawafanyi kazi peke yao wanao Makatibu Tawala nitawasoma haraka haraka na wasimame Arusha Nuru Milau; Dar es Salaam Beatha Swai, Dodoma Zawadieri Mchome, Iringa Bernard Nzungu, Kagera Peter Balie, Kigoma Martin Mgongolwa, Kilimanjaro Ndeshukurwa Sumari, Lindi Elisifa Mafole, Manyara Phinias Nkoo, Mara Chrisant Rugaimukamu Lubunga, Mbeya Asunta Ndimbo, Morogoro Godrefy Ngalea, Mtwara Alhaj Nassoro Kachechele, Mwanza Yahya Fadhili Mbila, Pwani Getrude Mpaka, Rukwa Innocent Mwenda, Shinyanga Joshua Kileo, Ruvuma Kaimu anaitwa Serungwi sijui ni mwanamume au mwanamke. Singida Daines Senyagwa, Tabora Seif Hassan Hussen na Tanga Paul Amani Richikila. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura Mbunge wa Tunduru ameniomba nitangaze kuwepo kwa wageni wake wafuatao nitawaomba wasimame kwa haraka haraka, na wote hao ni wamiliki wa viwanda vya korosho kote kule. Bwana Kirangi, Bwana Karamagi, Bwana Mapande, Bwana J. Haule, Bwana Hetashi, Bwana Banduka, ala amekuwa mjasiriamali ni yule yule Banduka. Ahsante sana naona Sera za CCM za Ujasiriamali zinafanya kazi kutoka Mkuu wa Mkoa kuwa Mjasiriamali. Bwana Abbas na Bwana Khamis Mkola.

Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah ameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wake Mheshimiwa Asha Bakari Makame ambaye ni Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania CCM. Karibu sana Asha Bakari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya vikao. Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa William Shellukindo ameniomba nitangaze kuwepo kwa mkutano wa Kamati ya Uwezekaji na Biashara leo saa saba kamili mchana katika ukumbi namba 432.

Kaimu Katibu wa Kamati ya Wabunge wa maeneo yanayolima korosho Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka katika maeneo yayozalisha korosho kwamba kutakuwa na mkutano saa mchana katika ukumbi namba 227.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli nyingine. Nadhani nimwite Katibu kwanza kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu kuongea. Nilikuwa napenda kufafanua kwamba kwa mujibu wa Kanuni zetu, taarifa kuhusu Wizara kwa maana ya Taarifa ya Kamati na Taarifa ya Kambi ya Upinzani huwa ni nusu saa. Lakini Ofisi ya Waziri Mkuu siyo Wizara ila ina Wizara kadhaa ndani yake . Sasa Kanuni zetu hazikuweka utaratibu mzuri wa kuzingatia hali hiyo. Kwa sababu tukizingatia kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inashughulikia mambo mengi sana pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo mara nyingine huwa ni Wizara.

Kwa hiyo, ninatumia mamlaka yangu chini ya Kanuni 126 kuitafsiri kanuni ya 81(1) inayoweka ukomo wa nusu saa kwamba taarifa ya Kamati kwa maombi ya wenyewe Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia Kambi ya Upinzani kwamba kwa kuzingatia uzito na shughuli zilizomo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, basi waweze kuchangia taarifa zao kwa muda usiozidi saa moja. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa muda usiozidi saa moja, na Kambi ya Upinzani kwa namna yoyote walivyojipanga kwa muda usiozidi saa moja. Baada ya kusema hayo, kwa heshima namwomba sasa Waziri aweze kuwasilisha hoja yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya Mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2006/2007 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2007/2008. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa maandalizi ya Makadirio haya kumetokana na ushirikiano na juhudi kubwa za viongozi na wataalam wa Wizara zote, Mikoa Halmashauri za Wilaya na Miji, mashirika ya umma na Taasisi mbalimbali. Aidha, makadirio haya yamekamilika kwa wakati kutokana na ushirikiano mzuri niliopata kutoka kwa viongozi wenzangu. Napenda kuwashukuru kwa namna ya pekee Mawaziri na Naibu Mawaziri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, Waziri wa Nchi, (Bunge na Uratibu), Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Naibu Waziri, (Mafa na Kampeni dhidi ya UKIMWI; na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Naibu Waziri,

(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). Wote hawa wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru vilevile wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu Bwana Vincent Mrisho na Bibi Maimuna Tarishi. Nawashukuru pia Naibu Katibu Mkuu Bwana Michael Mwanda na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu, Bwana Wilson Mukama ambaye sasa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ushauri wao wa kitaalam uliofanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, naomba nitambue michango ya Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mameya, Wenyeviti na Wakurugenzi wa Halmashauri katika maandalizi ya bajeti hii. Vilevile, namshukuru kipekee Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwa maoni na ushauri wao waliotupatia. Maoni hayo yamesaidia sana kuboresha Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, nawashukuru wajumbe wa Kamati za Kudumu za Buge lako Tukufu kwa kupitia na kukubali Makadirio ya Matumizi ya kila Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na asasi zilizo chini ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi za pekee na kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Mbunge, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; kwa hotuba zao nzuri sana. Nawapongeza kwa jinsi walivyoweza kufafanua kwa kina hali ya uchumi na mapato na matumizi katika kipindi kilichopita na kutoa mwelekeo wa mpango wa bajeti kwa kipindi kijacho, walifanya kazi nzuri sana. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana waliyoitoa wakati wa mchakato wa kuandaa na kujadili bajeti. Michango hiyo itaisaidia Serikali wakati wa utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Mwaka 2007/2008. Vilevile, nawashukuru kwa dhati Wabunge wote kwa kuipitisha Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, nchi yetu ilishuhudia matukio mbalimbali ya ajali za vyombo vya usafiri ikiwemo ajali ya ndege iliyotokea Mbeya Mjini. Ajali hiyo ilisababisha kifo cha aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Tunduru, Hayati Juma Jamaldin Akukweti, pamoja na wafanyakazi watatu wa Serikali ambao ni Bibi Theresia Nyantori, Mwandishi wa Habari wa Idara ya Habari; Bwana Nathaniel Katinila, Mratibu wa Mradi wa Masoko; na Bwana George Bendera, Afisa Habari Idara ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, nafurahi kusema Bwana Nisetas Kanje, Katibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Bunge na Uratibu); na rubani wa ndege hiyo Bwana Martin Sumari waliokuwa katika ndege ile sasa wanaendelea vizuri na afya zao.

Aidha, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao katika ajali mbaya ya basi la *Mohammed Trans* iliyotokea eneo la Kisaki Mkoani Singida tarehe 15 Juni 2007, na ile iliyotokea kwenye Jimbo langu la Uchaguzi eneo la Meserani Mkoani Arusha, tarehe 23 Juni 2007. Natoa pole vilevile kwa ndugu wa familia ya wajumbe watatu walioteuliwa hivi karibuni na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuimarisha Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza, waliofariki katika ajali ya gari iliyotokea jana tarehe 24 Juni 2007 karibu na Mji wa Singida.

Wajumbe hawa ni aliyekuwa Mbunge wa Mwanza Mjini Marehemu Stephen Kazi - Mwanaushirika wa siku nyingi, Marehemu William Kasubi na Mkuu wa Wilaya mstaafu Marehemu Ndonyo Henziron. Wajumbe hawa walikuwa wanakuja Dodoma kuonana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kuhusu majukumu waliyopewa ya kutumia ujuzi na uzoefu wao kuimarisha Bodi ya Chama Kikuu Ushirika cha Nyanza. Vilevile, natoa pole na kuwatakia majeruhi wote afya njema na Mwenyezi Mungu awasaidie wapone haraka. Mungu azilaze roho za Marehemu wote mahali pema peponi na kuendelea kuwapa afya njema walionusurika katika ajali hizo. Amen!

Mheshimiwa Spika, ningependa Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa jumla tutafakari hizi ajali zimezidi sana, tufanye nini ili kuokoa maisha ya binadamu wenzetu yanayopotea mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika**,** baada ya mwaka wa kwanza wa uongozi wa Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, yapo mafanikio yanayoweza kupimika katika baadhi ya sekta. Hata hivyo, kasi ya mafanikio hayo imepungua kutokana na changamoto tulizokabiliana nazo katika kipindi hicho. Changamoto hizo ni pamoja na ukame, uhaba wa umeme, kupanda kwa bei ya mafuta, uharibifu wa miundombinu, Homa ya Bonde la Ufa na uhaba wa shule za sekondari za kutosheleza wanafunzi waliofaulu elimu ya msingi. Serikali ilifanikiwa kukabiliana na changamoto hizo licha ya kuwa ziliathiri malengo tuliyojiwekea hususan kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Hivyo, Bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2007/2008 itaendeleza juhudi za kukuza uchumi na kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, hali ya Siasa, mazingira mazuri ya kisiasa ni nguzo muhimu na yenye kujenga mazingira bora ya kukua kwa uchumi na ustawi wa jamii. Hii ni pamoja na kuwepo kwa amani, utulivu na utawala wa sheria. Nchi ikiwa na utulivu wa kisiasa huwezesha wananchi wake kushiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na utoaji huduma zinazowezesha uchumi kukua.

Hali hii pia huwezesha na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza mitaji yao bila woga. Aidha, wananchi hupata fursa ya kushiriki katika shughuli za kisiasa na za kijamii kwa njia za kidemokrasia. Ninawapongeza viongozi wa vyama vya siasa pamoja na wananchi wote kwa kudumisha amani na utulivu nchini, licha ya tofauti za imani na za kiitikadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Serikali imeendelea kuratibu shughuli za vyama vya siasa na kuhakikisha vinafuata Sheria ya Vyama vya Siasa, Katiba na Kanuni za vyama vyao. Maombi ya usajili yaliendelea kushughulikiwa ambapo Chama cha *The Tanzania Peoples Organization for Democracy and Development (TAPODD)* kilipata usajili wa muda. Aidha, Chama cha *National Democratic Party for Rehabilitation (NDPR*-MAREJESHO) kilijitoa kwa kushindwa kutimiza masharti. Chama cha *FORD* kilipoteza sifa ya usajili kwa kushindwa kufanya chaguzi za viongozi wapya na hivyo taratibu za kukiondoa kwenye Daftari la Usajili wa Vyama vya Siasa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika**,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia mwaka 2007/2008, Serikali itatoa ruzuku kwa vyama vyenye Madiwani. Kiasi cha shilingi bilioni tatu kimetengwa kwa ajili ya madhumuni hayo. Ni matumaini ya Serikali kuwa ongezeko hilo la ruzuku kwa vyama vya siasa litaviwezesha kujijenga na kujiimarisha ili viweze kutoa mchango wao katika kuimarisha demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika**,** uchaguzi, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, nchi yetu ilifanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika jimbo la Tunduru na chaguzi ndogo za Madiwani katika kata 14 nchini. Katika uchaguzi mdogo wa Ubunge katika jimbo la Tunduru, vyama vitano vya siasa vilishiriki. Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, (Mb) kupitia Chama Cha Mapinduzi alichaguliwa kwa kura 35,876, sawa na asilimia 62 ya kura zote zilizopigwa. Chama cha CUF kilipata kura 18,124, *CHADEMA* kura 2,165, *UDP* kura 123 na *DP* kura 101.

Kwa mara nyingine, nampongeza Mheshimiwa Mtutura aliyeshinda uchaguzi huo na kujiunga na Bunge lako Tukufu tangu Mkutano wa Saba wa Bunge, Aprili mwaka huu. Kufuatia chaguzi za Madiwani katika Kata mbalimbali nchini, jumla ya vyama saba vilishiriki ambapo Chama Cha Mapinduzi kilishinda katika Kata 14 na *CUF* katika kata moja. Nachukua fursa hii pia kuvipongeza vyama vya siasa vilivyoshiriki kwenye chaguzi hizo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** Tume ya Uchaguzi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuwezesha uchaguzi mdogo wa Tunduru na chaguzi ndogo mbalimbali za Madiwani kufanyika kwa amani. Katika mwaka 2007/2008, Serikali itaendelea kuijengea Tume ya Uchaguzi uwezo wa kirasilimali ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa lengo la kukuza demokrasia, amani, mshikamano na utulivu. Aidha, Tume ya Uchaguzi itaanza kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kuingiza wale waliotimiza sifa za kujiandikisha na ambao hawakujiandikisha katika kipindi kilichopita. Serikali imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Bunge. Bunge hili ni mhimili muhimu wa jamii ya Watanzania. Bunge hili ndilo kielelezo cha uhai wa demokrasia nchini. Majukumu ya Bunge hili yanagusa maisha ya kila siku ya wananchi wetu.

Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Shughuli za Bunge zimefanyika kwa msisimko mkubwa wa michango kutoka pande mbili hapa Bungeni, yaani Kambi ya Chama Tawala, CCM na Kambi ya Vyama vya Upinzani. Msisimko huo umedhihirisha kuwepo uhai na demokrasia ya vyama vingi vya siasa katika Bunge letu.

Nitumie fursa hii kukupongeza sana Mheshimiwa Spika wewe binafsi, kwa uongozi wako mahiri uliofanikisha uhai wa demokrasia ndani ya Bunge letu. Aidha, nawapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa msaada wao katika kufanikisha ujenzi wa demokrasia ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2007/2008, Serikali itaendelea kushirikiana na Bunge ili kulijengea uwezo wa kumudu majukumu yake. Jukumu hili litaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na uwezo wa rasilimali tulizonazo. Serikali inatambua umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge kuwa na Ofisi zenye hadhi kwenye majimbo yao ya uchaguzi. Kwa kuanzia, Serikali imetenga fedha zitakazowezesha kujenga ofisi 40 za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali ina mtandao wa ngazi mbalimbali hadi vijijini, jukumu la kujenga na kuzitunza ofisi hizo litakuwa ni la Halmashauri za Wilaya. Aidha, Serikali imeridhia uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo baada ya kupata uzoefu wa nchi za Kenya na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwa njia ya pekee kwamba tutaleta sheria hapa kabla ya Bunge hili kuahirishwa ya kuelezea utaratibu wa kutumiwa na Mfuko huo wa Maendeleo ya Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu umeendelea kuimarika kwa sababu ni Muungano wa watu. Masuala machache ya kitaasisi yenye kusababisha kero na vikwazo kwa wananchi yataendelea kutatuliwa kwa mazungumzo na makubaliano ya pamoja.

Hata hivyo, napenda kusisitiza kuwa kwa vile Muungano huu ni hai, na kwa vile mabadiliko mbalimbali yanatokea kwa sababu za utandawazi na teknolojia, matatizo yanayojitokeza yataendelea kutatuliwa. Jambo muhimu ni mshikamano na umoja wetu katika kuyashughulikia. Dhamira ya Serikali zetu mbili ni kuondoa mambo yanayoleta vikwazo kwa kuhakikisha yanatatuliwa ipasavyo ili Muungano uendelee kuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya uchumi katika ngazi ya Kitaifa na kijamii. Katika ngazi ya Kitaifa, Serikali ilidhamini mikopo ya mabenki kwa wananchi kupitia Mifuko ya Dhamana kwa Miradi ya Muda Mrefu na wa Kati *(Development Finance Guarantee Facility),* Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi *(Export Credit Guarantee Scheme),* na Mfuko kwa ajili ya Biashara Ndogo Ndogo *(SME Credit Guarantee Scheme)* inayoratibiwa na Benki Kuu. Maelezo ya kina kuhusu mifuko hiyo yalitolewa na Waziri wa Fedha wakati wa kuwasilisha Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wananchi katika ngazi ya kijamii, Serikali iliendelea kutekeleza Mipango na Programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo, Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa, Mpango wa Kurasimisha Mali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA).

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 21 zilitengwa na kila Mkoa ulitarajiwa kupata mgawo wake wa shilingi bilioni moja kwa ajili ya wajasiriamali ili kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kupitia mikopo ya masharti nafuu. Napenda kurudia tena kwamba kila Mkoa unao shilingi bilioni yake moja, kila Mkoa. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2007, wajasiriamali 6,765 kupitia Benki ya *CRDB* walipata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.3 na wajasiriamali 15,024 kupitia *NMB* walichukua mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.6. Fedha hizo zilitolewa kwa mtu mmoja mmoja, vikundi na Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS).*

Hata hivyo, kumekuwepo na dhana potofu kuhusu fedha hizo. Wapo wanaodhani kwamba fedha hizo ni zawadi na hawawajibiki kuzilipa. Napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha tena wananchi kwamba fedha hizo zinapaswa kurejeshwa ili wananchi wengine waweze kukopeshwa. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote kutumia fursa zilizopo ili kuondokana na umaskini. Tutumie nguvu ya umoja kupitia Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS),* kwani umoja ni nguvu. *SACCOS* zinazoendeshwa kwa kutumia kanuni bora za ushirika zinatoa matumaini ya kuondokana na umaskini katika kipindi kifupi. Vile vile, zinajenga misingi endelevu na uhusiano wa kuaminika kukopeshwa na benki.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kama njia mojawapo ya kukuza uchumi vijijini na kuondoa vikwazo vinavyohusu uendeshaji wa mfumo wa soko la mazao ya kilimo. Programu hiyo inatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Manyara, Arusha, Tanga, Iringa, Kilimanjaro na Ruvuma. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, programu imewezesha kuandaa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo. Aidha, imewawezesha wakulima, wafanyabiashara na wasindikaji mazao wadogo kuwa wajasiriamali na kuwaunganisha na watoa huduma za kifedha. Vile vile, programu imewawezesha wananchi kukarabati miundombinu ya masoko vijijini pamoja na barabara.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ya programu hii ni utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika Wilaya za Babati, Hanang, Mbarali, Mbeya Vijijini na Sumbawanga Vijijini. Mfumo huu umeonyesha mafanikio makubwa kwa kuwawezesha wakulima kutumia mazao yao kama dhamana ya kupata mikopo kutoka benki wakati wanasubiri bei za mazao yao ziwe nzuri. Hadi kufikia mwezi Mei 2007, wakulima 879 wameweza kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.2 kwa kutumia Stakabadhi za Mazao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, programu itaanza kutekeleza shughuli zake katika Wilaya za Korogwe, Moshi, Mwanga, Simanjiro, Chunya, Ileje, Kyela, Makete na Njombe. Programu itaibua, kuhamasisha na kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika maeneo ya Kyela, Madibira - Mbarali, Mpitimbi – Songea Vijijini, Mbulu, Monduli na Mbozi. Aidha, Programu itawezesha kukarabati kilomita 100 za barabara za vijijini. Vile vile, ujenzi wa masoko ya Mtindiro (Muheza), Kiwira (Rungwe), Hedaru (Same), Tunduma (Mbozi), Dongobesh (Mbulu), Makita (Mbinga), Tarakea (Rombo) na Namanyere (Nkasi) utakamilishwa. Programu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko itaanza kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, programu ya Huduma ya Kifedha Vijijini inalenga kuwawezesha wakulima wadogo au kaya zenye kipato kidogo kuwa na kipato endelevu, mali na uhakika wa chakula kwa kuwahamasisha kujijengea utaratibu wa kuweka akiba kwa shughuli za uzalishaji.

Aidha, Programu inalenga zaidi kuwashirikisha wanawake na vijana vijijini kujiunga katika vikundi imara vya kuweka akiba na kukopa *(SACCOS* na *SACAS)*. Programu inatekelezwa katika Wilaya 22 za mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Dodoma, Singida na Kilimanjaro. Katika mwaka 2006/2007, *SACCOS* 125 zilinufaika na programu hii ikilinganishwa na *SACCOS* 80 mwaka 2005/2006. Ongezeko hili la *SACCOS* 45 ni sawa na asilimia 56. Pia, programu ilitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi 1,840 kutoka *SACCOS* 230 ili kuwawezesha kuelewa masuala ya ushirika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, programu hii itaziongezea *SACCOS* uwezo wa uendeshaji kwa kuboresha utoaji na usimamizi wa mikopo, kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Mikopo za *SACCOS* na Maafisa wa Mikopo wa kufuatilia mikopo hiyo. Natoa wito kwa wananchi katika maeneo ya programu kujiunga na *SACCOS* ili wanufaike na mikopo inayotolewa na asasi hizo kwa lengo la kushiriki katika kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar umetekeleza jumla ya miradi 1,647. Miradi hii yenye gharama ya shilingi bilioni 48.7 imechangiwa pia na wananchi. Miradi 623 ni ya elimu, 225 afya, 185 mifugo, 112 maji, 32 ustawi wa jamii, 24 chakula, 17 misitu, 16 masoko, 9 uvuvi, mitatu umwagiliaji na mmoja ushirika. Mfuko ulitoa mafunzo ya utoaji taarifa na ufuatiliaji miradi kwa Wajumbe wa Serikali za vijiji 617, Kamati za Mitaa 249, Mabaraza ya Ushauri ya sheria 19 na watoa huduma za kitaalamu 10.

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wananchi kwa kuibua na kuchangia miradi mingi. Aidha, nawapongeza *TASAF* kwa kuharakisha utoaji wa fedha na hivyo kuwezesha wananchi wengi kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Mfuko wa *TASAF* utapitia maombi ya fedha za kutekeleza miradi takriban 2,000. Mfuko utatoa mafunzo

kwa wanachama 10,000 wa vikundi vya kuweka akiba na kukopa, ufuatiliaji wa miradi ya jamii, kutoa ushauri na kujenga uwezo wa jamii zitakazotekeleza miradi ya *TASAF* katika Wilaya zote nchini. Aidha, utawezesha kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii katika Mikoa ya Mwanza, Morogoro, Arusha na katika Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Kiuchumi, barabara za Kitaifa katika mwaka 2006/2007, barabara kuu zenye urefu wa kilomita 318 za kiwango cha lami zilijengwa. Aidha, barabara kuu za lami zenye urefu wa kilomita 78 na kilomita 153.5 za changarawe zilikarabatiwa. Kuhusu barabara za mikoa, kilomita 368 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na kilomita 15 zilikarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, matatizo yaliyokuwa yakikabili Programu ya Mradi Maalumu wa Barabara Kuu za Ukanda wa Kati na Kusini Mashariki yalitafutiwa ufumbuzi na kuwezesha utekelezaji kuendelea ipasavyo na barabara hizo sasa wako makandarasi kazini wanaendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inavyoelekeza, Serikali katika mwaka 2007/2008 imechukua hatua za dhati kuimarisha Mfuko wa Barabara kwa kutenga jumla ya shilingi bilioni 218.474. Kiasi hiki ni mara mbili na nusu ya kiwango cha shilingi bilioni 85.693 zilizotengwa mwaka 2006/2007. Asilimia 90 ya fedha hizi zitatumika kuzifanyia matengenezo barabara na madaraja katika mtandao wa barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara na zile zinazotekelezwa na Halmashauri za Wilaya nchini.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Wizara, Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wakala wa Barabara na Halmashauri za Wilaya ni kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Serikali za Mitaa, Serikali imeendelea kuboresha mtandao wa barabara zilizo chini ya Serikali za Mitaa ili kuchochea maendeleo vijijini na kuondoa umaskini. Hatua hii inarahisisha usafiri wa wananchi na usafirishaji wa bidhaa, pembejeo na mazao ya kilimo. Ili kufikia azma hiyo, katika mwaka 2006/2007, Serikali za Mitaa zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 25.3 kutoka katika Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 10,014. Hadi kufikia mwezi Aprili 2007, jumla ya shilingi bilioni 19.3 zilikuwa zimepelekwa katika Serikali za Mitaa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo. Kazi zilizofanyika ni matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 3,181. Katika mwaka 2007/2008, Serikali imetenga shilingi bilioni 65.5 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri ili ziweze kupitika wakati wote. Suala la msingi sasa ni uwezo wa Halmashauri kutumia fedha hizo kwa ajili ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usafiri na Usafirishaji katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam lina nafasi ya pekee katika uchumi wa nchi yetu. Kukua kwa kasi kwa Jiji hili kumesababisha ongezeko la tatizo la usafiri na usafirishaji Jijini. Serikali imeanza kuchukua hatua za kukabiliana nalo ili kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii katika Jiji zisiathirike. Zipo hatua za muda mfupi, wa kati na muda mrefu za kukabiliana na tatizo hilo. Hatua za muda mfupi zilizoanza kuchukuliwa na Mamlaka ya Jiji, Manispaa, uongozi wa Mkoa na wadau wengine ni pamoja na kutumia kwa ufanisi zaidi barabara zenye njia nne nyakati za msongamano wa magari asubuhi na jioni. Hatua nyingine ni

pamoja na kuimarisha usimamizi wa sheria za usalama barabarani na kutengeneza taa za kuongozea magari. Barabara ndogo zinazoingia na kutoka barabara kuu zitakarabatiwa kwa viwango vya changarawe wakati zikisubiri kujengwa kwa kiwango cha lami. Baadhi ya barabara hizo ni Twiga - Jangwani - Kigogo hadi Tabata Dampo; Vingunguti hadi Segerea; Afrikana hadi Njia Panda ya Kawe; Kigogo hadi Ubungo Maziwa; na *Jet Club - Davi's Corner* hadi Mtongani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua za muda wa kati ni kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo kasi. Mradi huu unalenga kuweka mfumo wa usafiri utakaotumia mabasi makubwa yenye uwezo wa kubeba abiria kati ya 140 na 160 kwenye barabara kuu. Vile vile, kuwa na mabasi ya ukubwa wa kati yenye uwezo wa kubeba abiria kati ya 50 na 80 kwenye barabara ndogo za Jiji. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huu. Miundombinu itakayojengwa ni njia maalumu za mabasi, vituo vya mabasi, stesheni na karakana. Wakala wa kusimamia utekelezaji wa mradi, *DART Agency* umekwishaundwa. Mfumo wa uendeshaji wa mradi huu utajumuisha Serikali na sekta binafsi. Hatua nyingine ni kuandaa utaratibu wa magari makubwa ya mizigo na bidhaa za vyakula yanayoingia jijini yaishie nje ya mji wakati wa asubuhi na jioni ambapo kuna msongamano mkubwa wa magari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo Jiji la Dar es Salaam linaendelea kutekeleza mikakati ya muda mrefu kama ifuatavyo:-

(a) Kutayarisha mpango kabambe wa usafirishaji na uchukuzi Jijini (2008 – 2030) chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan. Tayari wataalamu wa *JICA* wameanza kazi hiyo kwa kufanya upembuzi yakinifu;

(b) Kutambua na kujenga barabara za mzunguko *(ring roads)* na barabara ndogo ndogo za kupunguza msongamano;

(c) Kushirikisha watu binafsi kuandaa maeneo ya kuegesha magari nje ya Jiji, mfano Tegeta na Ubungo; na

(d) Kuanzisha miji midogo *(satellite towns)* pembeni mwa Jiji la Dar es Salaam ambayo itakuwa na huduma zote muhimu.

Kwa kutambua kuwa Dar es Salaam ni kitovu kikuu cha uchumi wa Taifa, maboresho ya usafiri yanayoendelea Jijini Dar es Salaam yanapaswa kuungwa mkono na wananchi wote wa Jiji, kwa vile athari za usafiri zilizopo zinapunguza uzalishaji na kuchelewesha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za uzalishaji, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta zenye uwezo mkubwa wa kukuza uchumi iwapo juhudi za kutangaza vivutio vyetu zitaongezwa. Idadi ya watalii wanaoingia nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2006 watalii 644,124 waliingia nchini ikilinganishwa na watalii 612,754 katika mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia tano. Ongezeko hili lilitokana na juhudi za kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyoko nchini, kuimarisha

usalama kwa watalii pamoja na uwekezaji katika sekta ya utalii inayojumuisha hoteli, usafiri na uwindaji. Biashara ya utalii ina ushindani mkubwa duniani, hivyo, hapana budi kwa wananchi na wadau wanaotoa huduma katika sekta hii kufanya kazi kwa kuzingatia utaalamu na mwenendo mzuri unaovutia watalii.

Katika mwaka 2007/2008, Serikali itaimarisha usalama kwa watalii na mali zao na kujenga mazingira mazuri ya kutangaza vivutio vya utalii nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishati. Katika mwaka 2006/2007, Serikali imefanikiwa kurejesha uzalishaji wa umeme katika hali ya kawaida. Jitihada za hifadhi ya mazingira katika vyanzo vya maji pamoja na mvua zilizonyesha msimu wa mwaka 2006/2007 zilichangia kujaza mabwawa ya kuzalisha umeme. Changamoto kubwa kwa Serikali ni kuwafikishia umeme wananchi wengi waishio vijijini. Hivyo, kuna umuhimu wa kuharakisha utekelezaji wa mpango wa kusambaza umeme vijijini na kuongeza matumizi ya nishati mbadala itokanayo na mimea, wanyama, jua na upepo. Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi, lipo tatizo la hujuma za uharibifu wa miundombinu ya nishati ambayo Serikali imewekeza kwa gharama kubwa. Kumekuwepo na matukio ya mara kwa mara ya wizi wa mafuta ya transfoma, nyaya za umeme na vyuma vya nguzo za umeme hali ambayo inaathiri utoaji wa huduma ya umeme na vile vile kuhatarisha maisha ya watu na uzalishaji mali. Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2003 na 2006 gharama za transfoma zilizoibiwa mafuta na kuharibika ni shilingi bilioni 1.8, nyaya za umeme zilizoibiwa ni shilingi milioni 852.2 na vyuma vya nguzo ni shilingi milioni 337.

Napenda kutoa wito kwa wananchi wawe walinzi wa maeneo yao kwa kuwafichua wahalifu wote ili waweze kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria. Aidha, wateja wa *TANESCO* wanadaiwa malimbikizo ya madeni ya shilingi bilioni 234. Wadaiwa wote wa *TANESCO* wanatakiwa kulipa gharama za huduma wanazotumia ili kulipa Shirika uwezo wa kuendelea kuboresha huduma zake.

Mheshimiwa Spika, Madini. Kutokana na mazungumzo yanayoendelea kati ya Serikali na Kampuni za uchimbaji madini nchini, makubaliano ya kurekebisha baadhi ya vipengele vya mikataba baina ya Serikali na baadhi ya Kampuni za Madini yamefikiwa. Serikali imesaini nyongeza ya makubaliano ya mikataba hiyo ili kuiwezesha nchi kunufaika zaidi na uwekezaji katika sekta hii. Mafanikio yaliyopatikana katika baadhi ya vipengele ni:-

(a) Kuondolewa kwenye mikataba baadhi ya vipengele, kama vile nyongeza ya asilimia 15 kwenye mtaji wa uwekezaji ambao haujakombolewa. Hatua hii itasababisha kampuni kuanza kulipa kodi ya mapato mapema zaidi;

(b) Kuanza kulipwa kwa kodi ya Halmashauri kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 200,000 kwa mwaka kwa kila Halmashauri yenye mgodi. Halmashauri zitakazonufaika ni Tarime, Kahama, Nzega, Geita na Biharamulo. Kati ya hizo, Halmashauri za Kahama, Biharamulo na Tarime zimeshaanza kulipwa;

(c) Kampuni ya *Barrick Tanzania Limited* kuanza kulipa kwa hiari Dola za Kimarekani milioni saba kila mwaka kwenye mfuko wa uwezeshaji; na

(d) Kampuni ya *Resolute (T) Limited* kuanza kulipa kwa hiari Dola za Kimarekani milioni mbili kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali itaendelea na mazungumzo na kampuni zilizobaki. Natoa wito kwa kampuni za madini zilizoko nchini kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha pande zote zinanufaika na madini yanayochimbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* iliendelea kwa kujenga uwezo wa Halmashauri katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* na kutathmini utekelezaji wake, kuimarisha huduma za ugani na utafiti, na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa mwaka 2005/2006 ulifikia tani milioni 10.9 na kukidhi mahitaji ya Taifa ya chakula kwa asilimia 112 kwa mwaka 2006/2007.

Aidha, Serikali ililenga kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kwa jumla ya hekta 10,000. Hadi mwezi Mei 2007, jumla ya hekta 7,063 zimeendelezwa.

Katika mwaka wa 2007/2008, Serikali imelenga kuongeza eneo la umwagiliaji kwa jumla ya hekta 20,000 ambapo hekta 17,000 zitatokana na miradi iliyopo ya umwagiliaji na hekta 3,000 zilizobaki zitatokana na ujenzi wa mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali ilitenga shilingi bilioni 19.5 za ruzuku kwa ajili ya mbolea na mbegu bora. Hadi mwezi Aprili 2007, jumla ya tani 110,836 za aina mbalimbali za mbolea zilifikishwa katika vituo vikuu 24 vya kusambazia mbolea katika mikoa yote na tani 86,000 zimeuzwa kwa wakulima. Aidha, jumla ya tani 925 za mbegu bora za mahindi na mtama zenye ruzuku zimepokelewa katika vituo vikuu 24 vya usambazaji na tani 368 zimeuzwa. Hata hivyo, Serikali imebaini kwamba utaratibu uliopo wa usambazaji wa mbolea hauwanufaishi ipasavyo wakulima bali wafanyabiashara wa kati. Hivyo, Serikali inatafuta utaratibu mzuri zaidi wa kuhakikisha kuwa ruzuku inayotolewa kwa pembejeo za kilimo inawafikia na kuwanufaisha wakulima moja kwa moja.

Mwaka 2007/2008, Serikali itapanua ruzuku ya pembejeo ili ijumuishe mbolea, mbegu bora, dawa na miche. Jumla ya tani 89,323 za mbolea za aina mbalimbali; mbegu bora za mahindi na mtama tani 3,000; miche milioni 10 ya chai na kahawa na dawa za korosho vitatolewa kupitia mpango wa ruzuku. Aidha, Serikali itaajiri wataalamu wa ugani 2,500 ili kuboresha huduma za ugani nchini. Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri wahakikishe kuwa mbolea, mbegu bora na dawa za mimea zinawafikia wakulima kwa wakati. Napenda kusisitiza wananchi kuzingatia maelekezo ya kitaalamu yanayotolewa ili kuongeza tija na ubora wa mazao.

Mheshimiwa Spika, huduma za jamii, elimu ya msingi. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa watoto wote wanaostahili kuingia shule wanafanya hivyo. Jitihada za Serikali za kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kuandikishwa shule wanaandikishwa zimeonekana kwa idadi ya wanafunzi katika shule za msingi kuongezeka kutoka 5,981,338 mwaka 2002 hadi kufikia wanafunzi 7,959,884 mwaka 2006. Juhudi hizo za Serikali, wananchi na wadau mbalimbali zimewezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa katika kufikia lengo la elimu la milenia la kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kuandikishwa shule wanaandikishwa kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kufikia lengo hili, kwani hadi Januari, 2007 wameandikishwa wanafunzi milioni 1.2, sawa na asilimia 96.1. Napenda kuwapongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Halmashauri pamoja na Wakuu wa Wilaya kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, inakadiriwa kuwa Tanzania itafikia lengo la elimu la milenia mapema zaidi kabla ya mwaka 2015, na maelekezo yaliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mapema zaidi kabla ya mwaka 2010. Tatizo tulilonalo sasa ni kudhibiti vitendo vya utoro na mimba shuleni ambavyo vimekuwa vikiongezeka kwa kasi kwa kipindi cha mwaka 2002 hadi 2006. Kwa mfano, takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2002, wanafunzi waliokatisha masomo walikuwa 36,680 ikilinganishwa na wanafunzi 48,221 mwaka 2006. Ni wajibu wa viongozi wote, wazazi na wananchi kwa ujumla kusaidia jitihada za Serikali kukomesha tabia za utoro na kuwakatisha wanafunzi masomo kwa kuwapa mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya sekondari kutokana na mafanikio ya MMEM, yaliyosababisha idadi ya wanafunzi waliofaulu elimu ya msingi kuongezeka, Serikali ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009) ukiwa na lengo la kuongeza uwiano wa wanafunzi wanaohitimu vizuri elimu ya msingi na kujiunga na elimu ya sekondari. Chini ya mpango huu, idadi ya wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka 243,359 mwaka 2006 hadi kufikia 401,011 mwaka 2007 sawa na ongezeko la asilimia 65.

Aidha, wanafunzi waliojiunga na kidato cha tano katika Shule za Sekondari za Serikali imeongezeka kutoka 15,509 mwaka 2005 hadi 18,211 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la wanafunzi 2,702 sawa na asilimia 17.4. Katika mwaka 2007/2008, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine wa elimu itachukua hatua za kuhakikisha kuwa ubora wa elimu ya sekondari unakuwa wa hali ya juu kwa kukamilisha ujenzi wa majengo, maabara na kuajiri walimu wa kutosheleza. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi atatoa maelezo zaidi kuhusu mikakati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu ya juu, utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Juu, Sera ya Ufundi na Mafunzo, Sera ya Sayansi na Teknolojia pamoja na mpango kabambe umewezesha mabadiliko kuanza kuonekana katika sekta hii ya elimu. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya umma na binafsi inaongezeka. Kwa mfano, kwa mwaka 2006/2007, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu imefikia 68,929 ikilinganishwa na wanafunzi 55,134 mwaka 2005/2006. Hili ni ongezeko la wanafunzi 13,795 sawa na

asilimia 25. Serikali imeweka mazingira yanayowezesha sekta binafsi yakiwemo mashirika ya dini kuanzisha vyuo vikuu. Serikali imeanza kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa Chuo Kikuu kipya cha Dodoma kinaanza kudahili wanafunzi katika mwaka wa masomo 2007/2008. Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia atatoa maelezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali kupitia Mfuko wa *TASAF* imejenga jumla ya zahanati 225. Pamoja na kazi hii nzuri zahanati hizi nyingi zake hazina wataalamu wa kutosha. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali inakusudia kuajiri wataalamu ili kukidhi mahitaji ya zahanati hizo mpya. Katika hatua nyingine, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Afya ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Mahitaji hayo yanajumuisha kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na kuhakikisha kuwa huduma za rufaa nchini zinaimarishwa ili kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi. Katika kutekeleza sera hiyo, mwaka 2007/2008, Serikali itakamilisha mpango wa ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila Kata na itaendelea kutoa mafunzo ya wafanyakazi kwa ajili ya zahanati na vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi kamili wa zahanati na vituo hivyo utaanza mwaka 2008/2009 kwa kutumia dhana ya ushirikishwaji wa wananchi kama ilivyotumika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Ningependa ieleweke kwamba tumeamua kutumia huu wa kwanza kuajiri watumishi na kupata vifaa kwa vile vituo vya afya ambavyo vimejengwa kupitia utaratibu wa *TASAF.* Halafu mwaka unaofuata ndiyo na sisi tunaanza kujenga. *(Makofi)*

Aidha, ujenzi wa zahanati na vituo hivyo, unatarajiwa kukamilika mwaka 2009/2010. Napenda kusisitiza umuhimu wa viongozi wa Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Kata na Vijiji kushirikiana na wananchi ili kufanikisha mpango huo. Pamoja na hatua hizi muhimu, Serikali imechukua hatua za kuanza kukarabati Hospitali za Mikoa nchini. Kwa kuanzia, katika mwaka 2007/2008, Serikali itakarabati Hospitali 11 za Mikoa ya Tabora, Lindi, Dodoma, Kigoma, Shinyanga, Singida, Rukwa, Mara, Iringa, Ruvuma na Tanga. Vile vile, Mfuko wa Bima ya Afya umetenga fedha za kujenga majengo katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma yatakayotumika kutoa huduma za hadhi ya daraja la kwanza kwa wagonjwa ili kukidhi mahitaji makubwa yanayoongezeka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji katika mwaka 2006/2007, Serikali imetekeleza miradi mbalimbali ya maji safi nchini. Matokeo ya utekelezaji huo ni kuongezeka upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wakazi wa vijijini kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005/2006 hadi asilimia 55.68 mwaka 2006/2007. Aidha, upatikanaji wa huduma ya maji safi mijini katika Makao Makuu ya Mikoa umeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2005/2006 hadi kufikia asilimia 78 mwaka 2006/2007. Ongezeko la huduma kwa viwango hivyo katika kipindi cha mwaka mmoja linadhihirisha ikilinganishwa na malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ambayo yanalenga kufikia asilimia 65 ya huduma ya maji vijijini na asilimia 90 maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2010. *(Makofi)*

Pamoja na mafanikio hayo Mamlaka za Majisafi na Majitaka mijini zinakabiliwa na tatizo kubwa la kutolipwa na wateja wake. Wadeni wakubwa wa mamlaka hizo ni Wizara na Taasisi za Serikali ambazo kwa pamoja zina madeni yaliyofikia shilingi bilioni 1.65 hadi mwezi Mei, 2007. Wizara na Taasisi zote za Serikali zinao wajibu wa kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, utawala, ulinzi na usalama. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hali ya mipaka ya nchi yetu iliendelea kuwa ya amani na utulivu, hivyo kuwapa wananchi uhuru wa kuchangia katika ujenzi wa Taifa na shughuli za maendeleo. Majeshi yetu katika kipindi hicho yalijijengea utayari na utimamu ili kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwepo kwa usalama wa nchi, watu na mali zao. Jeshi la Ulinzi kwa kushirikiana na wananchi na vyombo vingine vya dola liliendelea kudhibiti vitendo vya uhalifu katika mipaka ya nchi yetu. Aidha, Jeshi la Polisi limefanya kati kubwa ya kudhibiti uhalifu ndani ya nchi. Takwimu za makosa ya jinai zinaonyesha kupungua kwa makosa hayo kutoka 51,420 mwaka 2005 hadi 50,816 mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha nchini, Serikali imepitia taratibu na kanuni za umiliki wa silaha ndogo. Zoezi la uhakiki wa silaha lilifanyika ili kudhibiti matumizi haramu. Jumla ya silaha 50,383 zilihakikiwa upya na 567 ziligundulika kumilikiwa kinyume cha sheria. Vile vile, jumla ya silaha za aina mbalimbali 2,787 na risasi 1,255 zilisalimishwa au kukamatwa katika Mikoa ya Kigoma na Kagera na zote ziliteketezwa. Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kusalimisha silaha ikiwa ni pamoja na kuwafichua watu wanaomiliki silaha kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kurejesha wakimbizi makwao. Katika kipindi cha Julai, 2006 mpaka Mei, 2007, wakimbizi waliokuwepo kwenye makambi walikuwa 484,357 ikilinganishwa na wakimbizi 526,779 walikuwepo katika kipindi kama hicho Julai, 2005 mpaka Machi 2006. Katika mwaka 2006/2007 kambi nne za wakimbizi zilifungwa na wakimbizi 54,920 walirejeshwa makwao. Hii inatokana na kuimarika kwa hali ya amani na usalama katika nchi za Burundi na Jumhuri ya Kidemokrasi ya watu wa Kongo. Kupungua kwa wakimbizi katika maeneo ya Magharibi ya nchi yetu, kutawawezesha viongozi, watendaji wa Serikali na wananchi kutumia muda wao mwingi pamoja na rasilimali katika harakati za maendeleo ya maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Mahakama. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Serikali imewezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki na utawala wa sheria. Kazi zilizofanyika ni pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Kuboresha Sekta ya Sheria ili kutoa huduma bora kwa jamii. Vile vile, imewezesha kuanzisha mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi wa kesi za jinai na uendeshaji mashitaka. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali itaiwezesha Mahakama kutekeleza programu ya kuboresha sekta ya sheria, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kuendesha kesi ili kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya Rushwa, ili kuongeza kasi na umakini katika vita dhidi ya rushwa, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika Mkutano wake wa Saba. Sheria hii mpya imeondoa upungufu uliokuwepo kwenye sheria ya awali. Mpango wa Utekelezaji wa Taifa wa Kupambana na Rushwa awamu ya pili (2007–2012) ulikamilishwa na kuzinduliwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein tarehe 10 Desemba, 2006.

Aidha, Serikali imejenga mazingira mazuri kwa kuimarisha Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKURU) kwa kuwaongezea wataalamu na kuwapatia vitendea kazi. Katika mwaka 2007/2008, Serikali itatoa mafunzo kwa watumishi wa umma na wananchi ili kuielewa sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na kurahisisha utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tawala za Mikoa, Kamati za Ushauri za Wilaya. Kamati za ushauri za Mikoa ni vyombo muhimu katika harakati za maendeleo ya Mikoa. Baada ya uzoefu tuliopata tangu Kamati hizo zianzishwe, Serikali ilikubaliana na ushauri wa wadau mbalimbali wa kuanzisha Kamati hizi vile vile katika ngazi za Wilaya. Sheria za Serikali za Mitaa na Sheria ya Tawala za Mikoa zilifanyiwa marekebisho mwezi Februari, 2007 ili kuwezesha Kamati hizo kuanzishwa. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Kamati hizo ni kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutathmini na kupanga mikakati ya kuratibu shughuli za maendeleo katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu meneo mapya ya utawala. Nchi yetu imegawanywa katika maeneo mbalimbali ya utawala. Lengo la kugawa maeneo hayo ni kuongeza huduma karibu na wananchi na kuwawezesha kupata fursa ya kutumia rasilimali walizonazo katika kujiletea maendeleo. Hata hivyo, ni vyema kutambua kuwa kuanzisha maeneo mapya ya utawala ni suala lenye gharama kubwa, hivyo, utekelezaji wake unategemea uwezo wa Serikali katika kuhudumia maeneo hayo. Serikali imepokea maombi ya kuanzishwa kwa mitaa na vijiji vipya kutoka Halmashauri mbalimbali. Tayari Serikali imesajili vijiji 48 na hivyo kuwa na jumla ya vijiji 10,392 na mitaa 1,755 nchini. Serikali vile vile, inakusudia kuanzisha Halmashauri mpya 11 nchini. Halmashauri hizo ni Halmashauri za Wilaya za Arusha, Meru, Bahi, Chamwino, Rorya, Chato, Longido, Mkinga, Nanyumbu, Siha na Misenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo kuhusu utaratibu wa kuanzisha Halmashauri hizo kutoka katika Halmashauri zilizogawanywa yametumwa kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zinazohusika. Katika mwaka wa 2006/2007, Serikali ilianza mchakato wa kuanzisha Wilaya mpya ya Rorya. Mchakato huu utakamilishwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo ya Halmashauri mpya zilizoanzishwa. Serikali itaendelea kushirikiana na Halmashauri hizo kujenga majengo ya ofisi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupeleka madaraka kwa wananchi. Kama Bunge lako Tukufu lilivyoelezwa na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha,

Serikali itaendelea kutekeleza sera yake ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi. Serikali imeanza kuchambua kazi na majukumu ambayo yamekuwa yakitekelezwa Wilayani lakini rasilimali fedha na rasilimali watu zikiendelea kubaki makao makuu ya Wizara. Utaratibu huu unadhoofisha uwajibikaji na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa miradi ya wananchi. Aidha, bila kuwashirikisha wananchi na vyombo vyao vya uwakilishi, ubora wa huduma zitolewazo huathirika. zoezi la kuchambua na kutathmini ni kwa kiasi gani Wizara zinazingatia upelekaji wa madaraka kwa wananchi limekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imebainisha miradi na majukumu yatakayohamishiwa kwenye Mikoa na Halmashauri kutoka Wizara tano zifuatazo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kwa upande mwingine, tathmini ilibaini kuwa katika Wizara ya Miundombinu, shughuli za kiutekelezaji zimehamishiwa kwenye Wakala za Serikali zilizoanzishwa chini ya Wizara hiyo. Kwa hiyo, jukumu lililopo hivi sasa ni kuzitathmini wakala hizo kwa nia ya kubainisha miradi na shughuli zinazostahili kuhamishiwa kwenye Mikoa na Halmashauri ili zipate kutekelezwa kwa ufanisi zaidi na hivyo kuinua kiwango cha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itazipeleka moja kwa moja kwenye Halmashauri shilingi bilioni 216.2 ambazo awali zilikuwa zinapitia Wizarani. Wizara nyingine nne zilizopo katika awamu ya kwanza nazo zina wajibu wa kutekeleza sera hii kwa kupeleka fedha na rasilimali watu kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kugatua madaraka, majukumu na rasilimali zinazohusika, kazi kubwa ya Serikali Kuu itakuwa ni kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji huko Mikoani na kwenye Halmashauri ili kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika kutokana na zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuzitathmini Wizara zilizosalia kuhusu uzingatiaji wa dhana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi katika mipango, mikakati na Bajeti zao litaendelezwa na limepangwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwezi Desemba, 2007. Wizara hizo zina wajibu wa kutoa ushirikiano unaohitajika katika kutekeleza na kufanikisha zoezi hili. Maandalizi yanayohitaji kufanyika ni pamoja na kufanya mapitio ya sera na sheria zinazosimamiwa na Wizara hizo na kuhakikisha kuwa zinaendana na upelekaji wa madaraka kwa wananchi. Nia ni kuiwezesha Serikali kuandaa Mpango na Bajeti yake ya mwaka 2008/2009 ambayo itazingatia sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa utendaji kati ya Halmashauri na Serikali Kuu. Halmashauri zote nchini ziliingia Mkataba wa Utendaji katika matumizi ya rasilimali fedha na Serikali Kuu mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya mwaka 2006/2007 kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu. Matokeo ya uamuzi huo yamesaidia kuboresha udhibiti

na usimamizi wa rasilimali na hivyo kuwezesha rasilimali hizo kutumika kama ilivyopangwa. Utaratibu huu utaendelea kutumika katika mwaka ujao wa fedha na tathmini halisi ya matokeo ya mikataba hiyo itafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa. Hadi mwezi Machi 2007, miradi 2,016 ilitekelezwa chini ya Mfumo wa Kuzipatia Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo *(LGCDG)* na Ruzuku ya Kujijengea Uwezo *(LGCBG).* Miradi hii ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 47.2 na sekta zilizohusika ni barabara, afya, elimu, maji, kilimo na utawala. Serikali ilichukua hatua za kuajiri wataalamu na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri, Waheshimiwa Madiwani na kutoa vitendea kazi. Hatua hizi zimewezesha ongezeko la kuridhisha kwa Halmashauri kufaulu vigezo vya kupatiwa ruzuku ya maendeleo kutoka Halmashauri 84 mwaka 2006/2007 hadi Halmashauri 109 kwa mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Halmashauri zote 121 nchini zitapatiwa fedha za ruzuku ya kujijengea uwezo baada ya kufuzu vigezo muhimu chini ya mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya watendaji na posho za Madiwani. Serikali imekuwa ikitenga fedha za kuwalipa mishahara maafisa watendaji wa vijiji na mitaa. Hadi mwezi Desemba 2006, Maafisa Watendaji wa vijiji 9,716 kati ya Watendaji 10,392 ambao wanapaswa kuwepo kulingana na idadi ya vijiji walilipwa na Watendaji wa Mitaa 1,512 kati ya watendaji 1,755 nao walilipwa. Aidha, wale ambao bado hawajalipwa taratibu za ajira zao zinakamilishwa. Wakurugenzi wa Halmashauri wanaowajibu wa kukamilisha zoezi la ajira za maafisa hawa. Vile vile, kutokana na majukumu mengi waliyonayo Waheshimiwa Madiwani, Serikali imekubali kuongeza posho zao kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 60,000 kwa mwezi kulingana na uwezo wa Halmashauri. Kazi ya kutathmini Halmashauri zisizo na uwezo inaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Malipo ya Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Namba 9 ya mwaka 2006 ya kuubadilisha Mfuko wa Akiba wa Watumishi wa Serikali za Mitaa kuwa wa pensheni. Lengo lilikuwa ni kuwawezesha wafanyakazi wanachama wa mfuko kuwa na sifa ya kulipwa mafao ya pensheni kwa kuzingatia muda wao wa ajira.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba utekelezaji wa sheria hiyo umeanza na wanachama wanaendelea kulipwa Mafao ya Pensheni. Aidha, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 10 katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 kati ya ruzuku ya shilingi bilioni 107.3 zinazohitajika ili kuuwezesha Mfuko kumudu mabadiliko hayo. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kukamilisha kiasi kilichokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2006/2007, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeendelea kutekeleza majukumu yake ambapo hadi tarehe 15 Aprili, 2007, mikopo ya jumla ya shilingi milioni 440 imetolewa na kufanya mikopo yote iliyotolewa kufikia jumla ya shilingi bilioni 2.5. Aidha, jumla

ya shilingi milioni 284.2 zimechangwa na Halmashauri na kufanya michango yote kufikia jumla ya shilingi bilioni 2.0 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 5.5.

Kwa upande wa mikopo iliyotolewa, jumla ya Halmashauri 43 zimepata mikopo kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya kilimo, ununuzi wa vyombo vya usafiri na ujenzi wa vituo vya mabasi, masoko na kituo cha mikutano. Katika mwaka 2007/2008, Serikali itaendelea kurekebisha muundo wa bodi kwa lengo la kuongeza ufanisi ili Halmashauri nyingi zaidi ziweze kunufaika. Chombo hiki ni muhimu kwa Halmashauri . Ili kiweze kuongeza kiwango cha mikopo, Halmashauri nazo hazina budi kuchangia kikamilifu ili kutunisha fedha za Bodi hiyo. Pamoja na kuchangia, Halmashauri zinao wajibu vilevile wa kurejesha mikopo kwa mujibu wa makubaliano ili kuipa Bodi uwezo wa kuendelea kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, katika mwaka 2006/2007, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kimeendesha mafunzo ya Maafisa Watendaji wa Vijiji 240 na wa Mitaa 102, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa 2,663, Maofisa Watendaji wa Kata 300 na Madiwani wapya 87 kutoka katika Mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida. Kazi nyingine ni pamoja na kuandaa mitaala ya programu nne za Astashahada na Stashahada za Utawala, Uhasibu na Fedha katika Serikali za Mitaa na kuiwasilisha kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kwa ajili ya usajili. Programu hizo zitaanza mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Kwa kutambua umuhimu wa chuo hiki katika kujenga uwezo wa rasilimali watu katika Halmashauri nchini, Mpango Mkakati wa miaka mitano 2007 – 2012 umeandaliwa. Utekelezaji wa mpango huo utaanza mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Elimu Kibaha katika mwaka 2006/2007, Shirika la Elimu Kibaha limewezesha taasisi zilizo chini yake kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Taasisi hizo zilitoa huduma zifuatazo:-

Kwanza mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi ikiwa ni pamoja na ufugaji bora wa kuku na ng'ombe, kutoa mafunzo kwa maafisa tabibu 120, kuhudumia wagonjwa 560,000, kutoa elimu kwa akinamama 210 kuhusu lishe bora, elimu na malezi bora; mafunzo kwa wanafunzi 960 wa shule ya msingi na 1,196 wa shule za sekondari. Vile vile, Shirika lilitoa huduma ya maktaba kwa wadau 2,116. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Shirika litatekeleza Mpango Mkakati wake ikiwa ni pamoja na upanuzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana na Hospitali Maalumu ya Tumbi kwa kujenga wodi mpya yenye vitanda 50. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya maji na barabara utafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpigachapa Mkuu wa Serikali, Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali inao umuhimu mkubwa katika kuchapa nyaraka za Serikali kwa kuwa sehemu kubwa ya kazi za Serikali hutumia nyaraka. Kuwepo kwa idara hii kunaiwezesha Serikali kudhibiti uchapaji wa nyaraka zake. Ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika idara hii, Serikali katika mwaka 2007/2008, imetenga fedha kwa ajili ya kuwezesha

ununuzi wa baadhi ya mitambo. Wizara, Idara, Wakala, Mikoa na Halmashauri zote zinao wajibu wa kuzingatia taratibu za uchapishaji wa nyaraka za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, moja ya kazi kubwa ambayo Mamlaka imekamilisha ni upimaji ardhi wa hekta 4,608 zilizotengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Chuo Kikuu kipya cha Serikali cha Dodoma. Aidha, Mamlaka imekamilisha uthamini wa mali za wananchi waliokuwa katika eneo hilo ili kuwezesha utwaaji ardhi. Katika mwaka 2007/2008, Mamlaka itapiga picha za anga na kutayarisha ramani za msingi kwa ajili ya kurahisisha ujenzi wa miundombinu na uendelezaji wa Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya mazingira, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua zilizokuwa zinaendelea kuchukuliwa kuhusu hatua zilizokuwa zinaendelea kuchukuliwa na Serikali za kudhibiti uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji. Hatua hizo zimeleta mafaniko hasa katika utunzaji wa vyanzo vya maji katika maeneo mengi nchini. Miongoni mwa matokeo ya hatua hii ni kuongezeka kwa uoto wa asili katika Bonde la Ihefu, kuongezeka maji katika Mto Ruaha na kujaa kwa Bwawa la kuzalisha umeme la Mtera. Vile vile utoaji wa elimu ya mazingira kwa wananchi umeimarishwa. Serikali pia iliendelea kuratibu na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za Kikanda na za Kimataifa zinazohusu hifadhi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya kuahirisha Mkutano wa Saba wa Bunge tarehe 20 Aprili 2007, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeunda Tume ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa zoezi zima la kuwahamisha wafugaji wa mifugo yao kutoka ndani ya Bonde la Usangu hususan eneo la Ihefu. Napenda kuliarifu Bunge hili kuwa Tume iliyoteuliwa imekamilisha kazi yake na imewasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Rais. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati wajumbe wote wa Tume hiyo. Kwa kufanya kazi yao kwa umakini na uharaka unaolingana na uzito wa jukumu walilokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuboresha mazingira ya miji yetu. Hii ni kwa kutambua kuwa miji ndiyo kioo na sura ya nchi. Vile vile, afya za wananchi zinategemea usafi wa mazingira. Matokeo dhahiri yameanza kuonekana kwa kiasi kikubwa katika upandaji miti, usafi wa miji na uzoaji taka. Kutokana na kufanikiwa kwa zoezi hilo, Serikali imetoa waraka Na. 1 wa mwaka 2007 kuhusu uboreshaji wa mazingira na huduma katika miji yote nchini. Nawapongeza viongozi wa Mikoa na Halmashauri zote nchini waliotekeleza vizuri maelekezo ya waraka huo. Mfano mzuri ni Jiji la Dar es Salaam. Natoa wito kwa asasi zisizo za Kiserikali, sekta binafsi na wadau mbalimbali kuendelea kushirikiana na Serikali na Halmashauri za Miji kuboresha mazingira ya miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utamaduni na michezo, mamlaka mbalimbali za Serikali zimechukua hatua za kutoa fursa kwa mwananchi mmoja mmoja au makundi ya jamii kuendeleza utamaduni wa Mtanzania. Moja ya eneo muhimu na ambalo ni kielelezo cha Mtanzania ni lugha ya Kiswahili. Serikali imeanza kuchukua hatua zitakazowezesha

ongezeko la matumizi ya Kiswahili nchi za nje. Itifaki ya kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ilisainiwa rasmi mwezi Aprili, 2007. *(Makofi)*

Aidha, lugha ya Kiswahili inatambuliwa na Umoja wa Nchi za Afrika kama lugha rasmi. Nitumie nafasi hii kuwapongeza baadhi ya viongozi ambalo wamekuwa wakitumia lugha ya Kiswahili katika Mikutano ya Umoja huu. Viongozi hao ni pamoja na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Joachim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji na Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, Spika wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Katika mwaka 2007/2008, Serikali itaandaa mikutano miwili ya Kimataifa kuhusu lugha ya Kiswahili. Mkutano wa kwanza utazihusu nchi za Maziwa Makuu na wa pili utazikutanisha redio zinazotangaza Kiswahili duniani. Ni Matarajio yangu kwamba Watanzania wote wataziunga mkono jitihada hizi zinazofanywa na Serikali katika kukuza lugha ya Kiswahili. Aidha, natoa wito hususan kwa vijana wetu wajitokeze kusomea lugha ya Kiswahili ili waweze kunufaika na fursa zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali imeendelea kuboresha michezo kwa kuchukua hatua mbalimbali. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuajiri walimu wa michezo wa mpira wa miguu wenye sifa za Kimataifa ili timu zetu za michezo ziweze kufikia viwango vya Kimataifa. Aidha, Serikali imechukua hatua za kufufua michezo katika shule na vyuo kwa ajili ya kuibua vipaji kutoka ngazi za chini. Mawaziri husika watatoa maelezo ya kina kuhusu hatua hizo. Napenda kuipongeza timu ya Taifa kwa hatua nzuri iliyofikia katika mashindano ya kutafuta timu zitakazoshiriki fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2008 nchini Ghana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu wa maafa, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, nchi yetu ilikumbwa na matukio ya maafa mbalimbali. Mvua zilizonyesha mwishoni mwa mwaka 2006 na mwanzoni mwa mwaka huu wa 2007 zilisababisha mafuriko katika Mikoa ya Mtwara, Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Singida, Iringa na Manyara. Mafuriko hayo yalisababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu, mazao, pamoja na makazi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa tani 135 za mahindi na shilingi milioni 253.3 kuwasaidia walioathirika na mafuriko hayo pamoja na maafa mengine. Nchi yetu imejifunza mengi kutokana na maafa yaliyotokea. Ni kweli kwamba hatuwezi kuzuia maafa yote lakini tunaweza kupunguza madhara yake endapo tutajiandaa kabla hayajatokea. Changamoto iliyo mbele yetu ni kwa wananchi wote kuchukua hatua za kuzuia pale ambapo tunaweza kufanya hivyo na kuchukua tahadhari kwani itasaidia kupunguza madhara ya maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kukabiliana na maafa linahusu wadau wengi. Aidha, kazi hiyo huweza kushirikisha nchi zaidi ya moja. Kwa kutambua hilo, Serikali imewezesha Majeshi ya Anga ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) kwa kushirikiana na wadau wa maafa nchini kuandaa na kufanya zoezi la vitendo la uokoaji lililojulikana kama *Exercise Blue Ruvuma*.

Aidha, Majeshi ya nchi za Afrika Mashariki yaliwezeshwa kushiriki katika zoezi la kukabiliana na maafa ya mafuriko na maporomoko ya udongo lililojulikana kama *Exercise Hot Spring* nchini Uganda mwezi Septemba 2006. Lengo la mazoezi yote hayo ni kukuza ushirikiano baina ya majeshi na wadau wa masuala ya maafa wa nchi hizo na kuimarisha mbinu za kukabili maafa ili kurahisisha mwitikio wa haraka wakati wa maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango mahususi wa Kimataifa wa *Hyogo Declaration and Framework for Action* wa miaka kumi (2005 hadi 2015) wenye mtazamo wa kupunguza visababishi vya maafa na kufanya ulimwengu kuwa mahali salama pa kuishi. Mpango huu unavipaumbele vikuu vifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha suala la kupunguza athari za maafa linapewa kipaumbele katika ngazi ya Kitaifa na ya jamii, pamoja na kuwa na muundo wa kutekeleza;

(b) Kuainisha, kutathimini na kufuatilia hali inayoweza kusababisha maafa na kuboresha uwezo wa kutoa tahadhari kabla maafa hayajatokea;

(c) Kutumia elimu na ubunifu, kuijengea jamii utamaduni wa kujikinga na maafa katika ngazi zot; na

(d) Kuimarisha mbinu za utayari ili kuwa na uwezo wa kukabili maafa katika ngazi zote.

Moja ya nguzo ya kuwezesha utekelezaji wa mpango huu ni elimu. Kundi muhimu katika jamii ambalo linaweza kusaidia sana katika jamii ambalo linaweza kusaidia sana katika matukio ya maafa ni waandishi wa habari. Ili kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya maafa Serikali kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Umoja wa Kitaifa inayohushughulikia upunguzaji maafa iliandaa warsha shirikishi kwa waandishi wa habari nchini. Mafunzo hayo yamewaongezea uelewa wa masuala ya maafa na kuwapa ujuzi wa kuandika habari za namna ya kuzuia au kupunguza maafa kabla hayajatokea. Mafunzo kama hayo huwajengea uwezo waandishi wa habari kuandika habari zenye mwelekeo wa kupunguza maafa kupitia fani yao, kujenga ushirikiano na wadau wa shughuli za maafa, kubadilishana taarifa na kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa habari sahihi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza waandishi wa habari kwa hatua hii, ni matarajio ya Serikali kwamba watatumia chombo walichokianzisha cha *Tanzania Media Disaster Risk Reduction Forum* kuwafikishia wananchi taarifa sahihi kwa wakati na hivyo kupunguza matukio na madhara ya maafa hapa nchini. *(Makofi)*

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali itaimarisha uwezo wake wa kuitikia maafa kwa ufanisi na kufanya tathimini ya kina ya hali ya maafa katika Mikoa yote. Aidha, itatoa mafunzo kwa Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya. Vile vile, itaendelea kutoa elimu ya maafa kwa umma kupitia vyombo vya habari na kushiriki vikao vya Kikanda na Kimataifa vinavyohusu masuala ya maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu magonjwa ya kuambukiza ya mifugo. Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulijitokeza nchini mwezi Februari, 2007 katika Wilaya za Ngorongoro na Monduli Mkoani Arusha, ugonjwa huu ulisambaa katika Mikoa tisa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa na Mbeya. Hadi tarehe 16 Juni, 2007, ugonjwa huo ulikuwa umesababisha vifo vya watu 139 na takribani mifugo 50,000. Katika kukabiliana na ugonjwa huu, Serikali ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 4.8 na Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa *(UNDP)* limetoa msaada wa Dola za Kimarekani milioni 1.36 kwa ajili ya chanjo na vifaa. Fedha hizo zimetumika kununulia dozi milioni mbili kati ya hizo, dozi milioni 1.62 zimesambazwa katika Wilaya 33 pamoja na mashamba ya mifugo ya Serikali na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Jumla ya mifugo 561,654 imechanjwa na zoezi hili linaendelea. Katika mwaka 2007/2008 Serikali itaendelea kutoa chanjo na elimu ili kutokomeza ugonjwa huu. Mamlaka zinazohusika zinao wajibu wa kusimamia kikamilifu utoaji wa chanjo na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa UKIMWI. Katika mwaka 2006/2007, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* imeendelea kuziwezesha sekta mbalimbali kukabiliana na janga la UKIMWI kama sehemu ya shughuli za kila siku. Miongozo imetolewa na Bajeti ya shughuli za UKIMWI imetengwa kwa Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, ushirikiano wa karibu na sekta binafsi umehimizwa. Kamati shirikishi za kudhibiti UKIMWI kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuboresha udhibiti wa UKIMWI kwenye ngazi ya jamii. Halmashauri za Wilaya 22 zimeongezewa uwezo wa kuendesha shughuli za UKIMWI kwa kupelekewa wafanyakazi wa kujitolea. Mamlaka za Serikali za Mitaa 122 zimepatiwa shilingi bilioni 1.85 kwa ajili ya kupambana na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imepanga kutoa misaada ya kiufundi kwenye Wizara na taasisi za Serikali na binafsi, Mikoa na Halmashauri za Wilaya na miji na asasi za jamii kwenye maeneo yenye athari kubwa ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Aidha, imepanga kuimarisha udhibiti wa UKIMWI kwa kutilia mkazo kuzuia maambukizo mapya hasa miongoni mwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hiyo, Tume itafanya utafiti kuhusu hali ya UKIMWI katika ngazi ya kaya na itahusisha maeneo ya mijini na vijijini. Utafiti huu unakusudia kukidhi malengo yafuatayo:-

(a) Kukusanya taarifa juu ya mwenendo, tabia na ufahamu juu ya UKIMWI, Virusi vya UKIMWI na Malaria;

(b) Kupima kiwango cha maambukizo ya UKIMWI na Malaria;

(c) Kukusanya taarifa mbalimbali zinazowahusu wagonjwa wa muda mrefu, watoto yatima na walio katika mazingira magumu; na

(d) Kukusanya taarifa juu ya huduma za afya na kiwango cha msaada kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huu ni muhimu sana katika kuangalia mwenendo wa hali ya maambukizi tangu kipindi cha utafiti uliopita wa mwaka 2003/2004 hadi sasa. Taarifa hizi zitasaidia Taifa na wadau wengine katika kufuatilia na kutathmini sera, mipango na mikakati iliyopo kwa sasa ili tuweze kuweka mipango ya kupambana na janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa kupima ni hatua muhimu katika kudhibiti maambukizi mapya ya UKIMWI, Mheshimiwa Rais ametangaza rasmi siku ya tarehe 14 Julai 2007 kuwa siku ya Kitaifa ya Kupima Virusi vya UKIMWI. Lengo la siku hii ni kuihamasisha jamii itambue umuhimu wa kila mmoja kufahamu hali ya afya yake ili kuweza kuchukua maamuzi sahihi dhidi ya UKIMWI. *(Makofi)*

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi wote kuwa Serikali imejiandaa ipasavyo kufanikisha zoezi hili. Nawahimiza viongozi wote wakiwemo viongozi wa dini zote kuwahamasisha wananchi kushiriki katika zoezi hili. Hii itasaidia kujua ukubwa wa tatizo na hivyo kuwa na mipango thabiti ya huduma za kinga.

Aidha, zoezi hili litaongeza utambuzi na tiba kwa wale wanaostahili tiba na kwa kiasi kikubwa utapunguza unyanyapaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu wa udhibiti wa dawa za kulevya. Nchi yetu bado inakabiliwa na tatizo la dawa za kulevya ambalo linaongezeka na kuathiri maisha na maendeleo ya jamii yetu hasa vijana. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali katika mwaka 2006/2007 imetekeleza mikakati mbalimbali ifuatayo:-

(a) Kuendesha operesheni maalumu ya kukabiliana na wafanyabiashara haramu wa dawa za kulevya iliyowezesha watuhumiwa 121 kuhojiwa na 86 kati yao kuwekwa chini ya uangalizi wa Mahakama. Aidha, kilo 225,229 za bangi ziliteketezwa na mashamba yenye ekari 1,070 ya bangi yaliteketezwa kati ya Oktoba, 2006 na Mei, 2007;

(b) Kutekeleza mradi wa ujenzi wa kituo maalumu kwa ajili ya matibabu ya waathirika wa dawa za kulevya mjini Dodoma;

(c) Kuelimisha umma juu ya athari za dawa za kulevya kwa njia ya *television,* redio, magazeti pamoja na kufanya maonyesho kwenye matukio ya Kitaifa;

(d) Kushirikiana na kuzisaidia asasi zisizo za Kiserikali na makundi mengine kwa lengo la kuelimisha umma na kupiga vita dawa za kulevya; na

(e) Kuendelea kuijengea Tume uwezo wa vitendea kazi ili kuiongezea ufanisi katika kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali itaongeza kasi ya kudhibiti biashara pamoja na matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuendelea na operesheni ya kukabiliana na wafanyabiashara wa dawa za kulevya pamoja na kutokomeza kilimo cha bangi nchi nzima;

(b) Kuendelea na kampeni za kuelimisha umma juu ya athari za dawa za kulevya na kudhibiti maambukizi ya UKIMWI;

(c) Kukamilisha Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya; na

(d) Kuandaa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ili kuimarisha udhibiti pamoja na kuipa uwezo zaidi Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano wa Kimataifa, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu tarehe 18 Juni, 2007, nchi za Burundi na Rwanda zilijiunga rasmi na Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki. Jumuiya hii sasa inakuwa na jumla ya nchi tano wanachama. Ni dhahiri kuwa uanachama wa nchi hizi utapanua wigo wa biashara kwa kuwapatia wafanyabiashara wa Kitanzania punguzo la ushuru wa forodha kwa nchi hizo kwa asilimia 80. Napenda kuchukua nafasi hii kuwahamasisha wananchi wachukue hatua za kunufaika na fursa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi kwa kushiriki kwenye mikutano mbalimbali kama vile Umoja wa Mataifa, *Leon Sullivan Summit VII;* Ushirikiano kati ya China na Afrika *(Sino-Africa Forum);* Mikutano ya Kimataifa kuhusu Uchumi Duniani *(World Economic Forum);* majadiliano na Shirika la Biashara la Kimataifa *(WTO)* na Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Aidha, Balozi zetu katika nchi mbalimbali duniani zimeendelea kutekeleza Diplomasia ya Kiuchumi kwa kutangaza bidhaa na vivutio mbalimbali vya Tanzania kwa kushiriki katika Maonyesho ya Bidhaa ya Kimataifa kama yale ya Marekani, Uingereza na China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali itaongeza juhudi katika Diplomasia ya Kiuchumi kwa kuwatumia Watanzania waishio nje ya nchi kuitangaza Tanzania na kuwavutia wawekezaji nchini. Katika harakati za kuitangaza nchi yetu, Serikali ilikubali Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nane wa *Sullivan* utakaofanyika tarehe 2 – 6 Juni, 2008. Maudhui ya Mkutano huo ni Utalii na Maendeleo ya Miundombinu. Tunatarajia wajumbe wapatao 3,000, Wakuu wa Nchi 30 na watu mashuhuri 40 kutoka nje ya nchi watashiriki katika mkutano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugeni huu ni fursa ya kipekee ya kuanzisha mahusiano ya kibiashara na kutangaza maeneo ya uwekezaji na vivutio vya utalii vilivyoko nchini.

Napenda kuchukua nafasi hii kuzihamasisha sekta zote na hasa sekta binafsi nchini kujitayarisha vema ili kunufaika na mkutano huo. Aidha, natoa wito kwa Watanzania waishio nje ya nchi kutumia uzalendo wao kuitangaza Tanzania kwa nguvu zao zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto, hii ni Bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Nne. Tumebakiwa na Bajeti nyingine tatu tu kufikia mwaka 2010 ambapo tutajipima ni wapi tumefikia katika utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea. Vile vile, imebaki takribani miaka saba kufikia malengo ya milenia na miaka 18 kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Miaka hii si mingi hata kidogo na muda unakwenda kasi kweli kweli. Hivyo, tuna changamoto kubwa ya kukuza uchumi wetu kwa kasi kubwa zaidi. Kwa mujibu wa wataalamu, ili kuondoa umaskini kwa haraka zaidi, kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kinatakiwa kisipungue asilimia 7 hadi 10 kwa mwaka, kwa zaidi ya miaka mitano mfululizo. Ukweli huu unatukumbusha falsafa ya hayati Mwalimu Julius Nyerere inayosema, nanukuu: “Lazima tukimbie wakati wenzetu wanatembea.”

Mheshimiwa Spika, kimsingi, kasi ya sasa ya ukuaji wa uchumi haiwezi kutuondoa kwenye umaskini na kwa hili hatuna mjadala wala hiari, lazima tuongeze kasi ya uzalishaji ili kukuza Pato la Taifa. Kila mwananchi mahali alipo anatakiwa kudhamiria na kuamua kuukataa umaskini kwa nguvu zake zote na kutafuta maendeleo kwa kila fursa inayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ambayo yatawezesha uchumi kukua kwa kasi kubwa zaidi. Mwaka huu tunatarajia Pato la Taifa likue kwa asilimia 7.3. Lengo hili tunaweza kulifikia, na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/2008 imezingatia kikamilifu azma hiyo.

Hata hivyo, kila mmoja wetu ni lazima atimize wajibu wake, kwa nafasi yake. Tufanye kazi kwa bidii na maarifa zaidi na zaidi ya hayo, viongozi tuhakikishe kuwa kila mwananchi aliye na uwezo wa kufanya kazi halali, anafanya hivyo kwa bidii. Tukumbuke kuwa hata Vitabu Vitakatifu vinatuambia kuwa: “Asiyefanya kazi na asile.” Kwa kweli tunahitaji kuwa wabunifu zaidi ili tusibaki kutamani tu maendeleo ya wengine, bali kila mwananchi ajitume kutafuta maendeleo pale alipo. Nasema inawezekana! Tukiamua kwa dhati tutaweza kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi kwa zaidi ya asilimia 10 yaliyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine kubwa iliyopo mbele yetu na ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesisitiza ni nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Serikali inakusanya fedha kwa njia ya kodi na misaada mbalimbali. Fedha zote ni mali ya wananchi wa Tanzania na lazima zitumike kwa kuzingatia kanuni na taratibu za fedha. Serikali inawajibika kwa wananchi ambao ni walipakodi na wafadhili wanaotupatia misaada kuhakikisha kuwa fedha zao zinatumika kwa maendeleo ya nchi na hazifujwi. *(Makofi)*

Mikoa na Halmashauri zinatakiwa kukamilisha taratibu za kuunda Kamati za Ukaguzi kama ilivyo kwa Wizara. Aidha, ninapenda kutoa wito kwamba katika mwaka

wa fedha ujao kila Afisa Masuuli ahakikishe kuwa anafuata miongozo bora ya uhasibu na utunzaji wa fedha. Vile vile, awasiliane na wakaguzi kutatua matatizo na siyo kutafuta sababu za kushindwa kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto ya kutatua kero za wananchi. Changamoto hii inahitaji kila mtumishi wa umma kuwajibika ipasavyo katika majukumu aliyopewa. Utatuzi wa kero hizo hauna budi kufanywa kwa wakati. Katika hali ya kawaida, sitarajii mwananchi yeyote kwa mfano, mwenye tatizo la mpaka wa shamba lake katika kijiji cha Kasharu katika Mkoa wa Kagera, aje Dar es Salaam kutatuliwa matatizo yake na kumwacha Mkurugenzi wa Halmashauri husika, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine katika ngazi mbalimbali. Akifanya hivyo, maana yake ni kwamba alikotoka uongozi hauwajibiki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kero nyingi za wananchi zinaweza kushughulikiwa katika ngazi nilizozitaja endapo kila ngazi ya utawala na utendaji itatimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini karibu asilimia 95 ya kero za wananchi ambazo zinafika kwenye ofisi za viongozi wa Kitaifa zinaweza kushughulikiwa katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Wizara. Ni wajibu wa viongozi katika ngazi zote kuweka utaratibu wa kushughulikia kero hizo katika maeneo yao. Ningependa tuzingatie methali moja ya Waingereza isemayo;*"if you want a brighter view of life, help someone else find the solution of his/her problem." (Makofi)*

Kwa tafsiri ya Kiswahili isiyo rasmi ya maelezo haya ni kwamba, kama unataka kuwa na mtazamo mzuri wa maisha, msaidie mtu mwingine kupata ufumbuzi wa kero yake.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba hii, naomba kusisitiza masuala yafuatayo:-

(a) Serikali itaendelea kuelekeza nguvu zake katika sekta za elimu, miundombinu, afya, kilimo na maji.

(b) Serikali itaendelea kuweka juhudi zaidi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

(c) Ajenda ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kukuza mauzo nje na diplomasia ya uchumi vitapewa msukumo wa kipekee.

(d) Tumefanikiwa kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za Serikali katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mwaka ujao nguvu zaidi zitaongezwa katika eneo hili.

(e) Sera ya kugatua na kupeleka madaraka na rasilimali karibu na wananchi kupitia Serikali za Mitaa itapewa kipaumbele.

(f) Amani, utulivu na umoja wa nchi yetu na watu wake vitadumishwa. Vile vile, kuimarisha Muungano na kujenga mazingira mazuri ya kisiasa kwa kukuza demokrasia na kuimarisha utawala bora.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07 Serikali imeonyesha kwa vitendo uwezo wake wa kusimamia na kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Pamoja na changamoto zinazotukabili ambazo nimezielezea hivi punde pamoja na mahitaji makubwa ya rasilimali za ujenzi wa miundombinu, kupanua elimu ya sekondari, Serikali imejipanga vizuri kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao. Uwezo tunao na rasilimali tunazo. Kinachotakiwa ni kujenga mshikamano na umoja wetu wa kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, nchi yetu imepata misaada, misamaha ya madeni na mikopo kutoka kwa wahisani mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali na Watanzania wote, nazishukuru nchi wahisani na Mashirika ya Kimataifa na yale yasiyo ya Kiserikali kwa misaada na mikopo waliyotupatia. Misaada na mikopo hiyo imechangia katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo yao na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwa mara nyingine kutoa shukrani kwa wale wote ambao wamewezesha Serikali ya Awamu ya Nne kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa kwanza wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Nawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa ushauri wao ambao umewawezesha Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yao ya Kitaifa kikamilifu. Pia, ninawashukuru kwa ushirikiano walionipa. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Phillemon Luhanjo kwa kutekeleza kazi za Serikali ipasavyo. Navishukuru vyombo vyote vya dola na vyombo vya habari kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Nawashukuru Watanzania wote kwa mchango wao ambao umeiwezesha Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2007/2008 kwa muhtasari.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa muhtasari naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2007/2008, ya jumla ya shilingi 1,465,530,957,000 (trilioni moja, bilioni mia nne na sitini na tano, milioni mia tano thelathini, laki tisa hamsini na saba elfu) ya Ofisi ya Waziri Mkuu na jumla ya shilingi 42,718,423,000 (bilioni arobaini na mbili, milioni mia saba kumi na nane, laki nne na ishirini na tatu elfu) kwa ajili ya Mfuko wa Bunge, ikiwa ni

mishahara, matumizi mengine na fedha za maendeleo za ndani na nje kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii nimeambatisha majedwali mbalimbali ambayo yanafafanua kwa kina zaidi Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa kunisikiliza, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana na hongera sana kwa kuweza kuwasilisha mambo mengi katika muda ambao unatosheleza, si mrefu wala si mfupi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ninapenda kufanya mambo mawili, kwanza, nimearifiwa kwamba Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wamekuja na wake ama waume, kutegemea jinsia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba wasimame pale walipo, wake na waume wa Wakuu wa Mikoa. Ahsanteni sana, karibuni sana na poleni sana kuwa ni wenza wa Wakuu wa Mikoa. Najua ni kazi ngumu kidogo kwa sababu Wakuu wa Mikoa huwa ni siku chache sana wanakaa nyumbani. Poleni sana kwa mazingira hayo! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, walioomba kuchangaia ni 85. Kwa hiyo, nimefunga orodha. Kwa uzoefu wetu, wameongezeka 93, hata sidhani kama tutafikia huko. Kwa hiyo, hakuna haja tena ya kuendelea kuleta majina kwa sababu itakuwa ni zoezi ambalo halina tija yoyote. Kwa hiyo, nimefunga orodha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hivi nimeombwa niwe mgeni rasmi kwenye maonyesho ya Asasi zisizo za Kiserikali, wapo pale katika eneo la Uwanja wa Tafrija wa Bunge. Baadae tukishatoka saa 7.00 itakuwa ni vizuri tukajumuika pale. Kwa hiyo, nalazimika sasa nimwite Mheshimiwa Job Ndugai, ili nikashughulikie suala hilo la Asasi zisizo za Kiserikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu

Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu la 25 Waziri Mkuu, Fungu la 27 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu la 37 Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu la 42 Ofisi ya Bunge, Fungu la 61 Tume ya Uchaguzi, Fungu la 91 Tume ya Kuratibu Dawa za Kulevya na Fungu la 92 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu la 56 Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mafungu ya 70 hadi 89 na 95 kwa ajili ya Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kujaza nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi hiyo, Marehemu Juma Jamaldin Akukweti aliyefariki dunia mwezi wa Januari, 2007.

Mheshimiwa Dr. Batilda Burian ana ujuzi, uzoefu na uwezo mkubwa na kwa kipindi kifupi tangu ateuliwe katika wadhifa huo amedhihirisha uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutuma salamu za rambirambi kwa familia zote zilizopoteza wapendwa wao kwenye ajali zilizotokea Mkoa wa Arusha, Singida na Mbeya. Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Taifa letu hupoteza maisha ya Watanzania kwa maelfu na mali zenye thamani kubwa kutokana na ajali za vyombo vya usafiri. Inabidi Serikali ichukue hatua za makusudi kubaini vyanzo vya ajali hizi na kuzidhibiti ili kuepusha hasara kubwa ya maisha na mali zinazotokana na ajali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu imegawanyika katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza ni ile inayohusu Sera, Bunge na Uratibu na ambayo inahusu Mafungu ya 25, 27, 37, 42, 61, 91 na 92 na sehemu ya pili ni ile inayohusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inayohusu Mafungu 56, 70 hadi 89 na 95. Kwa kuelewa ukubwa na majukumu yaliyopo katika Ofisi hii, Kamati yangu ilitenga jumla ya siku tatu kushughulikia Makisio yake, siku moja kwa ajili ya kupitia na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na siku mbili kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ikijumuisha mikoa 21 ya Tanzania Bara na Halmashauri za Miji na Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuiletea Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kazi ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tarehe 4 Juni, 2007, Kamati ilipokea muhtasari wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, kwa mwaka 2007/2008 uliowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kamati ilipokea pia taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2006/2007 ambapo ilielezwa jinsi fedha za Matumizi zilizotengwa katika Ofisi hiyo na

Taasisi zake zilivyotumika. Aidha, Kamati ilijulishwa juu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake na matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, ilitengewa jumla ya shilingi 76,154,733,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 40,636,793,400/= kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo. Hadi tarehe 30 Aprili, 2007, Ofisi ilikuwa imepokea na kutumia shilingi 76,192,326,217/38 za Matumizi ya Kawaida na shilingi 16,811,819,301/= za Miradi ya Maendeleo kwa fedha za ndani na za nje.

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya shilingi 3,308,992,000/= zilipunguzwa kwenye Fungu Namba 37 la Ofisi ya Waziri Mkuu na shilingi 270,000,000/= zilipunguzwa kutoka Fungu Namba 61 la Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mvua. Kiasi cha fedha zilizotolewa ni asilimia 63 ya Matumizi ya Kawaida na 42% ya Mpango wa Maendeleo ya fedha zilizoidhinishwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zake za ndani kama zilizovyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, Serikali ipange utaratibu maalumu wa kuwasiliana na wafadhili kuhakikisha kuwa fedha zote wanazoahidi kuchangia maendeleo zinatolewa katika mwaka unaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Matumizi ya Kawaida zilitumika kugharimia usafirishaji wa chakula cha njaa, kuratibu na kusimamia Uchaguzi wa Ubunge wa Tunduru, kuandaa rasimu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Dawa za Kulevya Namba 9 ya mwaka 1995, kuratibu miradi ya Mfuko wa Dunia *(Global Fund)* na kusaidia uandaaji wa sera itakayosaidia waathirika wa UKIMWI katika sekta ya umma na kadhalika. Kamati inaridhika na kiwango cha utekelezaji kilichofikiwa. *(Makofi)*

Halikadhalika, Kamati ilipokea taarifa ya kazi zilizopangwa kutekelezwa chini ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2006/2007 kwa mafungu 37, 42 na 92 kwa kutumia fedha za ndani na za nje. Utekelezaji huo ulihusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu, Dar es Salaam, uendelezaji wa jengo la Chimwaga, programu ya uendelezaji wa mifumo ya Masoko ya Kilimo, ujenzi wa makazi maalumu ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, kugharimia Mpango wa Kudhibiti UKIMWI kwa Wabunge na Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikusanya maduhuli ya shilingi 2,111,268,341.30 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi 1,893, 574,000 na kwa hiyo, kuvuka lengo kwa shilingi 217,694,341.30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa mwaka 2006/07, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ushauri ilioutoa wakati wa kujadili Makisio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliishauri Serikali iandae tena ratiba itakayoainisha Wizara zitakazohamia Dodoma hatua kwa hatua. Kamati ilielezwa kuwa

uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma upo pale pale na kwamba Serikali ilikwishatamka bayana kuwa kasi ya kuhamia Dodoma itategemea kwa kiasi kikubwa uwezo wa uchumi wa nchi kugharimia zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu haikuridhishwa na jibu hili kutokana na ukweli kwamba Ofisi Kuu za Serikali na Wizara nyingi zimekuwa zikiwekeza katika ujenzi wa majengo ya ukubwa mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam. Kama ujenzi huo ungefanywa Dodoma, hatua kubwa ingekuwa imepigwa katika kuhamia Dodoma. Aidha, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (*CDA)* imekuwa ikipewa kiasi kidogo cha fedha kila mwaka ambacho hakisaidii katika kuandaa miundombinu ya kuiwezesha Serikali kuhamia Dodoma. Kwa mfano, katika makisio ya mwaka 2006/2007 *CDA* ilitengewa shilingi 427,945,000/= tu kwa ajili ya kuboresha mandhari na miundombinu ya mji wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhiki na kasi ya kuhamia Dodoma na sababu zinazotolewa kuhusu kasi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine tena iandae ratiba itakayowezesha kutekelezwa kwa azma hiyo katika kipindi kitakachopangwa ndani ya ratiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, Kamati yangu iliishauri Serikali iweke utaratibu ambao ungewezesha ruzuku ya pembejeo za kilimo kutolewa kwa nchi nzima na kupitia kwenye vyama vya ushirika. Kamati ilijulishwa kwamba suala hilo lilipelekwa kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kwamba utekelezaji wake ungeanza katika mwaka 2007/2008 na ungejumuisha mbolea, mbegu bora, dawa na miche. Hata hivyo, suala hili ni la muda mrefu na wanaofaidika zaidi ni wasafirishaji na walanguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishauri kwamba Tume ya Uchaguzi iangalie uwezekano wa kupanga tarehe ya Uchaguzi Mkuu iwe katikati ya wiki badala ya siku za Ibada. Kamati ilijulishwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya mashauriano na wadau mbalimbali wakati wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kabla ya kupanga tarehe ya Uchaguzi Mkuu ujao. Ushauri mwingine ulihusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na maoni na ushauri wa Kamati, mbali ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha uliopita, Kamati ilipokea maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 yakiwemo Matarajio ya Mapato na Mpango wa Maendeleo. Aidha, Kamati ilifahamishwa juu ya kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huo. Mwisho, Kamati iliombwa kupitisha jumla ya shilingi 165,391,789,500 kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kupitisha Makadirio hayo, Kamati ilikuwa na maoni na mapendekezo kadhaa katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Kwanza, kama tulivyoshauri kwa kirefu kuhusu kuhamia Dodoma, Kamati ilifikia hatua ya kuishauri Serikali kuangalia upya uamuzi wake wa kuhamia Dodoma. Kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (*CDA*) yametengewa shilingi 1,412,694,509/= kwa ajili ya kuboresha mandhari na miundombinu ya mji wa Dodoma. Kamati haikubaliani na maelezo ya Serikali kuwa azma ya kuhamia Dodoma ipo na kuzihamisha Wizara zote kutategemea uwezo wa Serikali kwa kuwa vitendo vinatofautiana na azma hiyo. *(Makofi)*

Kamati inashauri kuwa kwa kuwa rasilimali nyingi za Serikali zinaelekezwa kujenga ofisi za Serikali Dar es Salaam badala ya Dodoma, Serikali ihakikishe kuwa inawekeza Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inapenda kufafanua kuwa kwa muda mrefu Serikali imeonyesha nia yake ya kuhamia Dodoma. Mchakato huo sasa umechukua muda mrefu kiasi cha wananchi wengi nchini kuonyesha wasiwasi kama kweli nia hiyo ya Serikali ipo. *(Makofi)*

Katika Bajeti ya mwaka 1995/1996, Serikali ilianza hata kutangaza baadhi ya Wizara zinazohitajika kuhamia Dodoma kwa awamu. Zoezi hilo lilifanyika kwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maji, Wizara ya Ushirika na Masoko na kadhalika. Dalili hizo zinaonekana kufifia kwa kuona kwamba hata hizo zinazoonekana kuhamia Dodoma kwa kiasi kikubwa zinaendelea kufanya kazi zake Dar es Salaam badala ya Dodoma. Mategemeo ya wananchi wengi ni kuona kwamba toka mwaka 1995 hadi sasa Wizara zote zingekwishahamia Dodoma. Cha kusikitisha zaidi ni jinsi Serikali inavyoendelea kujenga miradi mingi ya Serikali Dar es Salaam badala ya Dodoma. Mfano ulio dhahiri ni ujenzi wa nyumba za Mawaziri zipatazo 80 zilizojengwa Dar es Salaam badala ya Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Kamati yangu inapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa busara wa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma kinachotegemewa kuchukua wanafunzi 40,000/= kitakapomalizika. Chuo hicho kinategemewa kuanza rasmi mwezi Septemba, 2007 kikianza na wanafunzi 1,000. Hili ni jambo la kupongezwa na Watanzania wote kwani ile dhana ya Makao Makuu Dodoma hapa Rais ameionyesha kuitekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuiomba Serikali kutimiza wajibu wake na dhamira yake ya kuhamia Makao Makuu Dodoma kama ilivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilijadili kwa kirefu na kina juu ya utaratibu unaotumiwa na Serikali kutumia fedha za MMEM na MMES shuleni. Kwanza, Kamati inaridhika kwamba Serikali za Mitaa zinatumia fedha zake nyingi kujenga shule

za msingi na za sekondari na zinatumia watumishi wake kusimamia ujenzi huo. Kamati inazipongeza Serikali za Mitaa wakiwemo Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani kwa kusimamia ujenzi wa shule hizi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupitisha fedha za MMEM kwenye Halmashauri za Miji na Wilaya kwenda kwenye shule za msingi zinazohusika ni mzuri na umekuwa na matatizo madogo na machache. Utaratibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa kupitisha fedha za MMES kwenye shule za sekondari umekuwa na matatizo mengi na umesababisha malalamiko mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba Halmashauri za Miji na Wilaya zinatumia fedha zake nyingi kugharamia ujenzi wa shule za sekondari na kwa kuwa Mamlaka hizo zinatumia uwezo wake kuhimiza wananchi kuchangia ujenzi wa shule hizo kwa hali na mali; na kwa kuwa mamlaka hizo zina wahandisi na wasanifu wa majengo na wahasibu wenye sifa zitakiwazo, Kamati inashauri kuwa fedha za MMES zipelekwe kwenye Halmashauri za Wilaya ambako kuna vyombo vya sheria na usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Kamati yangu ilijielekeza linahusu Tume ya Uchaguzi. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Tume katika chaguzi zilizopita, ukiwemo Uchaguzi wa Tunduru, Kamati imeona kuwa bado kuna dosari ndogo ndogo ambazo hazina budi kufanyiwa kazi. Dosari moja kubwa ni ile ya kutokuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba majina ya wananchi wanaopata sifa za kupiga kura yanaingizwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura mara wanapopata sifa hizo ili kuwawezesha kushiriki katika chaguzi zinazofuata na wakati huo huo kuwaondoa kwenye daftari watu wanaopoteza sifa za kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa utaratibu wa kuwaingiza kwenye daftari watu wanaopata sifa za kuwa wapigakura, kunawanyima haki yao ya Kikatiba ya kuchagua wawakilishi wao. Kamati inashauri kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ibuni utaratibu utakaoondoa dosari hii kwa kuhakikisha kwamba Daftari la Kudumu la Wapigakura ni kamili na sahihi nyakati zote. Aidha, kuwe na utaratibu wa kupata vitambulisho vya Kitaifa ili kuhifadhi vizuri kumbukumbu katika daftari hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lililozua mjadala kwenye Kamati yangu ni lile la utaratibu wa Serikali wa kushughulikia maafa na majanga mengine yanayotokea kwenye Taifa letu. Ni maoni ya Kamati yangu kwamba Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuridhisha na kupongezwa katika kushughulikia tatizo la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiit, ni maoni ya Kamati pia Serikali haina maandalizi madhubuti ya kushughulikia aina nyingine za maafa na yanapotokea yanakuwa na athari kubwa kwa jamii na Serikali inaonekana kama haitoi umuhimu wa kutosha.

Kamati inashauri kwamba Serikali ifanye maandalizi madhubuti ya kupambana na maafa na majanga mengine katika ngazi zote ili kupunguza athari za majanga hayo kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linahusu jitihada za Serikali kuhusu kudhibiti maambukizi ya VVU na tatizo la UKIMWI. Kamati inatambua kwamba hadi sasa juhudi kubwa zimefanyika kuwaelimisha Watanzani kuhusu athari za ugonjwa huu kupitia vyombo vya habari, semina na kadhalika. Hata hivyo, pamoja na fedha nyingi zinazotolewa kukabiliana na ugonjwa huu, tatizo la UKIMWI bado linaendelea na baya zaidi wapo baadhi ya Watanzania walioathirika wanaodiriki kuwaambukiza wenzao kwa makusudi na kuzidi kuueneza ugonjwa huu.

Kamati inaamini kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI bado inao uwezo wa kukabiliana na hali hii. Kamati inashauri kuwa Serikali itunge sheria maalumu ambayo pamoja na mambo mengine, itawezesha kuwachukulia hatua wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la dawa za kulevya, Kamati iliona kwamba udhibiti wa dawa hizo umeelekezwa zaidi kwenye viwanja vya ndege kuliko kwenye maeneo mengine zinakoingilia dawa hazo. Kutokana na athari kubwa za dawa hizo kwa kizazi cha sasa na kijacho, Kamati inashauri kuwa Serikali ivishirikishe vyombo vyake vyote vya ulinzi na usalama kuwadhibiti waletaji, watumiaji na walimiki wa dawa hizo na kuwachukulia hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Aidha, uwekwe utaratibu wa kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya kupitia kwenye mipaka yetu yote. Uwekwe utaratibu utakaowapa wananchi vivutio vitakavyowafanya watoe taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama juu ya masuala yanayohusu dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Dodoma inahudumiwa na vyombo viwili ambavyo havina utaratibu mzuri wa kuainisha na kuratibu shughuli zake kwa manufaa ya wakazi wa Dodoma na kuuandaa mji huo kuwa Makao Makuu ya Taifa. Vyombo hivyo ni Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu *(CDA)*. *(Makofi)*

Kamati inashauri kwamba Serikali iangalie upya uhusiano kati ya vyombo hivyo utakaoshirikisha vyombo hivi katika ujenzi wa Manispaa ya Dodoma. Aidha, utaratibu wowote utakaowekwa uhakikishe kwamba wawakilishi wa wakazi wa Dodoma wanapata fursa za kujadili na kuidhinisha mipango ya kuendeleza Manispaa ya Dodoma, hususan ile inayogusa ustawi na maisha ya wakazi wa mji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maoni na ushauri wa Kamati yangu ilioutoa wakati ilipochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mafungu niliyoyataja hapo mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba nizungumzie Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo mwanzo, Kamati yangu ilitenga jumla ya siku mbili kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwanza, kutokana na majukumu mengi iliyonayo yanayowagusa wananchi walio wengi na pili, kulingana na uzito wa kuyashughulikia Makadirio hayo ikiwa ni pamoja na yale ya mikoa 21 ya Tanzania Bara ambayo Kamati iliyapitia kwa kina. Kazi hii ilifanyika katika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, tarehe 5 na 6 Juni, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Juni, 2006, Kamati yangu ilipokea maelezo ya utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2007/2008. Maelezo haya yaliwasilishwa na Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri wa Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, akisaidiwa na Mheshimiwa Celina Kombani, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Aidha, baada ya maelezo hayo, Kamati ilipokea taarifa za Mikoa 21 ya Tanzania Bara zilizowasilishwa na Wakuu wa Mikoa inayohusika. Nawapongeza sana Wakuu wa Mikoa kwa kusimamia maendeleo katika Mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitengewa jumla ya shilingi 43,838,462,000/= kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo, ruzuku kwa taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2007, jumla ya shilingi 36,717,924,822/49 sawa na 84% ya kiasi kilichotengwa zilikuwa zimetolewa na kutumika kama ifuatavyo, Mishahara, shilingi 886,501,687/50 na matumizi mengineyo shilingi 35,831,423,134/94. *(Makofi)*

Kwa upande wa Mikoa, jumla ya shilingi 60,514,146,000/= zilitengwa, mishahara, shilingi 38,160,280,000/= na matumizi mengineyo shilingi 22,353,866,000/=. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, jumla ya shilingi 49,678,951,852/= zilikuwa zimetolewa na kutumika kwa Mishahara, shilingi 27,697,252,852/= na matumizi mengineyo shilingi 21,981,699,000/=. *(Makofi)*

Kwa upande wa Serikali za Mitaa, jumla ya sh. 730,285,274,000/= zilitengwa: mishahara, sh. 576,648,574/= na Matumizi Mengineyo, sh. 154,636,700,000/=. Hadi Aprili, 2007 jumla ya sh. 596,528,438,581 (sawa na asilimia 82 ya kiasi kilichotengwa) zilikuwa zimepokelewa na kutumika: Mishahara, ilikuwa ni sh. 472,707,180,281/= na Matumizi Mengineyo, sh. 123,821,258,300/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/07, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitengewa jumla ya sh. 144,980,264,400/= kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo, sh. 4,371,996,000/= zilikuwa fedha za ndani na sh. 140,608,268,400/= fedha za nje. Hadi Aprili, 2007, sh. 4,033,000,000/= fedha za ndani na sh.105,826,003,360/= fedha za nje, zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa na Serikali za Mitaa, zilitengewa jumla ya sh. 48,796,439,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo na sh. 22,664,996,000/= fedha za ndani na sh. 26,131,443,200 fedha za nje. Hadi Aprili, 2007, sh. 22,664,996,000/= fedha za ndani na sh. 17,065,742,285/= fedha za nje, zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/07, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikadiriwa kukusanya mapato ya sh. 23,000,000/= wakati mikoa ilikadiriwa kukusanya jumla ya sh. 3,801,000/= na Serikali za Mitaa, sh. 66,008,661,029/=. Hadi Aprili, 2007, Wizara ilikuwa imekusanya sh. 19,321,214/95, Mikoa, sh. 3,800,000/= na Halmashauri, sh. 47,417,165,293/= sawa na asilimia 72 ya makadirio yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa zilifanikiwa kutekeleza majukumu yaliyokuwa yamepangwa kwa mwaka wa 2006/2007, ikiwa ni pamoja na kubadili Mfuko wa Akiba za Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) kuwa Mfuko wa Pensheni, kununua na kusambaza magari 33 kwenye Vituo vya Afya na magari 85 ya Wakuu wa Wilaya, kuwalipa watendaji wa vijiji 9,700 kupitia Mfumo wa kompyuta wa Hazina na kazi nyingine zilizokuwa na malengo ya kujenga na kuimarisha uwezo wa kutoa huduma bora kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/08, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inakusudia kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyokuwa mwaka jana. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu inakusudia kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa ofisi za Wabunge, kwa kujenga ofisi 40, kujenga nyumba za Wakuu wa Wilaya, maboma na Ofisi za Halmashauri za Wilaya mpya 11, kukarabati hospitali za mikoa kumi na moja na kuanza utekelezaji wa Mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kujadili Makisio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka wa 2006/2007, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo 14. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alitoa taarifa ya utekelezaji wa ushauri huo kama ifuatavyo:

Kamati ilishauri kwamba kuwepo na programu maalumu ya kuendeleza mikoa yenye maendeleo duni na kwamba katika mwaka wa fedha 2007/08, fedha za kutosha zitengwe kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na kuimarisha miundombinu ya Mkoa wa Rukwa. (*Makofi*)

Waziri alieleza kwamba Serikali imeachana na dhana ya kuandaa mipango maalumu ya maeneo na badala yake rasilimali zinagawiwa kwa kuzingatia vigezo maalumu vinavyojumuisha hali ya uchumi, idadi ya watu, ukubwa wa eneo na hali ya vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano. Aidha, Mikoa na Serikali za Mitaa zimeongezewa fedha kwa kuzingatia mazingira ya Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Manyara ujenzi wa Makao Makuu ya Mkoa unaombewa sh. 885,000,000/= katika bajeti ya mwaka wa 2007/2008 na katika mwaka wa 2006/2007 shilingi bilioni 1.6 zimehamishiwa kwenye mradi huo na kufanya fedha zote kuwa sh. 2,485,000,000/= ambazo zinatosha kukamilisha ujenzi wa jengo na kuweka huduma zinazohitajika.

Kamati ilishauri kwamba Wakuu wa Wilaya wapewe magari mapya na vitendea kazi vifaavyo kuwawezesha kutoa huduma bora. Mheshimiwa Waziri alitoa taarifa kwamba magari yamekwishanunuliwa na yamekwishawasili nchini. Mikoa imeongezewa fedha za matumizi ya kawaida kwa shilingi bilioni 1 kutoka sh. 6 bilioni hadi sh. 7 bilioni kwa mwaka wa fedha 2007/2008 jambo ambalo litawawezesha Wakuu wa Wilaya kutekeleza kazi ipasavyo.

Vilevile Kamati iliishauri Serikali kwamba Ofisi za Wabunge zipatiwe huduma na vitendea kazi vya kisasa. Mheshimiwa Waziri, alitoa taarifa kwamba kwa mwaka wa 2007/2008, Ofisi hizo zimetengewa jumla ya sh. 398,641,000/= kupitia kwenye makisio ya mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishauri kwamba utaratibu wa kutoa fedha za MMEM na MMES utazamwe upya na uzingatie kuwepo kwa Mamlaka zenye uwezo wa kuzisimamia.

Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba utaratibu uliopo hauna tatizo na kwamba utaratibu wa kutoa fedha za MMES ni kwa mujibu wa Mkataba na Wahisani. Kamati inakubali kwamba utaratibu wa kutoa fedha za MMEM hauna matatizo makubwa kwa kuwa unatumia uwezo uliopo kwenye Halmashauri za Wilaya na Miji.

Kamati haikubali kwamba utaratibu wa kutoa fedha za MMES hauna matatizo. Utaratibu huo una matatizo makubwa. Tunaheshimu mikataba na wahisani, lakini tunashauri kwamba wahisani washauriwe ili wakubali utaratibu huo ubadilishwe ili ufanane na ule wa MMEM wa fedha hizo kupitishwa kwenye Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilishauri kwamba kutokana na majukumu mengi waliyonayo Madiwani, Serikali iangalie uwezekano wa kuwaongezea posho. Mheshimiwa Waziri aliijulisha Kamati kwamba Serikali imekubali kurekebisha posho za kuwalipa Waheshimiwa Madiwani na kuangalia uwezekano wa kuwalipa kiinua mgongo wanapofikia mwisho wa kipindi cha Udiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya mapendekezo ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu, imeyafanyia kazi. Kwa jumla ushauri wa Kamati ulishughulikiwa ipasavyo hata kama Kamati haikukubaliana na maelezo yote yaliyotolewa na upande wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 Kamati ilijulishwa juu ya kazi mbalimbali zilizopangwa kufanywa katika Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri, na mwisho Kamati yangu iliombwa ipitishe jumla ya shilingi 1,508,249,380,000 (trilioni moja, mia tano na nane bilioni, mia mbili na arobaini na tisa milioni mia tatu na themanini elfu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 baada ya kupokea maelezo hayo Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa. Kwanza, ni kuhusu mgawanyo wa rasilimali za maendeleo katika mikoa. Kama tulivyoshauri katika taarifa yetu ya mwaka uliopita kwamba kuwe na programu maalumu ya kuendeleza mikoa yenye maendeleo duni, Kamati yangu bado inasisitiza kuwa pamoja na vigezo vilivyotumika kugawa rasilimali za taifa Mikoani, Mikoa ambayo ipo nyuma kimaendeleo izidi kupewa kipaumbele katika Bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Dar es Salaam zipo Mamlaka nne: Halmashauri ya Jiji na Halmashauri za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke. Halmashauri ya Jiji ilianzishwa kama chombo cha kuunganisha na kuratibu shughuli za Manispaa ili kuhakikisha kwamba Jiji la Dar es Salaam linaendelezwa kwa utaratibu ulioratibiwa vizuri.

Aidha, Halmashauri ya Jiji ina jukumu la kusimamia shughuli zinazohusu zaidi ya manispaa moja, jiji lote au ambazo zinaweza kutekelezwa kwa ufanisi zaidi na Mamlaka moja kwa niaba ya Manispaa. Halmashauri ya Jiji ina wajibu wa kuliwakilisha Jiji la Dar es Salaam ndani na nje ya nchi.

Kwa bahati mbaya sana haukuwekwa utaratibu ambao ungewezesha Halmashauri ya Jiji kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa, matokeo ni kwamba uhusiano kati ya Mamlaka hizo unategemea sana hisani, na Halmashauri ya Jiji imekuwa chombo kinachoendeshwa kwa gharama kubwa lakini chenye manufaa madogo kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaridhika kwamba Halmashauri ya Jiji ina nafasi muhimu katika maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam na inaihimiza Serikali ichukue hatua za haraka kurekebisha dosari zilizopo kwa kuweka utaratibu wa kisheria wa mahusiano miongoni mwa mamlaka za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Mkutano wa Saba wa Bunge, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya miradi ya Jiji la Dar es Salaam, likiwamo Shirika la Masoko ya Kariakoo. Kamati iligundua matatizo mengi ya kiutendaji ikiwa ni pamoja na

Shirika kuendeshwa kwa hasara, tatizo ambalo linatokana na Shirika hilo kukosa usimamizi madhubuti kwa kuwa Shirika linamilikiwa na Serikali Kuu asilimia 49 na Halmashauri ya Jiji asilimia 51. Uongozi wa Shirika unakataa kutambua milki ya Halmashauri ya Jiji na unadai kuwajibika kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba nafasi za uongozi kwenye Shirika ambazo zinashikiliwa na maafisa wanaokaimu, zitangazwe na zijazwe na watumishi watakaoajiriwa na Shirika. Aidha, Serikali ikubali kulimilikisha Shirika kwa Halmashauri ya Jiji kwa asilimia 100, jambo ambalo linaendana na sera ya Serikali ya kujitoa kushiriki moja kwa moja kwenye biashara na uzalishaji. Kamati inashauri kwamba utaratibu huu utumike kwa mashirika mengine yanayomilikiwa kwa pamoja na Serikali na Halmashauri ya Jiji, likiwamo Shirika la Usafiri la Dar es Salaam (*UDA*). Ni wajibu wa kisheria wa mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma zinazotolewa na mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla, kwa hatua zinazochukuliwa kupunguza tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa *Njia Tatu* asubuhi na jioni na mpango wa mabasi yaendayo kwa kasi. Ni dhahiri kwamba hatua zinazochukuliwa zitakuwa na manufaa katika kipindi kifupi kijacho. Inahitajika mipango mikubwa ya ujenzi wa barabara, *fly-overs* na reli ili kusafirisha abiria na mizigo yao na kudhibiti msongamano wa magari Jijini kwa muda mrefu zaidi. (*Makofi*)

Aidha, kuna haja ya kuchukua hatua za haraka kulipanga jiji la Dar es Salaam ipasavyo na kujenga miundombinu ya kukidhi mahitaji ya wakazi wa Jiji hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilijadili umuhimu wa kiuchumi wa barabara za Manyoni - Singida na Iringa – Dodoma - Babati na Babati - Singida. Kamati imebaini kuwa barabara hizi zinapita kwenye maeneo yenye rasilimali nyingi ambazo kama zingetumiwa vema zinaweza kuongeza pato la Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Kamati inashauri kuwa Serikali Kuu na mamlaka za Mikoa ya Iringa, Dodoma na Singida, zishughulikie ujenzi na ukarabati wa barabara za Manyoni - Singida, Iringa – Dodoma - Babati na Babati - Singida ili ziweze kuwa viungo na vichocheo vya maendeleo ya Mikoa hiyo na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maeneo ambayo Kamati yangu ilijielekeza kuyatolea maoni na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya sh. 1,508,249,380,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Mipango ya Maendeleo. Maombi hayo yamegawanyika ifuatavyo:

(a) Kuhusu Matumizi ya Kawaida, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sehemu ya Sera, Bunge na Uratibu (Mafungu 25, 27, 37, 42, 61 na 92) inaombewa jumla ya sh. 91,214,719,000.00

kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida: Sh.10,440,231,000.00 zinaombwa kwa ajili ya mishahara na sh. 80,772,488,000/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu sehemu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaombewa fedha chini ya Sehemu tatu. Sehemu hizo kwa pamoja zinaombewa jumla ya sh. 1,073,684,704/= kama ifuatavyo:

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaombewa jumla ya sh. 89,362,431,000: Mishahara inaombewa sh. 2,066,977,000/= kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na sh. 4,369,984,000/= kwa ajili ya mashirika yaliyo chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, jumla sh. 6,436,961,000/=. Matumizi mengineyo yanaombewa sh. 82,925,470,000/=.

(ii) Mikoa (Mafungu 70-89 na 95) inaombewa jumla ya sh. 83,058,794,000/=: Mishahara, sh. 38,800,794 na Matumizi Mengineyo, sh. 44,258,000,000/=.

(iii) Serikali za Mitaa zinaombewa jumla ya sh. 810,050,760,000/=. Mishahara inaombewa sh. 626,050,760,000/= na Matumizi mengineyo yanaombewa sh. 184,000,000,000/=.

(b) Kuhusu Mipango ya Maendeleo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sehemu ya Sera, Bunge na Uratibu (Mafungu Na.37, 42, 91 na 92) inaombewa jumla ya sh. 74,177,070,500/=: Sh. 5,064,000,000/= fedha za Ndani na sh. 69,113,070,500/= fedha za Nje.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaomba jumla ya sh. 434,562,676,000/= kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Maombi hayo yamegawanyika katika mafungu mawili: Ofisi ya Waziri Mkuu na Mikoa:

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu inaombewa jumla ya sh. 27,903.339,000.00, kati ya hizo Sh. 4,,535,000,000.00, fedha za Ndani na sh. 23,368,339,000.00 fedha za nje.

(ii) Mikoa inaombewa jumla ya sh. 332,482,266,000/=: Sh. 53,264,996,000 fedha za Ndani na sh. 279,217,270,500/= fedha za nje.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makusanyo ya Maduhuli katika mwaka wa Fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37), Mfuko wa Bunge (Fungu 42), na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61) inatarajia kukusanya jumla ya sh. 2,449,955,000 kama ifuatavyo:

- Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)
  - Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali sh. 1,926,106,000.00
  - Idara ya Utawala sh. 8,296,000.00
  - Ustawishaji Makao Makuu Dodoma sh. 510,000,000.00
- Mfuko wa Bunge sh. 1,002,000.00

- Tume ya Taifa ya Uchaguzi sh. 4,551,000.00

Kwa upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:-

- Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa sh. 31,030,000.00
- Mikoa sh. 4,288,000.00
- Halmashauri (fedha hizi ni kutokana na sh. 541,161,056,227.00 vyanzo vya Halmashauri, *Dev. Grants, Sector Basket, PADEP, TASAF, D by D* na kadhalika)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Pili, napenda nimshukuru Mheshimiwa Batilda Salha Burian, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mheshimiwa Mizengo Pinda, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), na Mhe. Celina Kombani, (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Makatibu Wakuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Idara, Taasisi na Vitengo na wataalamu wao wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano wa kutosha walioutoa kwa Kamati na kuiwezesha kutoa maoni yaliyoboresha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri ya kuchambua Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa muda wote wa siku tatu. Umakini na uzoefu wao wa muda mrefu katika maeneo mbalimbali ya Serikali na Halmashauri zake ndio uliofanikisha kazi hii. Naomba kuwatambua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Kh. Juma.

Wengine ni Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa. John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. (*Makofi*)

Vilevile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Emanuel Mpanda, kwa kuihudumia Kamati na kutayarisha Taarifa ya Kamati hii mapema kama mnavyoiona leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti Lubeleje, amewasilisha Hotuba ya Kamati yake kwa kumalizia na kuliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2007/2008.

Sasa aliyekuwa anafuata ni msemaji wa Kambi ya Upinzani na nimepata *note* hapa ya Mwenyekiti wa Kambi hiyo kwamba kuna marekebisho ambayo wanalazimika kuyafanya kwenye hotuba waliyokuwa wameiandaa mwanzo.

Mkisoma Kanuni zetu, Kanuni ya 21, inasema Bunge litaendelea kukutana mpaka ifikapo saa saba mchana isipokuwa kwamba Spika akiona inafaa aweza kusimamisha shughuli za Bunge wakati wowote kabla ya saa saba mchana hadi saa kumi na moja jioni.

Kwa kufuata utaratibu huo nimepata mawasiliano kutoka kwa Mheshimiwa Spika, kwamba amekubaliana na hoja zilizotolewa kwamba shughuli hizi zisitishwe hadi saa kumi na moja jioni na tutaanza na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwa ajili hiyo basi naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*(Saa 6.25 Mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta Alikalia Kiti)*

## HOJA ZA SERIKALI

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Nadhani watakuwa ni wawili, ni mmoja! Kwa hiyo, Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, ahsante sana!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niombe msamaha kwamba tulipaswa kufuta sehemu ya hotuba yetu kwa sababu baada ya hotuba ya Waziri Mkuu tulipaswa kuingiza mambo mengine ambayo hatukuwa nayo. Hii inatufundisha kwamba kwa siku zijazo ni vizuri tukaiga utaratibu ulioko Zanzibar ambapo Kanuni inataka hotuba ya Msemaji wa Serikali ipewe kwa upande wa Upinzani ili wajiandae vizuri angalau siku mbili. Labda hili ndilo la kuangalia kwenye Kanuni yetu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, 2007/2008, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 43(5)(c) na 81(1) , Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru wananchi wa Karatu walionichagua kwa kipindi cha tatu kuwa Mbunge wao. Ninawashukuru hasa kwa imani waliyokuwa nayo siyo kwangu tu, bali pia kwa Madiwani wetu wa CHADEMA kiasi cha kukifanya kwa mara nyingine tena CCM kuwa Chama Cha Upinzani Wilayani Karatu. Tunawapongeza sana wananchi hao kwa kuona tofauti ya dhahiri kati ya uongozi wa CCM na wa Chadema. Wameona kwa vitendo maendeleo ambayo kwa miaka 40 chini ya CCM hawakuyapata. Mimi pamoja na Madiwani wangu wa CHADEMA tunawahakikishia kuwa hatutawaangusha na kuwa kama walivyofurahia matunda ya dhamana waliyotupa kwa maana ya maendeleo yanayoonekana, kwa kipindi hiki pia tutafanya kila jitihada kutimiza ahadi zetu mbalimbali kwa mujibu wa ilani tuliyoiuza wakati wa kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo huo, nawapongeza pia Wananchi wa Bariadi kwa kuichagua UDP na kuifanya pia ‘Chama Tawala’ Bariadi. Natambua kuwa dhana hii ni mpya kwa wengi wetu. Wanaofahamu Demokrasia vizuri wanajua kuwa uwezekano upo wa chama kimoja kushinda uchaguzi kitaifa, na vyama vingine vikashinda na kuwa na madaraka ya uongozi katika ngazi mbalimbali za Serikali za chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa namna ya pekee sana wananchi wa Pemba, ambao kwa uamuzi na hiari yao wamekifanya CUF kuwa ‘Chama Tawala’ Pemba. Ni imani yangu kuwa Serikali Kuu itaheshimu daima maamuzi haya ya Wananchi na kujenga nchi ya Demokrasia ya kweli. Ninawapongeza vile vile Madiwani wa CHADEMA na wa CCM Kigoma ambao wametoa funzo kubwa kwa Tanzania nzima kwa kuwezesha kuundwa kwa Baraza la Madiwani Mseto, baada ya kuwa na nguvu zinazolingana. Hili ni funzo kwa vile wako wanaofikiri hakuna uwezekano wa Serikali ya Mseto Tanzania hata kabla ya kuifanyia marekebisho makubwa Katiba na Sheria zetu mbalimbali. Kama Kigoma utawala wa pamoja umewezekana baina ya CCM na CHADEMA, hivi Zanzibar inashindikana nini baina ya CCM na CUF? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika hotuba yangu mwaka uliopita, ninatoa tena mwito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na CCM kuwa njia pekee ya kupeleka maendeleo ya nchi yetu mbele 'ni kuanzisha rasmi na kwa vigezo vilivyo wazi vya mashindano ya maendeleo kati ya Wilaya zinazoongozwa na Upinzani na zile zinazoongozwa na 'Chama Cha Mapinduzi' ilimradi kuwe na uwiano wa rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashindano haya yatatoa kwa wananchi nafasi ya kupima utendaji kati ya Halmashauri zinazoongozwa na CCM na zile zinazoongozwa na vyama vingine. Huu ndio ukomavu wa kisiasa na demokrasia katika nchi yetu na ishara ya wazi kuwa Serikali na Chama Tawala kitaifa kweli vimedhamiria kimatendo kuruhusu mfumo wa vyama vingi nchini tofauti na hali ya sasa ambapo viongozi wa vyama vingine "wananunuliwa" au kurubuniwa kwa mbinu chafu kama ilivyotokea hivi karibuni kule Kigoma, au lile tukio la aibu na la kihistoria ambapo Mgombea U-meya kwa tiketi ya CCM, Bwana Nashon Bidyanguze alifanya jaribio la kumtorosha Diwani wa Chadema Bi Bahati Shabani Rehani toka Kigoma hadi Dar-es-Salaam kwa malengo ya kisiasa. Jambo ambalo ni kinyume kabisa na maadili mema. Kwa bahati mbaya wala hakuchukuliwa hatua ya kinadhamu au ya kimaadili na chama chake licha ya kukiaibisha na kuliabisha taifa zima kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Pinda Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Manaibu wao, Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote kwa Bajeti iliyowasilisha Bungeni hivi punde. Napenda kuwapa pia pole kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa shukrani iwapo sitakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie hekima na busara na kuwapatia nguvu na afya mnazohitaji katika kuliendesha vizuri Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya jumla ya bajeti 2007/2008. Kabla sijaanza kujadili hotuba ya Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

(i) Ninawasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu maoni ya chombo kinachojulikana kama 'Kambi ya Upinzani". Kambi ya Upinzani Bungeni inatambuliwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 11 hadi 13 na pia kifungu cha 83A, Toleo la 2004. Kambi ya Upinzani imetafakari kwa kina maana halisi ya maneno 'Vyama vya Upinzani', au "Kambi ya Upinzani" na kugundua kuwa maneno haya yana maana hasi katika mila na desturi za Mwafrika tofauti na neno '*Opposition'*. *(Makofi)*

(ii) Kilichofanya Kanuni ya sasa ya Bunge ni kuchukua tafsiri ya neno la Kiingereza ambayo katika falsafa ya Mwingereza haina maana sawa na 'kupinga' kama neno hilo linavyoeleweka kwa Mwafrika. Katika jamii ya

Kiafrika mtu anayepinga pinga mambo ni mtu mbaya sana anayestahili kutengwa. Lakini neno "*Opposition"* halina maana hiyo, na pia kwa wale wanaokuwa na matatizo na neno hilo wenzetu wanatumia zaidi neno "*Minority Party*" kuliko '*Opposition'*. Kwa vile suala la jina, ni uchaguzi wa mwenye jina hilo, tunawasilisha kwako kuwa Kambi ya Upinzani imebadilisha jina lake na sasa itakuwa inaitwa 'KAMBI YA USHINDANI' na tunapenda tutambulike hivyo. Maana halisi ni kuwa Vyama vya siasa huwa vinashindana kwa lengo la kutaka kuongoza Serikali tangu ngazi za chini, na kwa jumla kuingia IKULU. Vinakwenda kwa wananchi kushindanisha Sera na Ilani zao. Hivyo dhana ya Upinzani haiko kwa vile hakuna anayempinga mwenzake bali Vyama vinashindana. Ni imani yetu kuwa Ofisi yako itapokea jina hili jipya na litakuwa ndilo jina rasmi la Kambi yetu, baada ya marekebisho ya Kanuni za Bunge ambayo yanaendelea sasa. *(Makofi)*

(iii) Kwa vile jina "Vyama vya Upinzani" halitajwi popote kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wala Sheria ya Vyama vya Siasa, hatuoni kama badiliko hili linaweza kuwa na vikwazo. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye alinukuliwa na Gazeti la Rai wiki iliyopita kuwa "hata yeye hapendi jina "Vyama vya Upinzani" kwani inajenga dhana ya mtu au watu wanaopinga tu hata mambo ya maendeleo. Vyama vyetu pia vinaweza kwa wakati wao kuchukua jina hilo au jina lingine lolote linaloendana na falsafa na fikra za Mwafrika. Hadi hapo Kanuni zitakaporekebishwa, tutaendelea kutumia neno 'Kambi ya Upinzani', lakini ikieleweka kwa tafsiri hii ya Ushindani na siyo "Kupingana". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya pili tangu Serikali ya Awamu ya Nne iliposhika uongozi wa nchi yetu. Kambi ya Upinzani inatoa maoni yake kwa kufanya tathmini ya Malengo na Mwelekeo wa kazi za Serikali katika vipindi mbalimbali vya nyuma ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne tangu iliposhika madaraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mipango, naona umezama kabisa katika gazeti. Hairuhusiwi. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Sikuelewa! Umemsahihisha kule, Samahani!

**SPIKA:** Alikuwa anasoma gazeti, kinyume cha Kanuni ya 50. *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Mheheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake anazungumzia mipango ya maendeleo kwa maana ya miradi ya maji, afya, na miundombinu, mathalan, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaeleza kuwa fedha shilingi bilioni 218, kwa ajili ya barabara kuu na bilioni 65 kwa ajili ya barabara za Halmashauri zote zimetengwa mwaka huu. Pamoja na kuwa kiwango hiki ni mara mbili ya kile cha mwaka 2006/2007 kama ilivyoonyeshwa katika ukurasa wa18 wa hotuba yake. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, fedha hizi ni kidogo sana, na ni kwa msingi huo mjadala huu hauwezi kufanyika bila kuunganisha na maoni tuliyotoa wakati wa Hoja ya Bajeti ya Waziri wa Fedha.

Waziri Mkuu anazungumzia suala la Watalii 644,124 ambapo kwa maoni ya Upinzani kiasi hiki ni kidogo sana, na isitoshe si fedha zote zinakusanywa kwa utaratibu aliowasilisha Waziri wa Fedha. Miradi hii yote inahitaji fedha nyingi. Hoja ya Bajeti Kuu imekwishapita, lakini kwa vile Waziri Mkuu ni kiungo, Kambi ya Upinzani inadhani tungeliongeza vianzio vingine kuongeza mapato ili miradi yote aliyotaja Mheshimiwa Waziri Mkuu tuitekeleze maradufu zaidi kuliko inavyopendekezwa na Serikali. Kambi ya Upinzani inafahamu kuwa Bajeti Kuu imeisha kupita, lakini kama Serikali ina nia njema hakuna kinachozuia Serikali kuleta ndani ya Bunge hili angalau *"Supplementary Budget". (Makofi)*

Mapendekezo ya Kambi Upinzani kama yalivyotolewa kwenye maoni yetu kwa Waziri wa Fedha tunayarudia tena sasa kwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali kwa lengo la kuibua mjadala na Serikali ikiona inafaa ilete hapa Bungeni *Supplementary Budget* kama tulivyoomba. Kwa kifupi maoni yetu haya katika ujumla wake ni kama ifuatavyo:-

Maoni ya Upinzani kuhusu Bajeti : Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Kanuni zetu ,Toleo la 2004, hazisemi kitu kuhusu Bajeti 'Mbadala'. Hili tulilisema wazi katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri Kivuli. Hatukutegemea kama hili litakuwa na mjadala tena. Hata hivyo, anayebishia dhana ya Bajeti 'mbadala' ni yule asiyefahamu utendaji kazi wa Bunge katika mfumo wa Vyama vingi. Bajeti mbadala kwa kifupi ni Maoni ya Kambi isiyo madarakani kuwa tungekuwa sisi na ridhaa ya kutawala tungelifanya mambo kwa utaratibu kama tunavyopendekeza. Bajeti ya Kiongozi wa Upinzani ilifanya hivyo na si zaidi. Mawazo ya kuwa hakuna Bajeti mbadala hadi uwe Serikalini ni mawazo potofu ya watu wasioenda na wakati, na wala hawafuatilii kinachoendelea duniani. *(Makofi)*

(a) Maoni ya Bajeti yaliyowasilishwa na Waziri kivuli yanaonyesha Kambi ya Upinzani ingelikuwa Serikalini ingeliweza kukusanya shilingi trilioni 5.3 badala ya trilioni 3.5 iliyopendekezwa kusanywa na Serikali . Maoni ya Bajeti ya Kambi ya Upinzani ni ziada ya trilioni 2.2., zaidi ya ile ya Serikali. Na hizi ni fedha ambazo Serikali ingelikuwa makini ingezikusanya kutoka rasilimali zetu za ndani, mathalan maliasili, madini yetu na vito, mifugo yetu, udhibiti wa misamaha ya kodi, kutekeleza na kusimamia sheria zilizopo vizuri zaidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, iwapo ziada hii itakusanywa ongezeko hili litatumika ipasavyo, na; au ziada inayopendekezwa kutafutwa kwa kutumia vianzio vipya vilivyopendekezwa na Kambi ya Upinzani vingeongezea

maradufu maeneo yote ya huduma za jamii yaliyotajwa katika hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa iwapo kutakuwa na *Supplementary Budget* na Serikali kukubali maoni ya Kambi ya Upinzani au kuyakataa na kuondoa wakati huo kodi ya mafuta ya taa, mapato haya yangeongezeka kufikia shilingi trilioni 5.3 bila kumgusa mwananchi wa kawaida zaidi ya kiwango cha kodi anazolipa sasa. Maoni haya Serikali ina haki ya kuyachukua au kuyakataa, lakini kwa vyovyote vile pia inaweza kufanya mabadiliko hata sasa kupitia *Finance Bill, 2007* ambayo itawasilishwa hapa Bungeni baada ya majadiliano haya ya bajeti. Serikali ikikubali maoni haya bila kuweka itikadi mbele, maana yake ni kuwa mipango mingi zaidi ya maendeleo itatekelezwa kuliko ilivyo katika Bajeti ya Serikali ambayo kwa bahati nzuri tuna uwezo wa kuijadili kwani hatua hii bado haijawa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Mwaka 2007 na kwa uzoefu nilionao ndani ya Bunge hili kuna mambo katika bajeti yalikwisharekebishwa kwa kutumia *Finance Bill* inayokuja siku ya mwisho ya Bunge.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 81(7), huu ndio ubunifu uliokosekana kwa upande wa Serikali. Mtu makini anayesikiliza, anayetafakari na kusikiliza mawazo mbadala, anayesikiliza kilio cha wananchi wa kona zote za nchi, asingelishindwa kutambua kuwa Bajeti iliyowasilishwa na Kambi ya Upinzani inapunguza utegemezi kwa wafadhili kutoka asilimia 42 ya sasa ya Serikali ya CCM kufikia asilimia 31.8.

Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa katika masuala makubwa kama haya yanayogusa maisha ya watu tusipende sana kuweka ushabiki wa kisiasa na itikadi mbele. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutambua mchango wa Viongozi wa vyama vya siasa pamoja na wananchi kwa ujumla katika kudumisha amani na utulivu nchini kama ilivyoelezwa katika hotuba yake ukurasa wa 6. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vile Ofisi yake ina jukumu la kuratibu mambo yote ikiwa ni pamoja na maendeleo, ni imani yetu kuwa kilio hiki kisikilizwe kwa umakini mkubwa na kupatiwa ufumbuzi ama katika Bunge hili au kwa njia ya *Supplementary Budget* au kama busara ya Ofisi yake itakavyoamua.

Hata hivyo, sisi tunawaachia Watanzania wachambue wenyewe jinsi bajeti hii ilivyowaacha hoi watu wa ngazi ya chini hasa katika suala la mafuta ya taa. Kazi yetu kama Kambi ya Upinzani ni kuwaonyesha Watanzania kuwa “Inawezekana kabisa kama tukiwa na uzalendo, tukipenda nchi yetu, tukiwa wabunifu na tukiacha kufanya kazi kwa mazoea”.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya Elimu, ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia sana mafanikio yaliyopatikana kwenye MMEM na MMES na sisi wa Upinzani tunaunga mkono hoja hiyo. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani ina maoni kuwa Wananchi hao sasa wameelemewa na michango, tena mahali pengine kama Bariadi inakusanywa kwa mabavu, ng’ombe wanakamatwa na kupigwa mnada chini ya bei ya soko. Hali hii si nzuri kwa ustawi wa watu wetu.*(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu! Kanuni ya 50(1), katika matamshi yake sasa hivi kuhusiana na Bariadi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ametamka kwenye eneo la elimu kwamba wananchi katika Wilaya hiyo wamelazimishwa kuchangia elimu. Naomba athibitishe Mezani hapa kama kweli hilo ndilo limetokea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Dr. Slaa kuna haja ya kuweka vizuri, ni usemi ambao ni mzito sana kwa nchi yetu, hapa hakuna mambo ya utumwa, ubavu na sasa kama haliwezi kuthibitika bora uliondoe. Pia nikukumbushe tu kwamba kodi ya mafuta ya taa ilikwishaondolewa lakini wewe umeitaja kama vile inaendelea. Nakusihi upunguze kuingia katika mjadala wa Bajeti kwa sababu kwa kanuni ya 49(6) naweza pia nikakuzuia sasa. Kwa sababu hatufungui upya mjadala kuhusu bajeti, nenda kwenye hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa maelekezo yako. Lakini labda niseme tu kwamba hoja hiyo ya Bariadi ilitolewa hapa na Mheshimiwa Cheyo, haikupingwa, kwa hiyo, tulichukua kwamba ndiyo hoja sahihi. Kitu kilichoko kwenye *Hansard* inachukuliwa kwamba ndiyo rekodi iliyoko na haikupingwa. Lakini kama inamkera Mheshimiwa Mbunge wa Bariadi Magharibi nitaiondoa.*(Makofi)*

**SPIKA:** Uiondoe tu haitusaidii sana, bado tuna muda, kama una ushahidi ama kama Mheshimiwa Mbunge wa Bariadi Mashariki atakaporejea labda atapenda kuianzisha, lakini kwa leo hebu twende moja kwa moja kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hilo, basi kwa maana hiyo kwa kweli mimi naomba niiondoe kwenye hotuba yangu lakini iko tayari kwenye rekodi. *(Makofi)*

Hoja ni kuwa ni kweli Mheshimiwa Spika, nimecheki pia kwenye Kanuni zetu kwa kuwa *Finance Bill* haikupita na kwa uzoefu wa *Hansard* ambazo nimezicheki nimeona kwamba masuala ya bajeti ambayo hayataki kuondoa Azimio lile la Bunge tulilopigia kura yanaweza kuzungumzwa, ndiyo sababu ninaongelea masuala ya Bajeti kwa maana ya kutoa pendekezo kwa kipindi kinachofuata. Lakini hatuongei kwa maana ya kufuta, lile Azimio lilipitishwa na Bunge na *Finance Bill* inakuja siku ya mwisho, lakini kama unanielekeza niondoe, basi nitaondoa.

**SPIKA:** Hapana wewe endelea, lakini nakuona unachukua muda mrefu kuchambua, tena kama vile tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hilo ndilo tatizo, lakini sijui huko unakoendelea kama litaendelea basi itabidi nikukatize.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Sawa.

Mheshimiwa Spika, hapa siyo kodi isitozwe , na wala wananchi wasilipe kodi. Hoja ni kuwa kuna kiwango cha kuwakamua watu maskini. Waziri Mkuu anafahamu kuwa Serikali hii hii, miaka michache tu iliyopita ilifuta kodi ya "Upe" ya sh. 2,000/= kwa vile wananchi wengi walikuwa wanashindwa kupeleka watoto wao shule kwa sababu ya sh. 2,000. Leo wanapigwa kodi lukuki, tena kwa njia mbaya kama kupandisha kodi ya mafuta ya aina zote, ambayo kimsingi inaathiri gharama zote za maisha. Waziri Mkuu amesahau kuwa takwimu zilizotolewa na Serikali inaonyesha kuwa asilimia 35.4 wako katika kiwango cha chini cha 'Mahitaji ya Msingi', yaani katika kila watu 100, watu 35.4 ni maskini wa kutupwa (Tazama Kitabu cha Hali ya Uchumi, ukurasa wa 93). Hawa ndio watu ambao Serikali kupitia Waziri Mkuu inataka waendelee kukamuliwa wakati kuna vianzio vingine vingi tu vinaweza kuliingizia Taifa mapato mengi? Wakati Kambi ya Upinzani inaunga jitihada hizi za kuimarisha Elimu inasisitiza kuwa vianzio vingine vitafutwe kama tulivyoelekeza kwenye maoni yetu ya Waziri Kivuli wa Fedha kwa njia tulizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kiunganishi muhimu katika Serikali, na ndiye anayesimamia mipango yote ya Serikali. Hivyo, ni vyema akalichukulia kwa uzito suala hili la kuongeza kodi na ikiwa lazima alete Bungeni *Supplementary Budget* itakayompunguzia makali mwananchi. Isitoshe Serikali isimamie kikamilifu udhibiti wa fedha na mabilioni yaliyokaa tu kwenye akaunti zilizofungwa miaka mingi. Kambi ya Upinzani siyo tu imeonyesha vipaumbele vilevile vilivyoonyeshwa na Serikali, bali tumeongeza kipaumbele kingine ambacho Serikali haikukiona, yaani 'Utawala Bora'.

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake wala hakuweka uzito wowote kwenye suala hili, wakati katika maeneo mengi Utawala Bora ni tatizo kubwa sana. Wakati Bajeti ya Serikali imetoa asilimia 18, kwa mfano kwa elimu, maoni ya Kambi ya Upinzani inapendekeza asilimia 20, miundombinu tumeipa asilimia 21, kilimo tumeipa asilimia 12 badala ya 6.2 na kadhalika. Hapa tunafikiria tukiungana wote kwa pamoja kazi hii tunaweza kuifanya maradufu na ikaongeza kasi yetu ya kuweza kupiga vita umaskini katika nchi yetu. Cherekochereko za Serikali za nini? Wakati viwango hivi ni tone la mchanga katika bahari ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, tungelipenda kupata fedha nyingi zaidi ili matunda ya MKUKUTA, MKURABITA yaonekane kwa watu wengi zaid. Kambi ya Upinzani pamoja na kutambua mchango wa Serikali wa shilingi bilioni moja kwa kila mkoa lakini takwimu zinazotolewa na Waziri Mkuu hazitii matumaini. Kwa fedha hizo ni watu kama 16,700 ndio waliofaidi fedha hizo (bilioni.11). Kwa utaratibu huu, Watanzania zaidi ya milioni 17 wanaohitaji kuwezeshwa watafikiwa lini? Serikali itupe majibu kwa hoja, isiwe kama alivyotujibu Waziri wa Fedha. wakati wa ushabiki umepita, kwani wakati tunaendelea na ushabiki wa kisiasa dunia haitusubiri, inaenda mbele.

Mheshimiwa Spika, tunaisihi Serikali tufanye kazi kwa uzalendo. Tungelipenda Waziri Mkuu, asimamie utaratibu wa kuongeza kiwango hiki ili kuhakikisha uchumi wetu unakua haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu kama mratibu wa masuala ya Bunge, tungependa pia atueleze ni kwa nini Serikali katika Bunge hili iliwasilisha vitabu vyenye utata ndani ya Bunge hili, kama vilivyowasilishwa na Waziri wake wa Fedha ambaye hatimaye alisema 'Kambi ya Upinzani haina Uzoefu'. Ukweli ni kuwa Alhamisi wakati waziri anasoma Bajeti yake alikuwa amegawa vitabu vya Bajeti *Volume 11* yenye *cover* ya *Pink.* Baada ya kusoma Bajeti yake amegawa *Volume 11* nyingine safari hii yenye *Cover Blue*. Vitabu hivi viwili vinatakwimu tofauti. Chukua mathalan Kasma ya 25 Ofisi ya Waziri Mkuu. Kitabu Pink wakati anasoma Bajeti yake ilikuwa na Makadirio ya Matumizi ya Jumla ya *(Net Total)* 4,011,489,000. Kitabu kilichotolewa baada ya Bajeti *(Blue)* kwa Kasma hiyo hiyo, kina jumla ya *(Net Total)* 3,372,489,000. Vote 37 Ofisi ya Waziri Mkuu, pia nayo vivyo hivyo. Kitabu kinaonyesha jumla ya shilingi 12,332,530,800 wakati kitabu *Blue* kinaonyesha shilingi 10,442,530,800. Kambi ya Upinzani inaomba huu basi urekebishwe angalau tungeelezwa kitu gani kimetokea na au kuombewa msamaha kama kumetokea tatizo. Sisi imetupa tatizo kwa sababu hatuwezi kuandaa hotuba yetu kama hatuna taarifa sahihi. Huu ndio utaratibu mzuri uliosemwa na Serikali kupitia Waziri wa Fedha na kuwa utaratibu wetu wa Bajeti unaeleweka vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Je Waziri Mkuu anafahamu kuwa kwa taarifa zilizoko Waziri wake wa Fedha ni Waziri wa kwanza tangu uhuru aliyewachanganya Wabunge kwa kutoa vitabu viwili kwa matumizi ya aina mmoja na wala hajaomba hata msamaha kwa wabunge kwa makosa hayo? Waziri Mkuu anajua kuwa sababu moja ya hali hiyo ni Serikali anayoisimamia kutokuwa makini wakati wa maandalizi kiasi cha kutokuweka fedha kwa miundo mbinu hadi Kamati ya Fedha na Miundombinu (ambamo na Wapinzani wapo) ziliposhinikiza kupatikana kwa fedha hizo. Inawezekana msukumo huo wa Kamati umesababisha kubadilisha vitabu hivyo. Lakini hata Taarifa basi. Waziri Mkuu anaategemea vipi kambi ya Upinzani kujiandaa vizuri iwapo yanatokea mabadiliko ya ghafla hivi? Hata Hotuba yake tunaipata ndani ya Ukumbi wakati amekwisha kuanza kuizungumzia. Tutengeneze mazingira mazuri zaidi ili Wabunge wote tutoe mchango mzuri zaidi na ulioandaliwa vizuri zaidi, wakati mwingine uungwana ni muhimu na hauna gharama licha ya kwamba unajenga kuheshimiana na kuaminiana badala ya kupigiana vijembe ndani ya Bunge kama ilivyotokea mara kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti iliyowasilishwa na Waziri Kivuli ni kielelezo kamili, na inagusia kwa kweli karibu maeneo yote ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyazungumzia, basi sitarudia katika kuchambua hotuba ya Waziri Mkuu, nitaingia katika kueleza yale maeneo tu ambayo sisi tunafikiri tunahitaji kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza kuwa maoni yetu ni msingi muhimu katika kuijadili hoja ya Waziri Mkuu. Sitahitaji kurudia kuchambua tena Bajeti ya Waziri Mkuu peke yake, bali tutaitazama katika mtazamo huo mpana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Waziri Mkuu ni msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni, na mjadala wa Waziri Mkuu unaihusu Serikali yote, tunapenda au yeye au kupitia Waziri wake wa Fedha tupate majibu ya kina ndani ya Bunge hili kuwa Waziri

wake alizungumza zaidi kisiasa bila kujibu hoja za msingi. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na wananchi wote wanaopenda kujua ukweli, tunaitaka Serikali sasa ituhakikishie yafuatayo:

(a) Serikali sasa ikanushe au itoe Tamko kuwa kiwango cha magogo kilichouzwa China cha *cu*.mita 18,316 X $150 kwa Taarifa za Tanzania, ambapo vitabu vya China vinaonyesha *cu*.mita 108,605 x $ 450, tungependa tupate taarifa ya kina kwa sababu hii itatusaidia katika kuweza kuelekeza ni namna gani eneo analozungumzia Waziri Mkuu tunapoweza kupata fedha za kuongeza maradufu. *(Makofi)*

(b) Iwapo takwimu hizo ni sahihi, au kama Serikali haina taarifa kamili kama alivyokiri Waziri wa Maliasili na Utalii, je, Serikali inakubali kuwa kulikuwa na uzembe katika kusimamia rasilimali zetu? Na je, wahusika wa uzembe huo wamechukuliwa hatua gani au watachukuliwa hatua gani ikizingatiwa kuwa Mheshimiwa Meghji alikuwa ndiye Waziri wa Maliasili na Utalii kwa wakati huo? Haiwezekani kuwaadhibu wananchi kwa kodi isiyo ya lazima wakati Serikali inaacha makusudi kuchukua hatua za udhibiti na usimamizi kama walivyokabidhiwa dhamana.

(c) Serikali itoe maelezo ya kina, kwa nini takwimu za Soko la Dunia zinaonyesha kuwa mauzo ya *Tanzanite* ambayo inapatikana Tanzania tu, tuna $ 400 milioni, wakati takwimu za Tanzania zinaonyesha $ 16 millioni tu. Hapa tunafikiria vile vile kazi aliyotaja Mheshimiwa Waziri Mkuu tutaichangia vizuri tukipata uhakika wa takwimu hizi na ni kwa nini kama takwimu za kwetu ziko chini, zimekuwa ni chini kiasi hicho ili tuweze kusaidia ni namna gani elimu yetu, maji yetu, na barabara zetu tuwezeshe kushauri zitengenezwe vizuri zaidi. *(Makofi)*

(d) Je, Serikali inasema nini, kwa Takwimu hizi tu bado kuna haja ya kumkamua mwananchi wa kawaida kupitia kodi ya mafuta ambayo hata sasa Serikali ilichofanya ni kiini macho kwa kuhamishia kodi ya mafuta ya taa ya shilingi 4 kwenye kodi ya mafuta aina ya petroli na dieseli. Serikali inafahamu kuwa kusafirisha mafuta ya taa unahitaji dizeli na kama gharama ya dizeli iko juu, hata ya mafuta ya taa haitashuka? Mwananchi wa kawaida ndiye atakayeendelea kuathirika.

(e) Mheshimiwa Spika, duniani kote Vyombo vya Habari ni mhimili wa Nne wa Serikali. Ndio wenye kudodosa na mara nyingi huwa wa kwanza kugundua upungufu wa Serikali kutokana na taaluma yao ya Uandishi, *(Investigative Journalism).* Vyombo vinavyosimamia utendaji wa Serikali, mathalani Wabunge hutumia Taarifa hizo kwa kuitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa mambo yaliyoko kwenye vyombo hivyo vya habari kujua ukweli. Waziri Mkuu analiambiaje Taifa sasa kuhusu hili? Je, vyombo vya Habari visitoe habari hata kama ina ukweli na manufaa kwa Taifa hili? Je, Serikali anayoisimamia sasa iko tayari kutangaza rasmi kuwa vyombo vya Habari vinafanya kazi pale tu vinapoisifu na kuipigia debe Serikali?

Mheshimiwa Spika, tunaisema hivi kwa sababu katika taarifa yetu pia hiyo imeonekana na Waandishi wa Habari walisemwa hapa kwamba wanapendelea upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imefarijika sana kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekiri kufahamu Taarifa niliyoitoa hapa Bungeni kuhusu ubadhirifu mkubwa ndani ya *BoT* unaomgusa Gavana wa Benki Kuu, pamoja na wafanyabiashara wengine wakubwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 50(1) fasili ya 8. Naomba mwongozo wako kwamba hivi ni kweli mtu ambaye hawezi kuingia hapa Bungeni kuweza kujitetea kuhusu tuhuma ambazo zinatolewa hapa dhidi yake, je, ni haki kujadiliwa humu ndani ya Bunge? Naomba mwongozo wako! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge anazungumzia ubadhirifu ndani ya *BoT*, kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kujibu, tumsikie anavyoendelea huko. Lakini anachozungumza siyo kumsema mtu kwa maana ya Gavana Balali kama mtu, ni suala la ubadhirifu katika *BoT,* hivyo ni halali aendelee. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sasa kwa kuwa siendani na muda wangu, naomba Meza yako inilinde ili muda wangu ambao ninasimamishwa basi uweze kufidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli ninazungumzia hoja hii ya *BoT* kwa maana ya ubadhirifu uliotokea, na hoja hizi ziko kwenye vyombo vya habari, kwa hiyo hatumsemi Gavana kama Gavana kama mtu binafsi tunaisema Ofisi yake na yeye ambaye ametuhumiwa na vyombo hivi. Kwa vile ninalenga kutoa hoja ndani ya Bunge hili la kuunda Kamati Teule, na kwa kuwa ni lazima kwa mujibu wa Kanuni mbunge awe amelizungumzia jambo hilo, naomba nilizungumzie sasa suala la *BoT* katika upana wake ili hatimaye kwa wakati unaofaa niweze kutoa hoja yangu hiyo.

Wakati akichangia hoja ya *BoT* siku ya tarehe 20 Juni, 2007, Mheshimiwa Mzindakaya alitoa tuhuma nzito dhidi ya Wabunge, na ninanukuu: "kama kuna mambo mazito na ambayo Mbunge angependa kuyasema, mimi nafikiri kuhutubia habari za intaneti haitoshi kuwa ndio ushahidi sahihi kwa sababu baadhi ya mambo tunayoyafahamu sisi wengine tumefanyia *research*… ..kwanza takwimu si sahihi. Takwimu sio dola milioni 200, ni dola milioni 131."

Kwa hiyo, anakubali kwamba kuna ubadhirifu ndiyo takwimu sahihi. La pili, "baadhi ya wafanyabiashara wanaweza wakatumia ujanja wa kuwatumia Wabunge waje wawasemee mambo yao au tofauti zao katika biashara. Na jambo hili linahitaji kuliangalia….. "Bahati nzuri", naendelea kunukuu, "habari hii naijua kutoka kwa mhusika mwenyewe". *(Makofi)*

Mambo kadhaa yanajitokeza na kwa kuwa yamesemwa Bungeni ni vema nikayazungumzia pia Bungeni kwa lengo la kujenga baadaye hoja ya Kamati Teule. Pamoja na hivyo, ninatumia Hoja ya Waziri Mkuu, kwa vile Waziri Mkuu ndiye msimamizi wa shughuli zote Bungeni, na ndiye peke yake anayeweza kuratibu suala zito kama hili. *(Makofi)*

Natambua kuwa Kanuni 50(6) ambayo inasema kwamba tusiwaseme watu walio nje na ikawataja watu hao, lakini pamoja na hayo kwa sababu hoja hii ni nzito na ninalenga kutoa hoja rasmi kwa ajili ya Kamati Teule, naomba sasa kwa ruksa yako niendelee ili niweze kutumia kifungu hicho.

(i) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 49(7), na ninaomba kunukuu, "Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi ya kifedha nalo, isipokuwa baada ya kutaja jinsi anavyohusika, na kiwango cha maslahi hayo". Mheshimiwa Mzindakaya hakutamka lolote kuhusu maslahi yake katika jambo hili. Nasisitiza toka awali kuwa hoja hapa siyo uhalali au vinginevyo wa Mheshimiwa Mzindakaya kukopa fedha. Tatizo ni suala la *Conflict of Interest* inayojitokeza kama nitakavyoeleza hapa chini na pia kuleta utata mkubwa kwa vile amekiri kuwa ubadhirifu/Upotevu ni Dola za Marekani 131 milioni tofauti na nilivyosema mimi, tena taarifa amezipata kwa "mhusika mwenyewe" kwa maneno yake mwenyewe. Mambo yanayomhusu Mheshimiwa Mzindakaya hayahitaji majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, isipokuwa akipenda kufanya hivyo. Hivyo basi...!

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Kanuni ya 50(3) inasema kuwa , "ni marufuku kwa Mbunge yoyote kuzungumzia jambo lolote ambalo langojea uamzi wa Mahakama, au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi, na vilevile ni marufuku kusema kwa lengo la kutaka kupinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo ufutiliwe mbali."

Wakati mzungumzaji anazungumza amegusa jambo ambalo lilikwisha kuzungumziwa katika Mkutano huu wakati tukijadili Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango lakini analizungumza tena wakati tunajadili Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika!

**SPIKA:** Waheshimiwa tusiwe wepesi kuzuia mjadala wa afya ndani ya Bunge kwa sababu hili jambo baada ya kuzungumzwa lilivyozungumzwa na Mheshimiwa mhusika, limezua kile ambacho anayezungumza sasa utashi wa kujua kama ilikuwa ni haki kusemwa kwa namna lilivyosemwa kwa mujibu wa kanuni hiyo anayoinukuu ya 49(7). Kwa hiyo, tumwache kwanza aendelee, tuna muda mrefu wa kuweza kujibizana. Ni vizuri tukapata mjadala wenye afya unaozingatia mambo yote kuliko kufupisha fupisha na kuzuia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Slaa naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ningeomba Waheshimiwa Wabunge wasome. Tunapendekeza kitu kipya, *Supplimentary Budget* haijaongelewa, hii kauli ya Kambi ya Upinzani kwamba ili tuweze kupata haya aliyosema Waziri Mkuu...!

**SPIKA:** Endelea na hoja!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nilikuwa nimeshafika mbali. Mheshimiwa Mzindakaya hakutamka lolote kuhusu maslahi yake katika jambo hili. Nasisitiza toka awali kuwa hoja hapa siyo uhalali au vinginevyo wa Mheshimiwa Mzindakaya kukopa fedha. Tatizo ni suala la *conflict of interest* inayojitokeza kama nitakavyoeleza hapa chini na pia kuleta utata mkubwa kwa vile amekiri kuwa ubadhirifu upo. Kwa kuwa ubadhirifu amekiri upo, ni suala la Bunge hili sasa kuona linasimamia namna gani.

(ii) Mheshimiwa Spika, utafiti wetu unaonyesha kuwa hapa naongelea suala la *conflict of interest* ambayo ilimfanya atetee. Utafiti wetu unaonyesha kuwa mwaka 2004 Mheshimiwa Mzindakaya alichukua Mkopo kwa shughuli za Kampuni yake Binafsi inayoitwa SAAFI wa shilingi 6.217 bilioni, uliogawanyika kama ifuatavyo. Aliomba '*Overdraft facility* ya 450 Milioni zitakazolipwa kwa miaka 5; Mkopo wa shilingi 2.8 bilioni zitakazolipwa katika miaka 5; na Dola za Marekani 2.528. Jumla yote ni bilioni 6.217. Fedha zote zilikopwa Benki ya *Standard Charter*. Benki Kuu ilitoa (*Guarantee)* mdhamana wa asilimia 100. Mwaka huu wa 2007 Benki Kuu kutokana na mdhamana huo tayari imelipa kiasi cha shilingi 8.1 bilioni kwa niaba ya Mheshimiwa Mzindakaya na fedha hizo pamoja na riba zinakisiwa kufikia 9.7 bilioni hadi sasa (Hati *Ref. CIBD-14662* ya tarehe 24 Mei, 2007) na mkopo kutolewa 2005.

(iii) Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)* ambako Gavana wa Benki ndiye Kiongozi Mkuu na ndiye mhusika mkuu katika tuhuma zilizotajwa, hivi sasa deni hilo limehamishiwa *TIB* ambako Mheshimiwa Mzindakaya ndiko anakotakiwa kulipia deni la *BoT*.

(iv) Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mheshimiwa Mzindakaya ameomba adhaminiwe na *BoT* mkopo mwingine tena wa shilingi billioni 2. Mkopo huo uko kwenye hatua ya kujadiliwa na *BoT* ama kuidhinishwa au hapana.

(v) Kauli ya Mheshimiwa Mzindakaya ambayo kimsingi ilielekezwa kwangu kwa vile ndiye niliyenukuu taarifa ya intaneti inataka kutoa dhana kwa Watanzania kuwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, nikiwemo mimi hatufanyi utafiti ila yeye tu ndiye anayefanya utafiti. Hili ni tusi kwa Bunge hili, kwetu sisi Wabunge mmoja mmoja na kwa Watanzania waliotutuma tuwasemee, na linalenga kuupotosha umma wa Watanzania kuwa kuna Waheshimiwa Wabunge wanakurupuka tu kusema mambo bila kufanyia utafiti.

(vi) Kauli yake ni tuhuma nzito hasa anapojenga uwezekano wa baadhi ya wabunge 'kutumiwa na Wafanyabiashara waje wawasemee mambo yao au tofauti zao za kibiashara'. Hii inajenga dhamira potofu kwa watanzania kuwa kuna wabunge hawana dhamira yao wenyewe, hawajui wanalolifanya ila wanatumika kama chombo, dhamira ya kutumika pia inaweza kueleweka kuwa wananunuliwa. Nayasema haya yote ili huko mbele niweze kujenga hoja yangu kwamba tunapotaka sasa iundwe Tume kuna msingi

sahihi na inaeleza ni kwa nini kulikuwa na *conflict of interest*. Hii ni kauli nzito sana kusemwa dhidi ya Mbunge yeyote, wa upinzani au wa Chama Tawala, kwa sababu wote ni Wabunge kama Mheshimiwa Mzindakaya, tumechaguliwa na Wananchi wetu kama Mheshimiwa Mzindakaya. Mheshimiwa Mzindakaya hajaeleza kwa nini awe na mawazo hayo potofu na hisia za sisi kuhongwa na kununuliwa. Lakini ukweli ni kwamba fedha alizokopa kwa mdhamana wa *BoT* Watanzania wote sasa tunazilipa fedha hizo kwa manufaa binafsi. Mheshimiwa Mzindakaya pia katika taarifa yake hiyo anakiri.........!

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Slaa, nadhani hapo ulipofikia ilitosha kuonyesha chini ya Kanuni ya 49(7), kwamba kuna uwezekano wa *conflict of interest,* imekwisha, sasa kuendelea kumtaja Mzindakaya itafikia mahali kwamba pengine na wewe sasa una *over react* na humtendei haki, rudi tena kwenye hoja tafadhali!

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI – MHE. DK. WILBROD SLAA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja zilizoko na taarifa zilizotolewa na magazeti yote, kwa mfano ya tarehe 24 Juni, 2007, ukizingatia Nipashe, Mtanzania, Mwananchi ambapo Mheshimiwa Rais wetu anapiga kelele kuhusu ubadhirifu, matumizi mabaya ya fedha za umma, matumizi mabaya ya ofisi kwa maslahi binafsi, Kambi ya Upinzani kama tulivyokwisha kumwahidi Rais, tuko nyuma yake na tunamwunga mkono katika vita hii. *(Makofi)*

Tunawaomba Waheshimiwa wabunge wote wakiwemo wa CCM, wote wenye nia njema, tuweke itikadi zetu pembeni, tumwunge mkono Mheshimiwa Rais wetu katika hili.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 27(2 ) inatutaka, na kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu : "..watu wote wanatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu, na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao…" mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama watu wote wanatakiwa hivyo, kwa namna ya pekee sisi tulioapa kuilinda na kuitetea Katiba si ndiyo wajibu wetu wa kwanza! Chonde chonde waheshimiwa wabunge katika hili, kwa kuanzia na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe na wewe Mheshimiwa Spika na wabunge wote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu katika hili tupige vita ubadhirifu kama upo. (*Makofi*)

Kwa kuwa hatujauhakikisha ubadhirifu huu, hoja zetu zinaendelea, nchi inateketea kama tunavyoona kama ilivyo kwenye vyombo vya habari, kwani sisi sote tumechaguliwa na wananchi lakini....!

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Slaa, ukiendelea hivyo mwisho nitakuzuia kabisa kuendelea, hebu ondoa hili neno la kusema "nchi inateketea" *it is very strong.*

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI – MHE. DK. WILBROD SLAA:** Mheshimiwa Spika, naifuta.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kustushwa na taarifa za kiwango cha ubadhirifu na hujuma hizo, mathalani malipo ya mashaka makubwa ya Tshs. 40 Billioni kama ilivyoripotiwa na Gazeti la *Daily News*, (*Daily News, Issue No*. 0856-3812 na 9315 la 22 Juni, 2007, *p*.1), tena Gazeti la Serikali, na taarifa hiyo haijakanushwa hadi sasa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini mwa mtu yeyote kuwa Kampuni ya "Kagoda *Agricultural Ltd*" iliyosajiliwa tarehe 29 Septemba, 2005 na ndani ya wiki zisizozidi nane tayari ilikuwa imekwishapewa fedha zaidi ya sh. 30.8 bilioni kupitia *External Service Debt Account,* Benki Kuu, ambayo Gavana ndiye msimamizi mkuu. Taarifa hiyo bado inaonyesha kuwa mikataba 9 ilisainiwa tarehe 18 na 19 Oktoba na makampuni 12 ya nje chini ya mkataba na Kampuni ya Kagoda *Agricultural Ltd.* Pamoja na kasoro zilizojitokeza kwa mujibu wa Taarifa ya Wakaguzi ni kuwa nyaraka zilizotumika hazionyeshi makampuni yao (*letter head*). Majina yaliyotumiwa na wakopaji hao yanatia mashaka, walioweka saini kwa niaba ya Serikali za Ujerumani, Italia, Uingereza, Japani, Yugoslavia, Ufaransa na Marekani hayakuweza kutambulika kabisa wakati Mkaguzi alipowasiliana na Makampuni husika. Gazeti la "Kulikoni" lililotoka leo, Toleo Na 67 la Jumatatu 21-1 Julai, 2007, ukurasa wa 1, limebeba kwa undani zaidi habari hizo. Hali inatisha zaidi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutona na hilo basi naomba nisiendelee nalo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wameshapata ni nini, ila taarifa niliyotoa Bungeni kuhusu tuhuma inayomhusu Gavana wa Benki, inamhusisha Gavana moja kwa moja na kwa uzembe katika upotevu au matumizi mabaya ya fedha za Serikali ndani ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizo haziishii hapo, na naomba ninakiri, taarifa hizo zinamtaja mkewe Anna Muganda kuwa mmoja wa Wakurugenzi wa Kampuni ya *Time Mining*, ambayo ndiyo iliyokuwa inaendesha kampuni ya madini ya Meremeta, na hatimaye imeuzwa kwa bei ya kutupa, na baadaye *BoT* kulipa dhamana iliyowekwa na Benki Kuu, kabla ya kuuzwa kwa *Rand Gold*, ambako Anna Muganda mke wa Gavana pia ni mwenye hisa.

Watanzania tunajiuliza hapa kuna nini? Serikali kila ikihojiwa Bungeni haitoi majibu kama alivyojibu waziri wa Fedha Bungeni juzi. Wakurugenzi wa Alex Stewart nao walitoka *Time Minning* ambako Ana Muganda anahusika. Haya yote yametokea kwa bahati mbaya? Vivyo hivyo kwenye *External Debt Service Account*, au kwenye *Bank M*, ambayo inasemekana imeandikishwa bila kufuata utaratibu na inamilikiwa na wamiliki walioonyeshwa kwenye waraka niliowasilisha wiki iliyopita. Mmoja wa wamiliki hao anasemekana kuwa Gavana Balali kupitia Kampuni yake na mkewe, Anna Muganda, inayoitwa "*Napster Group*" iliyosajiliwa Uswizi. *(Makofi)*

(i) Mheshimiwa Spika, kwa hili tunaomba watanzania wote watuunge mkono, ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa wabunge ambao dhamira zao ni safi, wana uzalendo wa kweli, tuungane ili kuokoa siyo tu jina la nchi yetu lakini pia rasilimali zake nyingi zinazoteketezwa bila huruma.

(ii) Kutokana na haya yote, ninawomba watanzania wote pamoja na wabunge wa CCM ndugu zangu, tuungane kwa pamoja, hatuna sababu ya kugombania fito wakati nyumba tunayojenga ni moja. Tukubaliane kuchukua hatua ya pamoja. Narudia tena rai yangu kuwa suala hili si la kuangalia kwa jicho la kiitikadi, bali uzalendo tu utawale mioyoni mwetu. Hivyo basi: (*Makofi*)

(a) Tunamwomba kwa heshima kubwa Mhe. Gavana Daudi Balali ajiuzulu kwa hiari yake ili uchunguzi wa kina uweze kufanyika na kubaini ukweli wa taarifa hizi zilizozagaa kila mahali, zenye athari si tu kwa jina lake lakini pia kwa jina na heshima ya nchi nzima, ikiwa ni pamoja na kuharibu jina la Bunge hili iwapo litashindwa kusimamia jambo hili zito.

(b) Iwapo Gavana Balali atashindwa kujiuzulu, basi tunaiomba Serikali imsimamishe mara mmoja ili uchunguzi wa kina uweze kufanyika. Suala hili linachukuliwa kama jambo dogo, lakini athari yake ni kubwa. Si vema, uchunguzi ufanyike wakati mhusika yuko Ofisini, na kwa vyovyote vile uchunguzi utakaochukua mwaka mzima, ni njia ya wazi ya kutengeneza mazingira ya kuvuruga uchunguzi. Wabunge tunaomba kabisa kwa hili tuungane, na tuweke dhamana ya utaifa na uzalendo mbele kabla ya maslahi ya vyama vyetu.

(c) Mheshimiwa Spika, hapa ninasukumwa zaidi na msemo wa Kiswahili kuwa ‘Machozi ya wanyonge huwa hayaanguki ardhini bali huanguka mionyoni mwao na kwa hivyo Mungu kutoka mioyo hiyo husikia kilio chao.’ Tunaomba hayo machozi yao yatusukume sisi katika kuona haki inatendeka. (*Makofi*)

(d) Kambi ya Upinzani inaomba sana kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge, Kifungu cha 104, Bunge hili liunde Kamati Teule ya Bunge kutimiza jukumu lake la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba. Serikali ikitaka inaweza kuendelea na utaratibu wake wa ukaguzi. Kwa utaratibu huo tutakuwa tumelinda heshima ya Bunge letu ambalo sasa watu wengi wanazidi kuona kuwa linalinda maslahi ya ChamaTawala, na au linageuzwa kuwa *‘Rubber Stamp’*.

(e) Mheshimiwa Spika kama niliivyosema, suala hili lisiangaliwe kwa jicho la vyama bali liwe suala la uzalendo na utaifa zaidi, na Kamati Teule ni muhimu ikizingatiwa kuwa *External Auditors* aliozungumzia Waziri wanachunguza tu upotevu/matumizi mabaya kwenye *External Debt Service Account* tu, na tuhumu zilizoko zinaenda mbali zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, maswala haya ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu, na hivyo tunapenda kupata majibu ya kina na siyo majibu ya kisiasa na kishabiki ambayo hayana manufaa wala kwa Taifa letu wala kwetu binafsi isipokuwa kama tuna maslahi yaliyojificha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hali ya Kisiasa Nchini, kwa ujumla hali ya ulinzi na Usalama, na ya siasa nchini ni shwari kama inavyoelezwa na Serikali. Kambi ya

Upinzani inapenda kulipongeza kwa kuungana na Waziri Mkuu, Jeshi letu la Polisi, kwa namna ya pekee kwa jinsi lilivyoweza kudhibiti ujambazi, hasa ujambazi wa silaha za moto. Kambi ya Upinzani inatoa mwito kwa Watanzania wote kushirikiana na Jeshi la Polisi katika masuala yote yanayohusu usalama wetu na wa mali zetu, kwani bila ushirikiano wa raia wema Jeshi la Polisi halitaweza kudhibiti uhalifu kila mahali na kila wakati kutokana na idadi yao na uduni wa nyenzo.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo makuu kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 ni pamoja na "Kuwezesha na kudumisha hali ya Utawala Bora katika ofisi ya Waziri Mkuu," na Waziri Mkuu ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za Serikali na mratibu wa Wizara, Idara na vyombo vyote vya Serikali za Mitaa. Kambi ya Upinzani inadhani Ofisi ya Waziri Mkuu ina nafasi kubwa sana katika kusimamia, kuimarisha, kukemea na hata kurekebisha pale ambapo kuna dosari katika masuala yote ya Utawala Bora na Haki za binadamu katika nchi yetu. Utawala Bora na Haki za Binadamu zisipoheshimiwa na kusimamiwa kikamilifu, yote tunayofanya yanapoteza maana kwani maendeleo yote ni kwa ajili ya Binadamu. (*Makofi*)

(i) Masuala haya ni kama yanavyoonekana kwenye Hotuba yetu kama nilivyowasilishwa mezani ikiwa ni pamoja na mauaji yanayotokana na imani ya kishirikina ambayo yameripotiwa katika mikoa mingi.

(ii) Mheshimiwa Spika, tuko karne ya Sayansi na Teknolojia, lakini bado tunaendekeza ushirikina. Wahanga wakubwa wa uhalifu huu ni akina mama (wazee) na watoto. Kambi ya Upinzani inadhani Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, inahitaji kuongeza jitihada zaidi katika kusimamia sheria ya *The Witchcraft Act, Cap.* 18 (R.E.). Sheria hii ikisimamiwa vizuri na vyombo vyote husika, tunaweza kuokoa maisha ya watu wetu wengi. Takwimu zinaonyesha mwaka jana peke yake wameuwawa zaidi ya watu 40. (*Makofi*)

(iii) Taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwa kuna unyanyasaji unaotokana na maamuzi mabovu kama vile utekelezaji usio na mpango wa kuwaondoa Wamachinga na Mama na Baba lishe ambao umewasababishia upotevu wa mali, na kuwarudisha katika lindi kubwa la mali. Wakati naandika sikujua na limeonyeshwa kwenye Televisheni wale waliohamishwa, ieleweke hapa hakuna anayepinga kuwahamisha kwa maana ya kufanya miji yetu kuwa safi, tunachosisitiza ni utaratibu bora unaojali ubinadamu katika kuwahamisha watu hawa. (*Makofi*)

(iv) Unyanyasaji wa Wafugaji kama ulivyotokana na Agizo la Serikali la Machi 2006 la kuwaondoa wananchi kutoka bonde la Usangu/Ihefu na hapa pia suala sio hakuna anayekataa uhamishaji lakini madhara yaliyotokana na uhamishaji huo ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi wananchi wamepoteza mali, vitendo vya rushwa vilionekana, kusambaratika kwa familia, kuwanyima elimu watoto waliokuwa shule, kuwanyima huduma za kimsingi na muhimu kwa binadamu, kusababisha kwa ghafla

kuporomoka kwa uchumi na kuna taarifa za Asasi binafsi zisizo za Serikali zilizoenda kufanya utafiti na taarifa hizi ziko wazi, sasa tungependa basi Serikali ifanye hivyo.

(a) Kwa vile Tume ya Serikali imefanya uchunguzi wa kina Taarifa ya Tume hiyo itolewe hadharani. Hili ni jambo linalogusa Watanzania wengi tungependa lijulikane hadharani.

(b) Serikali ikubali kufanya haraka tathmini ya mali na iwalipe fidia wote walioathirika. Kuna watu wanasemekana wamepoteza kuanzia ng'ombe laki, mia nne wakabaki ng'ombe 40, hii ni hali ya hatari kwa maisha ya watu hawa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe mjadala wa wazi wa kitaifa juu ya mstakabali wa makabila ya wafugaji, na hili tunalisema makusudi kwa sababu wananchi kama Wabarbaig waliondolewa kwenye kitu kinachojulikana kama *Wit Complex* yenye zaidi ya eka laki moja. Lakini leo wamekuwa kama wakimbizi ndani ya nchi yao wanakwenda huko na huko. Kwa hiyo, tungependa mjadala huu uweze kuona mstakabali wa makabila haya ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, liko pia suala la Adhabu ya Kifo (*Death Penalty*), bado halijafanyiwa kazi ya kutosha na Serikali yetu. Hotuba yangu inaonyesha kwa kirefu sababu za kuondoa adhabu hii, ikiwa ni pamoja na mateso ya kisaikolojia anayopata mhusika kwa kusubiri bila kujua siku ya kunyongwa, uwezekano wa kumhukumu asiyehusika na ukiisha kumnyonga haiwezekani tena kumrudishia uhai wala fidia, na abu zinazotolewa za adhabu hii hazionyeshi kuwa na mafanikio yanayotegemewa kwa maana ya kuwazuwia wengine waone ubaya wa kosa hilo na kutolifanya (*detterent effect)*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamsihi Mheshimiwa Waziri Mkuu, aingilie suala hili yeye mwenyewe, na kusukuma taratibu zinazohusika za kuzifanyia marekebisho sheria zetu ili adhabu hii ifutike katika vitabu vyetu vya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani hairidhiki na kasi ya mazungumzo yanayoendelea kati ya CUF na CCM. Kambi ya Upinzani isingelipenda, baada ya matukio ya mwaka 2001, kuchezea shilingi chooni. Mshikamano, umoja na amani katika visiwa vya Zanzibar na Pemba pia ni amani kwa nchi nzima. Hivyo, tunaitaka Serikali ivisukume vyama vya CCM na CUF kufikia haraka mwisho wa mazungumzo haya kabla wananchi hawajakata tamaa na kujichukulia sheria mikononi mwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Uchaguzi, mwezi Desemba, 2007 tutakuwa tumekamilisha miaka miwili kamili tangu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Taarifa mbalimbali sasa zimetoka, mathalani Taarifa ya Tume ya Uchaguzi (*NEC*), Taarifa ya *TEMCO*, Taarifa ya Wakaguzi wa Nje wakiwemo Bunge la *SADC*. Katika taarifa hizi mambo mbalimbali yamejitokeza. na ninapenda kuyagusia kwa kifupi tu. Mambo haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, suala la Mgombea Binafsi limejitokeza sana hadi Mahakama Kuu kulitolea maamuzi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulifanyia kazi mapema pamoja na Mabadiliko Makubwa ya Katiba yanayodaiwa na wadau wengi.

(ii) Daftari la Kudumu, Mheshimiwa Waziri Mkuu amelizungumzia vizuri na hapa ningependa kuwapongeza, lakini tunasisitiza kwamba utaratibu unaotakiwa ni ule unaomwezesha mtu anayefikia miaka kumi na nane pale pale kuweza kuandikishwa. Utaratibu huku duniani na siku hizi tuna teknolojia huhitaji tena kuwa na taratibu za gari kwa sababu kazi hizi zinafanyika haraka. Vianzio vya fedha Waziri Mkuu ananionyesha fedha ziko wapi vianzio tumeonyesha katika bajeti yetu na tunaomba ulete *supplementary budget*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la Watanzania walioko nje ya nchi na wangependa kutumia haki yao na Mheshimiwa Rais wetu mwaka jana alipokwenda Namibia aliwaahidi hivyo, kwa hiyo, tunaamini kwamba suala hili pia litafanyiwa kazi. *(Makofi)*

(iii) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imefurahishwa na Uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu suala la Takrima. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itekeleze hukumu ya Mahakama kuu, kujenga mazingira ya Demokrasia. (*Makofi*)

(iv) Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Nchi za Kiafrika, (*AU*) wamekwishapitisha azimio la wanawake kuwa asilimia 50 katika nafasi za maamuzi na uongozi. Kambi ya Upinzani haina tatizo kabisa na azimio hilo ikizingatiwa wanawake ni asilimia 51 ya Watanzania wote. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa tahadhari na inamtaka Waziri Mkuu, ambaye Ofisi yake ndiyo yenye dhamana ya masuala ya Uchaguzi, na mratibu wa Vyama vyote, aitishe vikao mapema iwezekanavyo na vyama vyote vya Siasa, akishirikisha pia wadau mbalimbali wakiwemo Vyama vya hiari na madhehebu ya dini kwa lengo la kuwa na mjadala wa kitaifa kuhusu suala hili zito. Utulivu na amani katika nchi vinapatikana kwa kuwa na siasa "Shirikishi". *(Makofi)*

Baadhi ya changamoto zilizoripotiwa na taarifa mbalimbali tulizotaja hapo juu, ikiwemo Taarifa ya *NEC,* ni pamoja na kutumika visivyo kwa Jeshi la polisi na polisi kutumia nguvu za ziada pasipo lazima. Kambi ya Upinzani inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu kufanyia uchunguzi wa kina kwa kuwashirikisha na watu walio huru, mathalani Majaji wa Mahakama Kuu kujua sababu za msingi za vurugu hizo kwa lengo la kupata mapendekezo na kuondokana na matatizo hayo katika chaguzi zijazo.Ni imani yetu Serikali haitasubiri Uchaguzi mwingine ili kuzifanyia kazi dosari hizi.

Mheshimiwa Spika, suala la Makao Makuu kuhamia Dodoma, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2006/2007 zilitengwa *T.Shs*. 427,945,000. Lakini kwa bahati mbaya kazi zilizofanyika ni usafishaji wa mifereji ya maji taka, ujenzi wa uwanja wa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (*Nyerere Square*), ununuzi na ujenzi wa mabanda mawili katika uwanja wa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya mji wa Dodoma. Katika Mwaka wa Fedha 2007/2008 Ofisi ya Waziri Mkuu wamepewa jumla ya Sh. 1,633,999,000 kwa ajili ya *CDA*. *CDA*

wamepewa jumla ya Sh. 1,704,5754,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi, yaani zaidi ya fedha walizopewa kwa shughuli za kustawisha Makao Makuu. Kazi wanazotarajia kufanya ni zile zile za kumalizia ukarabati wa Nyerere *Square*, kusafisha mifereji ya maji, kuotesha miti, kukarabati barabara za Manispaa ya Dodoma na kupima viwanja.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa kuhamisha Makao Makuu ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, na hatuna sababu ya kuhoji mambo ya Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, Sera hiyo iliyopitishwa zaidi ya miaka 30 iliyopita, haijatekelezwa au imetekelezwa kwa kiwango kidogo sana tangu ilipotangazwa 1973 kwa Tangazo la Rais, Na.230. Kwa takwimu hizi hakuna mkakati wowote wa muda mfupi wala wa muda mrefu wa kutekeleza sera hiyo kikamilifu. Wakati huo huo, Taifa linaathirika sana na sera hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2001 tuliambiwa ndani ya Bunge hili kuwa Wizara 5 zimehamia Dodoma kwa mujibu wa Taarifa ya *Hansard*. Tunataka Waziri Mkuu alithibitishie sasa Bunge hili toka uamuzi huo wa kuhamia Dodoma ufanyike ni Wizara ngapi zimehamia kikamilifu Dodoma? Kambi ya Upinzani inataka Serikali ilieleze Bunge hili ni kwa nini shilingi bilioni zaidi ya 3 zinatengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi ya Waziri Mkuu Dar-es-Salaam, badala ya Ofisi hiyo kujengwa Dodoma ambayo ni uthibitisho wa dhamira ya kuhamia Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu aliondolee wasiwasi Bunge hili kuwepo au kutokuwepo matumizi mabovu ya walipa kodi kutokana na viongozi wa Serikali, wa kisiasa na watendaji, kuwa na nyumba mbili moja Dodoma na moja Dar-es-Salaam, zote zikigharimiwa na Serikali kinyume na Kanuni za fedha za Serikali. Kambi ya Upinzani inataka pia kuelezwa kwa kina iwapo taarifa hizo ni za kweli, Serikali inalielezaje Taifa hili kwa nini walipa kodi waendelee kugharimia Sera ya Chama cha Siasa ambayo haitekelezwi inavyotakiwa na wala hakuna mkakati na bado wanaigharimia kwa gharama kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ieleweke wazi kuwa Kambi ya Upinzani haina tatizo kabisa na kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma. Kambi ya Upinzani inakerwa na Sera ambayo miaka nenda rudi haitekelezwi lakini fedha zinatumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali za Mitaa ni vyombo muhimu sana katika uongozi wa nchi kwa vile vyombo hivi viko karibu na watu na ndiyo ngazi inayokutana na wananchi kuliko ngazi nyingine zote. Katika hotuba yangu ya mwaka jana nilizungumzia mambo mengi na namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mengine yamekwisha kutelekezwa. Naomba nirudie tena machache mwaka huu kwa lengo la kutoa mchango wa Kambi ya Upinzani katika kujenga Serikali imara za Mitaa na hivyo kujenga demokrasia ya kweli nchini mwetu, mambo haya ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema, Wenyeviti wa vitongoji, wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Madiwani na viongozi ambao mchana kutwa na usiku kucha

wako kazini kusimamia programu zote zinazobuniwa na Serikali, mathalani, Programu za kupiga vita Umaskini, MKUKUTA au MKURABITA. Kama alivyosema Waziri Mkuu na Wenyeviti hawa ndio wanaosimamia pia programu ya MMEM, TASAF na kadhalika, bado wanatakiwa kubuni mipango na miradi inayohusiana na maeneo yao. Hawa ndio walinzi wa amani na usalama katika maeneo yao. Ni dhahiri basi, hawa ni viongozi muhimu sana katika nchi yetu.

(b) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubuni 'mpango maalumu' wa kuwawezesha viongozi hawa kujengewa uwezo ili waweze kusimamia vizuri zaidi rasilimali nyingi zilizopelekwa chini na Serikali kuu kupitia Programu hizi. Hata semina zinazofanyika nyingi haziwafikii, tunaomba semina hizo sasa ziteremke chini kwenye ngazi yao lakini pia wajengewe utaratibu wa malipo angalau ya posho ya uhakika zaidi. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, Vijiji vipo chini ya 13,000, kata ziko kama 2,500. Tukiwa na mpango mkakati hawa tunaweza tukawalipa na ni injini ya maendeleo katika vijiji vyetu na katika kata na tukaweza kupiga vita umaskini kwa utaratibu ulio wa uhakika zaidi. (*Makofi*)

(d) Watendaji wa Kata ambao ni waratibu wakubwa wa maendeleo, wanaosimamia 'Amani' katika maeneo yao, wanamsaidia Mkurugenzi wa Wilaya (*DED)* katika utekelezaji wa majukumu yake. Hawa, wanahitaji vyombo vya uhakika vya usafiri mathalani pikipiki. Ni vema Serikali ikabuni mpango wa kudumu (*sustainable programme*) wa kuwasaidia Watendaji hawa kupata vifaa hivi, hata kama ni kwa kuwakopesha kama tunavyofanyiwa sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Makatibu Tarafa wana pikipiki lakini kwa kweli kazi nzito zaidi anafanya Katibu Kata kuliko Katibu Tarafa. Sina tatizo na Katibu Tarafa kupewa pikipiki lakini tungempa yule ambaye ni msingi mkubwa kwa maendeleo yetu.

(e) Serikali itazame upya Sheria Na. 7 na 8 ya Mwaka 1982 na kuweka wazi zaidi majukumu ya Wakuu wa Wilaya, kama kufuta nafasi hizo zimeshindikana, ili kuleta tija zaidi kati ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya (*DED)* ambaye ndiye mwenye wataalamu na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambaye kimsingi ana viongozi wakuu wasiozidi watatu katika ofisi yake. Sheria zinazoongoza Serikali za Mitaa pamoja na Sheria ya *Regional Administration* inayounda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa nayo iangaliwe upya.

(f) Mheshimiwa Spika, mpango huo wa maboresho sasa uko karibu mwaka wa 8. Matunda ya Maboresho bado hayajaonekana kikamilifu na fedha nyingi sana za wafadhili na za ndani zimetumika katika Semina za Warsha na Warsha za Maboresho**.**

(g) Kambi ya Upinzani pia inapenda kupata tathmini ya kina ya Mpango wa Maboresho, ukionyesha malengo yake na mafanikio na matatizo tuliyokutana nayo, na mpango mzima umegharimu fedha kiasi gani za ndani na ngapi za nje.

(h) Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya wadau kwa siku nyingi ni kuwa ili uchaguzi uonekane na utendeke kwa haki na huru, ni vyema kurudisha uchaguzi huu chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa sababu ni vigumu chini ya *system* ya sasa ya uchaguzi huu kuwa huru na haki. (*Makofi*)

(i) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu kwa kina kauli ya Serikali juu ya mapendekezo haya yote yanayohusu Serikali za Mitaa katika ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya jumla: Kambi ya Upinzani inataka kutoa rai kuwa ili tufanikiwe katika mipango ya maendeleo yetu, ni lazima tuondokane na dhana ya itikadi katika masuala yanayogusa maslahi na ustawi wa Taifa. Maendeleo hayajui itikadi.

Mheshimiwa Spika, barabara ni barabara tu, haijali chama na watu wa vyama vyote wanapita. Maji hayana sura, na wananchi hawatajali chama gani kimeleta maji bali wataangalia nani kawaongoza kupata maji. Hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ndiyo Mratibu wa Vyama vya Siasa, ni vyema ikaandaa utaratibu wa kujenga imani kwa Watanzania kufanya kazi pamoja bila ya kuangalia itikadi za kisiasa. Utamaduni wa amani na mshikamano hujengwa, hauji tu kwa miujiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kuwa Waziri Mkuu atakuwa kiungo kati ya Serikali na Vyama kama malengo ya Ofisi yake yanavyoeleza, na atapanga mapema iwezekanavyo kukutana na vyama vya siasa ili kubadilishana mawazo na viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa. Mheshimiwa Rais tayari amefanya hili, tungeomba mratibu wetu naye afanye utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa ya TAKUKURU (*PCCB*) kuhusu *Richmond Co.Ltd/Dowans* inayohusu mradi wa dharura wa umeme, Kambi ya Upinzani inapenda Taarifa hiyo itolewe hadharani, na kwa Waheshimiwa wabunge kuitafakari, na kuijadili. Taarifa hiyo ina upungufu mkubwa, na inaleta dhana kuwa pamoja na sheria mpya TAKUKURU haina meno. Ni imani yetu kuwa ofisi yako itakubali ombi hili na kuwasilisha Taarifa hiyo mapema ili Watanzania wote wajue kilichotokea.Kambi ya Upinzani inapenda kupata Taarifa na majibu ya kina kuhusu hoja hizi. Mwenyezi Muungu atupe busara zake kama tunavyoomba kwenye Dua kila siku asubuhi. Naomba nikushukuru tena kwa mara nyingi kwa kunipa fursa hii, na pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza na hasa kwa kuwaomba watusaidie katika hoja ambazo zinalinda na kutetea maslahi na rasilimali za taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, kabla hatujaendelea na wachangiaji wengine kuna mambo kadhaa ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa ameyasema ambayo baadhi ya wahusika walioguswa wameniandikia kutaka kupata nafasi ya kuweza kujibu sehemu ambazo zinaonyesha ni upotoshaji. Kwa hiyo, baada ya kusoma moja ambalo nimelipata sasa hivi kutoka kwa Mheshimiwa Mzindakaya, nitatoa nafasi chini ya Kanuni ya 40 kumpa nafasi

Mheshimiwa Mzindakaya chini *adjournment motion* leo saa mbili kasorobo. Lakini kuna mengine ambayo yanahusu Serikali nayo nitayatafutia utaratibu ili yaweze kusahihishwa.

Baada ya hapo sasa Waheshimiwa tunao wachangiaji 91 ukiacha 10 waliokwisha changia mara moja ambao nimewaacha kabisa wasitegemee. Mheshimiwa Kawawa, Mheshimiwa Msafiri, Mheshimiwa Mshashu, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Mheshimiwa Dr. Chegeni, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Mwakyembe, Mheshimia Anastazia Wambura, na Mheshimiwa Juma Njwayo, sitawapeni nafasi kwa sababu ninao 91 kabla ya nyinyi. Sasa kwa leo tutaanza na Mheshimiwa Mudhihir atafuatiwa na Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, na Mheshimiwa Phillemon Ndessamburo, nitawatamka wengine kadri tunavyoendelea.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo baada ya wasemaji wakuu, na naomba uniruhusu nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mimi sina chembe ya tatizo na hotuba yake, wala sina chembe ya wasiwasi na utendaji wake. Nimesimama hapa kutaka kuzungumzia ubabe na ukiukwaji wa Katiba kwa baadhi ya watendaji wetu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi wa Wilaya ya Lindi, baada ya kuona wilaya haina hospitali mwaka 2003, Baraza la Madiwani tulikaa na tukaazimia kujenga hospitali ya wilaya eneo la Kitomanga. Serikali inaongozwa na CCM kwa kuwa ni sikivu ikatutengea pesa shilingi milioni 300 za kuanzia kwa maana ya Mwaka wa Fedha 2004/2005 tulipata shilingi milioni 100 na 2005/2006 milioni 100. Uamuzi huo hatukuuchukua kwa sababu tu ya kwamba sisi ni madiwani, tulizingatia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ibara ya 146, na naomba kunukuu: “Madhumuni ya kuwepo Serikali Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi na vyombo vya Serikali ya Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kwa ujumla”. Serikali ilipokubali mpango wetu, ilikubali kwa kuzingatia vilevile ibara ya 8 ya Katiba ambayo nainukuu pia: “ Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo: (a) Wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote, na Serikai itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.”

Kwa mshangao mkubwa, Ofisi ya *RAS* Mkoani Lindi imeamua kuuzima mradi huu ambao umeshaanza kwa vipindi viwili vya mwaka wa fedha na unapouliza, unapata maneno ambayo hayavutii kuzungumzwa na mtu mzima na anayeambiwa kuwa mtu mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina kipindi cha tatu humu Bungeni, sijawahi kupiga kelele kwa viongozi wowote, lakini ukiona mwanaume anapiga kelele ujue ameshikwa pabaya. Sisi tunajiuliza, sisi Viongozi, Madiwani, hivi jeuri hii ya kukiuka Katiba, jeuri hii ya kupuuza maamuzi ya viongozi waliochaguliwa na wananchi inatoka wapi? Sisi badala ya kuheshimiana na ofisi hii, tunaogopana. Tukifikia kuogopana, haya aliyotuagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu leo katika hotuba yake, ibara ya 50 kwamba, napenda kusisitiza umuhimu wa Viongozi wa Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Kata na

Vijiji kushirikiana na wananchi ili kufanikisha mpango huo. Yatawezekana? *(Kicheko/Makofi)*

Unapoambiwa hapa Kitomanga ni kama uso na hiyo hospitali ni sikio, huyu mtumishi anamwambia Diwani kwamba maamuzi ya Halmashauri hapa mlipochagua ni kama sikio katika uso maana yake masikio ni sisi, hatuenei katika mtazamo wake kwetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, ni kweli sisi mtaalamu huyu tunamWogopa badala ya kumheshimu na katika mazingira hayo tuna hofu kwamba huenda tukashindwa kufanya naye kazi. Kwa hiyo, hatua ya mwanzo, mimi ningependa kupendekeza hapa kwamba kitabu hiki cha maendeleo, yaani Kitabu cha Nne kwenye *Vote 76, 6338 Sub- vote* kuna *construction of regional block* milioni 155. Lakini chini 6340 kuna *rehabilitation of regional block* shilingi milioni 484. Hii hela hapa juu shilingi milioni 155 ndiyo ile ambayo imetengwa kwenda kujenga Hospitali ya Wilaya. Hapa ana–*rehabilitate* na hapa ana–*construct* jengo hilohilo. Moja, ningeomba, kwa niaba ya wananchi ya Wilaya ya Lindi lenye Majimbo matatu, yaani Jimbo la Lindi Mjini, Mchinga na Mtama pesa hizi zipelekwe kulekule kwenye hospitali ya Wilaya kulikoamuliwa. *(Makofi)*

Wakati Serikali ya awamu ya nne inasema tutajenga zahanati kila kijiji, tutajenga kituo cha afya kila Kata, mtaalamu mmoja tu kwa kupinga Katiba anasema hapo ni sikioni. Sisi tuliamua kujenga pale kwa sababu kubwa moja. Barabara ya Kibiti – Lindi ikishaanzia Mbagala mpaka Lindi Mjini hakuna hospitali hapo njiani kilomita karibu 460. Tunaona matokeo ya Hospitali ya Tumbi Kibaha. Tunaona matokeo ya Hospitali ya Morogoro zinavyookoa majeruhi ya watu leo tunajenga hospitali anasema hapa ni sikioni.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine kwa umri wangu siwezi kuyasema hapa, lakini yapo maneno ambayo kwa kweli yanatufikisha mahali tunashindwa kufanya kazi na mtaalamu huyu kwa kufikiria tu kwamba sisi ni sikio katika uso. Hilo la kwanza.

La pili, umeme wa *Mnazi Bay*. Leo asubuhi Naibu Waziri wa Nishati na Madini alikuwa anajibu hapa kwamba wanahangaika kutafuta gesi maeneo mengine. Hakuna haja ya kuhangaika, tayari gesi iliyopo *Mnazi Bay* inatosha kusambaza umeme Mtwara yenyewe, Tandahimba, Newala, Masasi, Nachingwea, Liwale, Ruangwa, Mji wa Lindi na Mchinga ambako mwaka jana tuliahidiwa humu ndani kwamba utafika umeme na kulitengwa shilingi milioni 320.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini haina matatizo na mradi huu na Mashirika yake ya *TANESCO* na *TPDC,* wamekubaliana tayari na Kampuni ya *ARTUMAS* ambayo imewekeza mpaka hivi sasa jumla ya dola milioni 170.

Lakini Afisa mmoja tu naye ni mbabe sana yupo pale Wizara ya Fedha ameiyumbisha Serikali kutia mkataba na *ARTUMAS* mpaka hivi leo, ndiyo juzi imeandikwa barua na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu nilipoomba *appointment* naye kwake akanikubalia na tukamwita yule afisa nikamwomba Waziri wa Fedha kwamba mwambie huyu bwana abadilike. Sisi Lindi ni watu kama kule

kwao. Ndiyo kwa upondo barua imetiwa saini. Baada ya hapo hatujui kutachukua miezi mingapi tena umeme ule kufanya kazi. *(Kicheko)*

Rais amekwenda pale akasema, nataka umeme tarehe 25 Desemba, 2006 uwe tayari. Kaenda Waziri Mkuu kazungumza hilo hilo, halafu afisa mmoja tu pale Wizara ya Fedha anatembea utafikiri anataka kupaa, mabega yako hivi yeye peke yake anatuyumbisha Watanzania wote! Ubabe wa namna hii unatupunguzia kasi yetu ya Serikali ya awamu ya nne. *(Makofi)*

Sasa mimi ningependa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa njia hii ya kuwasimamia watendaji katika mambo tuliyoamua, nafikiri ndiyo njia nzuri ya kuunga mkono kuliko ile iliyoshauri Kambi ya Upinzani hivi punde. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni maji. *World Bank* toka mwaka juzi inachimba kutafuta maji. Mimi naomba nikiri kuwa vijiji vya Chikonji, Likwaya, Kiwawa, Namkongo na Kilolambwani, sina majibu tena ya kutoa juu ya mradi wa *World Bank.*

Mheshimiwa Spika, siku ile ulituonya hapa kwamba kila anayemtaka kiongozi kwenda huko anamtaka Naibu Waziri wa Maji tu, lakini mimi sio lazima yeye, nikimpata Waziri mwenyewe na Katibu Mkuu nikaenda naye huko Chikonji na hata Likwaya akasikilize maneno ya wananchi wenyewe anisaidie kujibu, mimi nimemaliza ufundi wa kujibu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama utamruhusu Naibu Waziri kuja, basi bado nitafurahi twende pamoja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la nne ni hospitali ya rufaa. Mwaka jana nilizungumza kwa uchungu sana humu ndani kwamba tugawe maendeleo *evenly* sisi Lindi na Mtwara ni wamoja na Ruvuma tugawanegawane angalau tufanane. Sisi wengine ni watu wa kufuata tu. Waziri Mkuu akasimama hapa akasema ataliingilia suala hili kati.

Mheshimiwa Spika, najua kuna hatua alizichukua, lakini aliowaagiza mpaka leo hawajafanya jambo, watu wa Lindi, Mtwara na Ruvuma tuna haki ya kujua hatimaye maamuzi yaliyofikiwa ni yapi. Ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu utatusidia kulitatua hilo.

Mheshimiwa Spika, tulithibitishiwa hapa kwamba *EWURA* watahakikisha wafanyabiashara hawa hawaleti kiburi. Lakini jana Lindi kuna Sheli moja pale inaitwa *BP,* yaani kituo cha mafuta, jana mafuta ya petroli yalikuwa yanauzwa Sh. 1,650/= kutoka Sh. 1,300/= jana Jumapili Lindi Mjini, Jumamosi ilikuwa ni Sh. 1,350/= jana Sh. 1,650/= bado tarehe moja Julai haijafika, sasa ikifika tarehe 1 Julai sijui mambo yatakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa bajeti ni nzuri, lakini kilio cha Wabunge wa CCM tunataka usimamiwaji uwe barabara ili watu wasije wakaichukia bajeti yetu ambayo nia yake ni njema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, mimi sitaki kuwa Msemaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini kwa hili moja la Kaka yangu Msemaji Mkuu wa Upinzani linatugusa sote. Hili la jina.

Mheshimiwa Spika, ninachofahamu, jina ni utambuzi tu. Wanadamu hawatofautishwi mambo yao kwa majina yao, majina ni kwa ajili ya utambuzi tu basi. Wewe Juma na wewe Abdallah mnafahamiana na hivyo. Tabia ndiyo kinachomtofautisha binadamu mmoja na mwingine! Sasa mnasema tuiite Kambi ya Ushindani, sisi tumeshashindana wakati wa Kampeni za Uchaguzi, tumeshindanisha sera zetu na wananchi wakatoa maamuzi yao, yamekwisha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sisi Serikali ya CCM tuachiwe, muda wa kushindana hatuna tena, sasa tuna jukumu kubwa la kusimamia Ilani ya Uchaguzi. Mnataka kutu–*derail* tutoke katika njia ya kusimamia Ilani yetu tuje tushindane, tunashindania nini sisi na ninyi? Chambilecho alisema kwamba tunajenga nyumba moja, tunagombea fito za nini? Nafikiri mfano ule unakuja zaidi kwako. Sisi bwana kushindana, muda huo hatuna na wana-CCM tusikubali kushindana, sasa hivi tuna kazi moja ya kusimamia Ilani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kushindana kwenye nini? Kama hivi, tuzungumzie ushuru wa mafuta ya taa leo ambao ulishaondolewa juzi, tunaendelea kushindana leo. Kazi ya Kambi hii ya Upinzani ni kushauri, siyo kulazimisha na anayeshauriwa ana hiari ya kuchukua kipi na kuacha kipi. Kazi ya upinzani ni Serikali kivuli, siyo Serikali mbadala. Hakuna mbadala katika Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nasema, kwa binadamu tulivyoumbwa, laiti macho yangekuwa na miguu, kule angani ingekuwa ni ajali kila siku watu wote wakipita pale wakiona Ikulu wanataka kuingia kule. Hatuenei sote mle! Tuingie kwa utaratibu na utaratibu tunashindanisha sera wakati wa kampeni, zikiisha ushindani wote umekwisha, tunakuja hapa sote tunashauri kumsaidia mwananchi wa Tanzania.

Kwa hiyo, hii habari ya Kanuni, najua wamesema kujipa jina ni haki ya mwenye kujipa jina, lakini kwa sababu na sisi tunaliita hilo jina na sisi tuna haki ya kuliona linafaa au halifai na kwa haraka haraka tu, hili halifai, ninyi mbakie kuwa Kambi ya Upinzani tu bwana! Hiyo itakuwa imetosha kabisa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, jamani Ndundu – Somanga wakati inajengwa hii barabara basi wakati wa mvua wale wakandarasi waliokuwepo barabarani wahakikishe kwamba hatukai tena foleni huku magari 20 huku 40. Sisi wananchi wametukubali kwa ilani yetu tusipokuwa makini na madhubuti kwa watendaji wetu tutaumia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumkumbusha tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba hizi shilingi milioni 155 za *rehabilitation,* maadamu wanazo za

*construction,* zitoke ziende kwenye Hospitali ya Wilaya. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu habari ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini atakapokuwa ana-*wind-up* atupe mambo yake yanakwendaje.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Waziri wa Maji na Naibu wake nimpeleke Chikonjia akasikilize malalamiko ya wananchi, lakini nitafurahi zaidi akiwa na Naibu Waziri. Ndiyo! Kwa sababu amepita maeneo mengi na kila alikopita amefanikiwa, kwa nini kwangu asije? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Meza imenifahamisha kwamba kulikuwa na makosa, kumbe Mheshimiwa Philemon Ndesamburo alikwishazungumza katika kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, nimefuta jina lake sasa.

Kwa hiyo, mpangilio sasa ni huu. Baada ya Mheshimiwa George Boniface Simbachawene atafuatia Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda na atakuja Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu.

Mheshimiwa Simbachawene sasa!

**MHE. GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nimpongeze tu Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri ya kina na ambayo imetoa sura ya kila kinachoendelea katika nchi yetu. Sina wasiwasi naye, napenda nimhakikishie kwamba kwa namna yoyote lazima sera za Chama cha Mapinduzi zitatekelezwa tu. Kelele za mlango hazimzuii mwenye nyumba kupata usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ambayo nimeona niyafanye ya utangulizi, napenda kutoa pole kwa ajali ilitokea Monduli na kupitia kwa Mbunge wa Monduli Mheshimiwa Waziri Mkuu, niwape pole wananchi wale waliopoteza maisha yao katika ajali iliyotokea majuzi. Lakini pia niwape pole iliyomhusisha Mbunge wa zamani wa Mwanza, Mheshimiwa Stephen Kazi na wengine wote kwa pamoja. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amin!

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze na jambo langu la kwanza. Tunazungumzia dhana ya *Decentralisation by Devolution,* yaani *D by D.* Katika dhana hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anawasilisha alisema zinakwenda shilingi bilioni 216 kwenye Serikali za Mitaa na zitakwenda moja kwa moja vijijini.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu mimi hapa ni uwezo wa kuzitumia na kuzisimamia fedha hizi kule vijijini na moja kwa moja bila kupoteza muda, nishauri kile ambacho nilidhani pengine kinaweza kutusaidia.

Wakati fulani tukiwa bado vijana wadogo tulikuwa tunasikia kwamba kwenye vijiji kuna Mameneja wa Vijiji. Miradi mingi ambayo inafanyika kule vijijini na

inasimamiwa na wananchi kwa hakika inakosa utaalamu kwa kiasi kikubwa katika usimamizi wa miradi.

Pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika ujenzi wa shule yaani shule za msingi na sekondari na zahanati ni kweli kwamba ufanisi wa baadhi ya miradi umekuwa ukileta matatizo kidogo ni vema sasa Serikali ikaona namna ambavyo inaweza ikafanya nap engine kupitia bajeti ijayo au kama inawezekana bajeti hii kuwarudisha Mameneja wa Vijiji au kama sio Mameneja wa Vijiji, basi hata katika *level* ya Kata ili waweze kusimamia miradi hii kutokana na hii dhana ya *D by D,* vinginevyo fedha nyingi zitapotea na miradi mingi haitakwenda kama inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia hapa ni suala la barabara za vijijini, kwa maana ya barabara za Halmashauri. Barabara za Halmshauri pamoja na hii dhana ya sasa katika *policy* kwamba tunashirikisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwamba ni lazima kuwe na Makandarasi, lakini uzoefu unaonyesha kwamba utendaji wa kazi wa utengenezaji wa barabara za vijijini sio wa kistadi na sio mzuri sana na hivyo kwa kweli tunahitaji kufanya jambo. Fedha nyingi zitakwenda kule, lakini mwisho wa siku utakapotaka kujua *value for money,* hatutaweza kuiona na hata fedha zilizosemwa zimekwenda karibu shilingi bilioni 23 bajeti iliyopita sidhani kama leo zinaweza zikaonekana. Ni kwa sababu Sekta hii Binafsi ya Makandarasi kwa namna ambavyo inatengeneza barabara zile haitengenezi katika kiwango kinachoweza kikahimili mustakabali wa maendeleo ya hatua kwa hatua.

Mimi ningependa kushauri jambo hapa kwamba pamoja na ile Sheria ya *procurement* kuuza *tender,* kilichobakia na wahandisi wetu katika Halmashauri za Wilaya ni kuuza *tender* tu na siyo kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani turudishe ile hali ya wakati fulani ambapo kila Halmashauri kulikuwa na vifaa vya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri ikiwa na buldoza, kijiko, vifaa vya ujenzi wa barabara, nina hakika hata hii Sekta Binafsi kwa maana ya Makandarasi wataweza ku–*hire* hivi vyombo na kutengeneza barabara nzuri zaidi tofauti na sasa ambapo mtu anapata *tender* ya barabara pengine shilingi milioni 10 halafu anakwenda kuchukua buldoza, akakodi Dar es Salaam au Mwanza alilete Dodoma, afikishe Mpwapwa apeleke Kibakwe, afikishe Wota, hivi kweli hizi pesa alizolipwa zitaweza kumtosheleza na yeye akapata faida? Kwa hiyo, kinachotokea pale ni kuburuzaburuza tu ilimradi ionekane nimefanya lakini kwa kweli ukiangalia pale, *there is no value for money*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Sheria ya *Procurement,* una barabara ya milioni pengine 10 na ndizo barabara, maana fedha za kwenye Halmashauri pengine tunapata fedha za barabara kwa mwaka mzima shilingi milioni 150 au milioni 170.

Kwa hiyo, barabara moja ya kutoka pengine Kibakwe – Ikuyu – Ipera inaweza ikachukua shilingi milioni 10, katika ile shilingi milioni 10 kutangaza tu *tender* peke yake kwenye gazeti ni Sh. 690,000/=, kufungua *Tender* pamoja na *stationery* ni kama Sh.

600,000/=, kufanya *evaluation* pale wanakaaa wataalam ni kama Sh. 200,000/= inakwenda kwenye hiyo hiyo shilingi milioni 10. Kufanya *awarding Tender Board* inakaa tena ni karibu Sh. 600,000/= ukijumlisha ni karibu Sh. 2,000,000,000/= imekwisha, barabara haijatengenezwa na wala mkandarasi hajafika. Hiyo ni *tender* tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeshauri kwamba Halmashauri zimiliki vifaa hivi kama hazifanyi zenyewe, basi Wakandarasi watakodi na hivi watafanya kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Hiyo ipo kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga wana vifaa vyao, Rombo, Kinondoni, Meatu nao wana vifaa vyao wanafanya kazi nzuri na mimi kama Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* nimetembelea miradi hiyo, ni mizuri kuliko Halmashauri ambazo hazina vyombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi ndipo barabara za kule kwangu Kibakwe za Rufu, Wota, Matonya, Galigali, Malolo, Chinyika na hata Godegode ndipo zitakapotengenezwa, vinginevyo tutabakia fedha hazitoshi, hazitoshi, mpaka Ubunge unakwisha unaambiwa wewe hufai, anakuja mwingine naye hataweza hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, siasa ya Majimbo na siasa yetu ya Tanzania ni maji, barabara, kilimo, elimu na umeme. Lakini umeme hatuzungumzii sana, tunachozungumzia ni barabara. Kwa hiyo, hapa tukipata barabara kwa msaada huu, naamini kwamba tunaweza kupiga hatua katika ujenzi wa barabara bora.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalopenda nilizungumzie ni suala zima la kilimo. Wananchi wanajitahidi sana. Tumezungumzia mikopo na tukazungumzia Mfuko wa Uwezeshaji. Kwa ufahamu wangu, nilifahamu kwamba huu Mfuko wa Uwezeshaji ungeliweza kuwasaidia sana wakulima, lakini katika watu wanaozungumzwa kukopeshwa na mfuko huu ambao mimi ningeamini kwamba wengi walikuwa ni wale wa kipato cha chini, wengi ni wale waliopo vijijini ambao wangetaka kupata mikopo midogo midogo kama *Power tillers, tractors* ndogo au majembe ya kukokotwa na wanyama na mimi nilifikiria hivyo, lakini hata ninavyozungumza leo, katika Jimbo langu la Kibakwe hakuna hata mtu mmoja aliyepata mkopo kutoka kwenye mfuko huu wa uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitagemea kwamba hapa na mimi ningeweza kufanya *politics* yangu kwa maana ya kwamba wangepata vifaa vya kufanyia kazi na hivyo kujikomboa kiuchumi. Tafsiri ya Mfuko wa Uwezeshaji imekuwa kinyume kabisa na matarajio yetu tuliyokuwa tumeyaweka kwenye kilimo kwa maana ya sisi tulio kwenye Majimbo yaliyoko vijijini, lakini na wa mijini walitegemea kwamba sasa watu wenye kipato kidogo kama Wamachinga na Mama Ntilie wangeweza kupewa msaada kwa mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie elimu. Katika suala la elimu tunatambua wazi kwamba mgawanyo wa fedha uliokuwepo katika ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu haukuwa unatosheleza na hivyo wananchi kwa kushirikiana na fedha zilizotolewa na Serikali waliweza kukamilisha miradi. Mimi ningependekeza kwamba, baada ya

ongezeko hili la asilimia 18 ya bajeti, basi *effect* hii itiwe kwenye kubadilisha viwango vile vya Serikali katika miradi ya madarasa, nyumba za walimu na madarasa ya sekondari na nyumba za walimu wa sekondari kwa sababu viwango vyake vinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hapa kwamba angalau sasa kwenye darasa iwe angalau milioni sita na kwenye nyumba ya mwalimu angalau iwe kwenye milioni nane, hapo ndipo tunaweza tukafanya wananchi wakachangia kiasi na wakaweza kukamilisha pamoja na kusikiliza hotuba ya Waziri Mkuu. Sikuisikia hii, lakini nadhani iko kwenye mgawanyo wa ndani ambao ningefurahi kama ataisema wakati atakapokuwa ana-*wind-up*.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tatizo lingine la ubadhirifu wa fedha. Ubadhilifu wa fedha katika Halmashauri zetu ni tatizo sugu na wanaofanya makosa hayo wamekwishazoea. Ninapenda kuishauri Serikali kwamba ichukue hatua maana wanaoiba fedha hizo, kesi zinavyoendeshwa karibu wote wanashinda na wanaochukuliwa hatua na kukamatwa ni wachache mno.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hatuwezi tukahukumu, lakini kwa kweli panapokuwa na uwazi, kuna *express evidence* na unashangaa mtu huyo anaonekana ameshinda kesi, inamjengea mwingine imani kwamba hata mimi nikiiba sitaweza kuchukuliwa hatua. Hatua zichukuliwe haraka kwa wale wote na wapo wengine ambao wamepandishwa hata vyeo wakati kwao wana matatizo makubwa.

Nilitembelea na Kamati Zahanati ya Kinesi kule Tarime shilingi milioni 50 ya *joint rehabilitation* fundi ilikuwa imepelekwa pale katika ile shilingi milioni 50 tulichoona kama Kamati ilikuwa ni chumba kimoja cha Mganga kimepigwa rangi. Sijasikia kilichofanyika lakini nina imani kubwa hatua kubwa zinaendelea pamoja na kwamba wahusika walionekana wamehama, wamekwenda sehemu nyingine kwa sababu ilikuwa ni katika *intervention* ya kubadilika Serikali. Lakini kwa kweli hatua kama isipochukuliwa itajenga imani kwamba ukiiba fedha ya Serikali huwezi kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, nishauri jambo la mwisho ambalo ni msongamano wa magari Dar es Salaam. Msongamano hautakwisha mpaka tukubaliane kwamba magari madogo ya *Hiace* yaondoke Dar es Salaam. Nami niungane na Waziri Mkuu kwa aliyoyasema kwamba kwa kweli tufikirie kuwa na magari ya abiria yenye uwezo wa kubeba abiria 50 – 80. Kwa sababu *Hiace* moja inachukua abiria 18 – 20. Kwa hiyo, unahitaji magari karibu 10 kuweza kubeba abiria wa gari mbili tu kubwa. Kwa hiyo msongamano ni lazima utaondoka! Sisi Kibakwe kule tunahitaji hizo *Hiace* zije, nafikiri huko Korogwe wanahitaji *Hiace* ziende na ziondoke Dar es Salaam.

Lakini nafahamu kwamba wamiliki wakubwa wa magari haya wapo Dar es Salaam na wangependa wakae maghorofani waangalie magari yao chini yanapita. Katika hili, kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu kusiwe na simile, magari madogo yaondoke na tuweke magari makubwa Dar es Salaam pamoja na jitihada za kuleta magari yaendayo

kasi na hili lifanyike kwa haraka sana, hali ni mbaya. Unafanya shughuli moja tu Dar es Salaam kwa kutwa nzima.

Mheshimiwa Spika, nimalizie sasa kuwapongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa kutimiza miradi ya maji vizuri. Lakini miradi hii ya maji mingi kwa kweli inakuwa ni ile ambayo inafadhiliwa na *World Bank* au na Taasisi mbalimbali, lakini haitokani na bajeti yetu. Mimi ninapendekeza wakati mwingine na katika bajeti za *basket* tuweke miradi ya maji iwe katika bajeti yetu ya ndani kwa sababu haitekelezeki tukingojea kwa mfano miradi ya *World Bank,* tulipata katika Wilaya ya Mpwapwa Kisima, Wiyenzele, Chinyanghuku, Makose na hata Kidenge, lakini mpaka leo tunaambiwa subiri, subiri na hii ni kwa sababu tunategemea bajeti kutoka kwa wafadhili. Angalau tungeweza kufanya miwili kati ya hii ingekuwa ni hatua nzuri.

Hali kadhalika, hata ya *Quick Winds* Singonali, Kibakwe na hata Mang'anga tangu tulipoingia kwa mfano ya *World Bank* tangu nilipoingia Bungeni nikaenda kifua mbele kujidai kwa wapiga kura wangu kwamba nimepata miradi hii, sasa hivi naona hata aibu kurudi tena niwaambie maana nitawaambia nini? Ninaomba kupitia Bunge na wananchi, wananiona, wajue kwamba mipango haijakaa vizuri na Serikali ndivyo inavyosema kwamba tuvumilie miradi hii itakuja, siyo kwamba mimi Mbunge wao ninaizuia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace S. Kiwelu. Wakati huo huo Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes ajiandae.

**MHE. DR. GUIDO GOROGOLIO SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia machache kuhusu hotuba ambayo imetolewa asubuhi ya leo na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kuchangia, naomba niungane na wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini kutokana na ajali za magari. Nasema kwamba Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema Peponi roho za Marehemu waliopoteza maisha yao. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa rambirambi hizo, sasa naomba nami niingie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli nashindwa hata sijui nianzie wapi, kwa sababu hotuba hiyo imejitosheleza kwa kila hali, imegusa maeneo yote ambayo mwananchi wa kawaida anatarajia kuyasikia na kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilishindwa kuchangia bajeti kwa sababu niliona kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo ambayo inashughulika huko vijijini. Nilitegemea kwamba pengine kutakuwa na mambo ambayo yatakuwa tofauti na yale niliyokuwa nayafikiria, lakini naomba niseme kwamba kwa kweli yote yale ambayo nilikuwa

nayafikiria pengine yanaweza yakawa ni tatizo, yote yameingizwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ni matarajio yangu kwamba yatatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba yatatekelezwa kutokana na jinsi ninavyomfahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama wote tunavyokumbuka, nyadhifa ambazo amewahi kushika siku za nyuma. Nakumbuka kabisa wakati akiwa Waziri wa Mazingira jinsi alivyoshughulikia suala la mazingira. Mojawapo ni kile Kiwanda cha Nguo cha Mbagala na mengi mengine yaliyojitokeza ya kisiasa. Nakumbuka wakati akiwa Waziri wa Maji na Maendeleoya Mifugo mpaka akaenda akagundua mtaalam wake mmoja ambaye hakuwa na sifa, lakini akachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, pia hivi juzi tu usimamizi alioufanya kuhusu uharibifu wa mazingira; kuna maeneo ambayo miaka ya nyuma yalikuwa kabisa kabisa haiwezekani hata kuangaliwa kutokana na uharibifu uliokuwa umefanyikae. Kwa mfano katika Bonde letu la Usangu. Lile bonde kulikuwa na maji ya kutosha kabisa, lakini kutokana na uharibifu wakati kama huu lile bonde lilikuwa linakauka. Lakini kutokana na jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hivi watu wanapita kwa kutumia Boti katika eneo lile. Wanyama wote, maliasili, viboko, mamba sasa hivi wamerejea.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo vinanipa imani kwamba hata hii mipango ambayo ameitoa leo hii itatekelezwa. Sina hayo tu, lakini usimamizi aliouonyesha katika ujenzi wa Shule za Sekondari. Sasa nitakuwa kwa kweli ninakosa fadhila ikiwa sitatoa mfano wa upande wangu wa Jimbo langu la Songwe.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2006 Jimbo la Songwe lilikuwa na shule ya sekondari moja tu ya Serikali, lakini leo hii ninasimama hapa kifua mbele, nina shule za sekondari sita ambazo zimejengwa kutokana na jitihada ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimamia na ninatarajia mwakani tutaongeza shule za sekondari nyingine mbili za Totowe na Namkukwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mfumo huo huo, naomba pia nimpongeze Mkuu wetu wa Mkoa ambaye alisimamia ipasavyo kutekeleza yale maagizo aliyokuwa anayapata kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Nampongeza sana Mkuu wa Mkoa, alikuwa bega kwa bega na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kwa jitihada ambazo walizionyesha wakati wa kushughulikia suala la ujenzi wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, sasa hapo naomba nizungumzie kidogo. Sisi Wilaya ya Chunya tuna bahati mbaya kidogo kwamba kiongozi anapoonyesha jitihada za kuleta mabadiliko kimaendeleo, huyo kiongozi baada ya muda kidogo anahamishwa. Naomba kabisa viongozi hao wawili, Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi wake kweli kabisa wameonyesha kwamba wana nia ya kutusaidia sisi Wilaya ya Chunya, naomba wasihamishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa sababu nimeshasema kwamba hotuba hii inajitosheleza, lakini sio vibaya nikaingia kidogo kueleza hali halisi ya Wilaya yangu ya Chunya kwa sababu ndiyo Wilaya ambayo mimi ninaisimamia na ndipo wananchi walinipa nafasi hii ya kusimama hapa Bungeni nilipo leo. Ni kweli kabisa kwamba Wilaya ya Chunya iko nyuma sana kimaendeleo. Ni Wilaya ambayo ilianzishwa mwaka 1922. Sasa hivi ndiyo inaonekana kwamba ni Wilaya ya mwisho kabisa kimaendeleo. Pamoja na rasilimali zote ambazo tunazo, tuna dhahabu, tuna makaa ya mawe, tuna misitu, tuna mbuga za wanyama, tuna asali, tuna tumbaku, tuna Ziwa, tuna vivutio kadhaa vya utalii na bonde nzuri sana la Songwe ambalo linaweza likachukua kila kitu.

Mheshimiwa Spika, mbali na vitu vyote hivyo, lakini Wilaya ya Chunya bado iko nyuma. Sasa katika kufuatilia, mimi nimeona kwamba kuna sababu kuu mbili ambazo zinaifanya Wilaya ya Chunya iendelee kuwa nyuma. Sababu ya kwanza ni ubovu wa miundombinu hasa barabara. Nitaeleza kwa nini ninasema hivyo. Sababu ya pili, ni watumishi wanaopelekwa katika Wilaya ya Chunya kukaa kwa muda mrefu zaidi na kuamua kufanya kazi kwa uzoefu.

Mheshimiwa Spika, nitajaribu kufafanua ubovu wa miundombinu pamoja na watumishi kukaa kwa muda mrefu. Matokeo yake ni kwamba tumekuwa na umaskini wa kipato wa kukithiri. Hivi sasa ninavyoongea kipato cha mwananchi wa kawaida katika Wilaya ya Chunya na Jimbo langu ni Sh. 467/= kwa siku. Ukifanya mahesabu utapata kwenye Sh.14,000/= kwa mwezi, na ukifanya mahesabu zaidi utapata Sh. 168,000/= kwa mwezi. Sh. 467/= hata kilo ya sukari hainunuliwi, hata kilo la nyama hainunuliwi.

Kwa hiyo, hiyo ni hali halisi inayoonyesha kwamba Wilaya ya Chunya bado tuko nyuma kimaendeleo. Lakini ni kutokana na ubovu wa miundombinu. Inashindakana kuja wawekezaji, inashindakana kuja hata wataalam, inashindakana hata viongozi wa Kitaifa kuitembelea ile Wilaya ili kusudi kuona kuna nini wanachoweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano kidogo tu wa viongozi wa kitaifa. Katika awamu zote nne za Serikali yetu, ni Rais mmoja tu ndiye aliwahi kutembelea Wilaya ya Chunya naye alikuwa ni marehemu Baba wa Taifa. Marais hao wengine waliokuwepo madarakani bahati mbaya hawakupata nafasi ya kuja katika Wilaya ya Chunya. Nina imani kwamba sasa watakuja. Lakini ninashukuru kwamba Makamu wa Rais, Mawaziri Wakuu wamewahi kuitembelea Wilaya ya Chunya ingawa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa ameniahidi kwamba yeye atakuja Chunya.

Mheshimiwa Spika, matokeo mengine ni kwamba kutokana na miundombinu kuwa mibovu, basi kilimo nacho kimekuwa duni. Tatizo lingine ni kwamba sasa hii hali ya miundombinu ndiyo hiyo ambayo inasababisha matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Rais alikuwa ameamua kuja kuitembelea ile Wilaya. Labda nikianza kutoa mifano halisi inaweza ikaeleweka vizuri zaidi. Rais alikuwa ameamua kuja kuitembelea ile Wilaya ya Chunya. Sasa kwa sababu ya ubovu wa barabara na nafikiri ndiyo sababu kuu akapangiwa kwenda kwenye eneo moja.

Bahati nzuri eneo la Mashariki la Wilaya ya Chunya ambako ndiko Jimbo la kwanza la Mashariki, Jimboni kwangu ikashindikana kupangiwa kwa sababu ya miundombinu mibovu na ni kweli jiografia ya ile Wilaya ni ngumu. Kwa hiyo, ukimpangia kiongozi kuitembelea kwa siku moja haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ni asilimia 46 ya eneo lote la Mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo, ukimpangia kiongozi kuitembelea Wilaya ile kwa siku moja ni kweli kabisa haiwezekani. Sasa kasheshe ambayo ilitaka kunipata mimi, wananchi wa Jimbo la Songwe baada ya kujua kwamba sasa Mheshimiwa Rais hawezi kufika kule walianza kunifuata. Wakasema wao wanaamini kabisa kwamba Serikali ya awamu ya nne ni awamu ambayo imekuja na Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, inakuwa namna gani Rais asitembelee kule kwao?

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ile ziara iliahirishwa. Vinginevyo, ningewekwa kiti moto kana kwamba mimi ndiye ninayepanga safari za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kabisa kwa siku zijazo na ninakumbuka kwamba Rais aliahirisha akatuahidi kwamba mwezi Agosti, mwaka huu atakwenda Chunya. Naomba kabisa na Mkuu wangu wa Mkoa yupo pale apewe siku mbili kutembelea ile Wilaya. Vinginevyo, kwa kweli kutakuwepo na matatizo, tutaanza kulaumiana kwamba Mkuu wa Mkoa kwa nini amepanga hivyo, Mkuu wa Wilaya kwa nini amepanga hivyo. Ni kutokana na jiografia ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya pili, ni watumishi kukaa katika eneo lile kwa muda mrefu na kuamua kufanya kazi kwa uzoefu. Hili nasema kwamba ni tatizo, mtumishi anakaa mahali kwa muda zaidi ya miaka 10 na kwa bahati mbaya kwa sababu ya eneo lenyewe ndiyo halitembelewi tembelewi na viongozi, basi huamua kujiingiza kwenye mambo mengine. Wengi wamefungua baa, wengi wamefungua maduka, wengi hata kwenye siasa wamejiingiza kutafuta nafasi za uongozi, kwa nini? Kwa sababu ya hali halisi na uzoefu wamekaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alipokuja kule alionyesha kwamba ana nia ya kuweza kuwahamisha na ameishaanza kuwahamisha. Namwomba Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aendelee na hasa zaidi wale ambao wanatusumbua ni walimu ambao wamekaa kwa muda mrefu katika eneo hilo ambao sasa wameamua kujiingiza kwenye siasa. Sijui kwa wenzangu, lakini wameamua kujiingiza kwenye siasa. Sasa huwa ninafikiri ule Waraka Na.2 wa Watumishi sijui hao hauwahusu au ni namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba labda waangalie katika hayo maeneo ambayo ni dhahiri kabisa kwamba watumishi wa Serikali wanazuiliwa kujiingiza katika mambo mengine. Lakini katika ule Waraka, umesema wazi wazi kwamba, endapo wewe kama unataka kujiingiza kwenye siasa, basi jiuzulu katika upande uliopo na kujiuzulu ni kitu kizuri tu. Watu mnakwenda mnapambana jukwaani, lakini hii ya kuanza kufanya mambo kisirisiri na nini haifai. Kwa kweli hili ni jambo

ambalo mimi linanipa shida kidogo. Katika matatizo haya , mimi naiomba Serikali kabisa ijaribu kuona ni matatizo katika Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie kwa kujaribu kuikumbusha Serikali kuhusu ahadi za Serikali ambazo imezitoa kwenye Bunge hili. Kuna ahadi ambayo ilitolewa kutengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe na lami kwenye sehemu mbalimbali korofi katika Jimbo langu. Barabara ya Mbalizi-Mkwajuni na Makongorosi, naomba itengenezwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba muangalie zile dakika 15, haipendezi hotuba yoyote mwishoni inakuwa ni nzuri kama unaweza ku-*summarize* vizuri. Nitoe tahadhari tu kwamba, katika Kanuni, rasimu mpya tunazoandaa, haya mambo ya kupongezana sana yanawachukulieni muda bure. Akishasema Mheshimiwa Waziri Mkuu amepongeza au mtoa hoja, muwe mnaunga mkono tu, basi kwamba unaunga mkono aliyoyasema kuhusu kupongeza. Lakini ukianza na pongezi ndefu ni ustaarabu, utamaduni, lakini tubadilike na wakati.

Sasa namwita Mheshimiwa Grace Kiwelu. Nimeambiwa Mheshimiwa Gosbert Blandes hajaonekana. Kwa hiyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, baada ya hapo atakuja Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nami napenda pia pamoja na kutwambia kwamba tusipongeze, lakini naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida siku hizi kila tukiamka asubuhi, tukitazama Vyombo vya Habari kupata taarifa za ajali. Leo asubuhi nimesikiliza katika *radio* wanasema leo ni siku ya kumi tumepoteza Watanzania 51. Hii inatisha kwa Watanzania wengi hivyo kufa. Tunaiomba Serikali na Wizara inayohusika kulifanyia kazi jambo hilo na wale madereva wazembe wanaosababisha ajali hizo waweze kuchukuliwa hatua kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pole kwa familia waliopatwa na misiba. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi na wale waliopata majeraha, basi tunamwomba Mwenyezi Mungu awawekee mkono wake waweze kupona na kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Timu ya *Taifa Stars* kwa ushindi waliouleta katika nchi yetu na tuliweza kuileta katika Bunge lako Tukufu na kuipongeza. Lakini napenda tu kuwaambia wale ndugu zangu wa upande wa pili, ilionekana sana kusema ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini napenda

kuwaambia, hakuna Chama chochote makini kilichoingia kwenye uchaguzi bila kuweka suala la michezo mbele. Sisi CHADEMA tunaamini kabisa michezo ni chanzo kinachoweza kuwapatia vijana wetu ajira na tunapenda kuwambia CCM, katika zile ajira walizoahidi kwa Watanzania wakipitia katika suala la michezo wanaweza kuleta hizo ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tulipongezwa kwamba Wapinzani tunasoma Ilani za Chama cha Mapinduzi. Tunasoma kwa nia njema tuweze kuwakumbusha wenzetu yale ambayo waliwaahidi Watanzania kupitia kwenye Uchaguzi Mkuu kama kweli wanayatekeleza na kama wameyasahau, basi tuwakumbushe na kama waliyatumia tu kupata kura, basi tuwakumbushe Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nianze na elimu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* na ninakushukuru kwa kunipanga katika Kamati hiyo kwa sababu nimeweza kuzunguka na kuona mambo mengi na kujifunza mengi. Tunayoyasema hapa ni kwa ajili ya kuboresha wala si kwa ajili ya kusutana.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wananchi kwa kujitolea kujenga shule za sekondari za Kata pamoja na hali ngumu ya maisha, lakini walitii agizo na waliweza kujenga shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo katika shule zetu za sekondari za Kata. Moja ni tatizo la walimu na hili nilishauliza swali ndani ya Bunge na Waziri alijibu kwamba wameliona tatizo hilo na wameanza mkakati wa kuwapata walimu hao.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hosteli hasa kwa wasichana katika shule hizo za sekondari za Kata. Nitatoa mfano. Tulitembelea katika shule ya sekondari ya Kisarawe katika Manispaa ya Temeke Kisarawe II. Shule hiyo imejengwa kilomita 20 kutoka kwenye makazi ya watu, hakuna usafiri wa kuwafikisha wanafunzi hao shuleni na wanafunzi wakifika shuleni siku hiyo kesho yake hakuna masomo, inabidi walale na wanalala madarasani. Shule haina umeme, haina ulinzi wowote na ni shule ya mchanganyiko wasichana na wavulana. Je, hiyo elimu wanayoipata watoto hao ndiyo ile elimu tunayoitegemea iwe bora! Wanapata masomo siku moja na siku ya pili hakuna masomo kwa sababu siku ya pili ni ya safari ya kurudi nyumbani, wanalala hakuna chakula wala hawana ulinzi wowote.

Mheshimiwa Spika, kubwa linalotokea pale ni kwa wanafunzi wasichana kupata mimba. Hawana ulinzi wowote, wakati tunasema tunatoa kipaumbele kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, katika hili, tunaomba lifanyiwe kazi ili watoto wetu hao wa kike waweze kupata elimu bora pamoja na wavulana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hosteli, pamoja na kwamba watashirikishwa tena wananchi, lakini tunaomba zijengwe kwa kushirikiana na Wizara. Maana wananchi nao kwa kweli wamechoka, lakini kwa kuwa ni watoto wetu hatuna budi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, linalofuata ninalopenda kulizungumzia sasa ni afya. Wakati tunaahirisha Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba kutakuwa na ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya na ujumbe huo tuupeleke kwa wananchi na amesema pia katika hotuba yake aliyoisoma leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninajiuliza, hivi vile Vituo vya Afya na Zahanati tulizonazo zote zinafanya kazi? Tuna wahudumu wa kutosha wa kuweza kuwahudumia wananchi? Mheshimiwa Rais alipokuwa katika Mkoa wa Rukwa alisomewa taarifa kwamba zipo Zahanati na Vituo vya Afya 12 vimefungwa havina wahudumu. Je, hizo Zahanati na Vituo vya Afya tutavyovijenga sasa hivi tumejiandaa kwa kiasi gani? Tunao wahudumu wa kutosha, tuna vifaa vya kutosha katika hospitali zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isieleweke kwamba sisi tunapinga, ni wazo jema, lakini linahitaji maandalizi, wasije wakashirikishwa wananchi wakapoteza nguvu zao nyingi lakini wakakosa kupata matunda waliyoyategemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba kabla ya kuwashurutisha wananchi kujenga Vituo vya Afya, tufanye maandalizi kwanza kuhakikisha kwamba wahudumu tunao wa kutosha, vifaa vya kutosha tunavyo ndipo wananchi hao waanze kujenga hivyo Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema mwanzo, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, tulitembelea Halmashauri nyingi sana katika nchi yetu na tulikutana na ubadhirifu mkubwa hasa kwa watendaji wa Halmashauri. Wengi wanafanya kazi zao tofauti na maadili ya utumishi wa umma unavyotaka, fedha nyingi zinapotea na fedha nyingi hawazionyeshwi kwenye vitabu.

Mheshimiwa Spika, hili nataka niliseme kwamba katika ujenzi wa shule wananchi walichangia sana, lakini Halmashauri nyingi hazionyeshwi nguvu za wananchi na hii inatutia wasiwasi mkubwa sana kwamba wananchi wametumia nguvu zao, walibeba mawe, walichota maji, walisomba mchanga, lakini nguvu zao hazithaminiwi kama fedha. Hata kama nguvu zao inatia wasiwasi kwamba fedha zile aidha wanachukua watendaji wanaweka mifukoni na hawaonyeshi katika vitabu zile nguvu za wananchi. Kwa hiyo, tunawaomba watendaji wa Halmashauri waonyeshe nguvu za wananchi ili wananchi waone kwamba wameshirikishwa kwa vile vitu walivyovifanya ni mali yao.

Mheshimiwa Spika, watendaji hao wamekuwa wakifanya makosa katika Halmashauri zao na kusababishia Halmashauri kupata hati chafu. Wananchi wanapata hukumu kwa sababu ya makosa ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ziko Halmashauri nne ambazo zimepata hati chafu. Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Igunga, Kigoma Vijijini na Manispaa ya Sumbawanga. Wananchi hao tunawaadhibu kwa makosa ya watu wengine, fedha wamechukua wengine! Kama ni tatizo la Uhasibu, mwananchi kwa nini abebe lawama? Wananchi wanakosa ruzuku ya maendeleo kwa sababu ya watu wengine! Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

hebu walishughulikie tatizo hili hata kama ni wahisani wametupa masharti hayo, basi wajaribu kuzungumza nao waambiwe kwamba Watanzania wanaumia kwa sababu ya makosa ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tulilokutana nalo kwenye Kamati yetu ya *LAAC* ni suala la mikopo. Mikopo ya akinamama na vijana, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana katika Halmashauri zetu na katika maagizo tuliokuwa tukitoa kwenye Halmashauri zilizokuja mbele ya Kamati ya *LAAC* ni kuhusu hilo na kila walipokuja kwenye Kamati yetu tatizo hilo halitatuliwi wala halijibiwi.

Mheshimiwa Spika, juzi tulipokuwa na Mkoa wa Singida ilidhihirika kabisa kwamba mikopo hiyo ilitolewa kisiasa na Kambi ya Upinzani tulishasema hili ndani ya Bunge lako Tukufu, tukaambiwa sisi ni waongo. Lakini hili limedhihirika tulipokuwa na Mkoa wa Singida na bahati nzuri tulikuwa na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na yeye alikiri hili, akasema kwamba mikopo hii inawapa shida sana kuikusanya kwa sababu mikopo hiyo mingi ilitolewa kisiasa na waliopewa fedha hizo hawajulikani. Vikundi havijulikani vilipo na hivyo inakuwa ni tatizo sana kuwapata watu hao na wanafanya utaratibu wa kuweza kuondoa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali inapokuwa ni suala la Kitaifa, hebu tuweke utaifa mbele.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Haroub S. Masoud.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, natumia kifungu namba 80(1). "Ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni." Kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni anawajibika kuwa na uhakika wa maelezo anayoyatoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub Masoud hakuna kanuni 80(1). *(Makofi)*

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, samahani kanuni 50(1). Kanuni inaeleza wazi kabisa kwamba: "Mchangiaji yeyote anapokuwa Bungeni akichangia anatakiwa aseme jambo ambalo ana uhakika nalo."

Je, Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anazungumza anaweza kuthibitisha kwamba Mheshimiwa John Chiligati anaweze kuthibitisha hayo anayoyasema yeye hapa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Grace Kiwelu anamnukuu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ambaye alikuwa naye safarini. Kama yeye anasema uwongo, utagundulika tu na athari zake zitakuwa mbaya kwa Mheshimiwa Grace Kiwelu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Grace Kiwelu endelea.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ninayosema ni kweli na katika Kamati yetu tuna *Hansard,* kila tunachosema kinarekodiwa. Tulipokuwa Mkoa

wa Singida *Hansard* yake iko, nitaomba iletwe mbele yako Mheshimiwa Spika na usome tuliyoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaendelea. Kwa hiyo, ninawaomba viongozi wetu pale linapokuja suala la kitaifa, basi wote tushirikishwe, kusiwe na mambo ya kutengana kwa kuwa wote ni Watanzania.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, samahani kidogo, turekebishe hapa. *Table* inabidi tunapofanya *interruption* ya utaratibu mrekebishe saa. Sasa kengele inaendelea kulia inatuletea matatizo. Tutakuwa tunamnyima haki yake Mheshimiwa Mbunge anayezungumza. Nahisi pengine ni dakika tatu hivi tumempotezea.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Basi niendelee kuweka msisitizo kwamba nchi yetu hii ni yetu wote, tunaomba Watanzania wote washirikishwe, ile mikopo yote itolewe, kama ni kwa vijana na akina mama basi wasibaguliwe kufuata vyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ninalotaka kulisemea ni kuhusu kuhamia Dodoma. Hiki ni kipindi changu cha pili katika Bunge lako Tukufu na kila tunapokuja ni suala la kuhamia Dodoma. Sasa walituambia kupanga ni kuchagua. Unaweza ukachagua ukawa umechagua vibaya, kwa hiyo unaruhusiwa kupanga tena. Je, bado wana dhamira ya kweli ya kuhamia Dodoma? Kama hawana, waliambie Bunge lako Tukufu. Au ni ule usemi aliosema Mheshimiwa Phares Kabuye kwamba Dodoma itakuwa ni Makao Makuu ya Bunge na Makaburi ya viongozi?

Mheshimiwa Spika, tunataka katika kikao hiki Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha hoja yake, atuambie nini walichofikia CCM? Kama wanaona Dodoma hapafai, basi wasiendelee kuliingizia Taifa gharama, turudi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kuendelea kunilinda. Nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepewa taarifa na Mheshimiwa Eustace Katagira kwamba Mheshimiwa Gosbert Blandes hajisikii, vizuri ndiyo maana hayupo hapa. Kwa hiyo, tunaendelea sasa. Namwita Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama na nadhani baada ya hapo, wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Paschal Degera.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii ya awali kabisa kukushuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro na kwa dhati ya moyo wangu, naomba kabisa nianze kwa kuwadhihirisha kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazingatia

utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kimsingi mimi mwenyewe ninaiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichaguliwa Chama chetu kuongoza nchi kwa miaka mitano. Tulinadi ilani hii ya Uchaguzi kwenye kona zote za nchi yetu na nataka niwahakikishie kwamba kwa muda wa miaka miwili au mwaka mmoja na nusu Watanzania wanaendelea kuridhika na utekelezaji wa Ilani ya CCM. Mfano mzuri wa uhakika na ushahidi wa dhati ni kura za ndugu yetu Mtutura Abdallah Mtutura na kura zile za Madiwani ambao CCM imepata ushindi wa kishindo. Ninawapongeza Watanzania kwa kuendelea kuwa na imani na Chama chetu.

Mheshimiwa Spika, yako mambo ambayo tumeyapa kipaumbele katika bajeti yetu ya mwaka huu. Mimi nataka kusema hatujakosea na hasa kwa kutanguliza kuipa kipaumbele elimu. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mawaziri wote hawawezi kukwepa kupokea sifa na heshima ya Watanzania kwa Mapinduzi makubwa waliyoyafanya kwa kipindi kifupi cha uongozi wao kuimarisha elimu katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari na kupandisha asilimia ya watoto waliomaliza elimu ya msingi kujiunga na elimu ya sekondari. Waziri Sitta anastahili pongezi na wananchi wa Simanjiro wameniomba nimpongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ombi moja la wananchi wa Simanjiro ambalo Bunge hili linapaswa liifahamu ni Jiografia ya Wilaya ya Simanjiro. Umbali kati ya kijiji kimoja na kijiji kingine ni wastani wa kilomita 50 mpaka 70. Kwa hiyo, tunapojenga shule za sekondari za Kata tunazungumzia umbali wa kutoka kijiji ‘A’ kwenda kijiji ‘B’ ambayo tunazungumza umbali wa kilomita 50 na 70.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, shule zote 11 tulizoanza kuzijenga zinalazimika kuwa shule za bweni na kwa maana hiyo natarajia Waziri Mkuu na Waziri wa Elimu waiangalie Wilaya ya Simanjiro kwa jicho la huruma kwa upande wa ujenzi wa hosteli za watoto ili watoto hao waweze kusoma shule kwa sababu hawawezi kusoma shule za kutwa. Hicho ndicho kilio chetu cha kwanza ambacho ningependa kukifikisha mbele ya Serikali ya Chama chetu kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa ilani ibara ya 43 iliweka bayana suala zima la kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. Nina heshima tena kuipongeza Serikali ya awamu ya nne kwa kuanza utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Wilaya ya Simanjiro yaani Orkesmet. Lakini pamoja na pongezi hizo ni lazima nieleze tatizo lililopo katika utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, katika hili ningependa sana Waziri Mkuu anisikilize vizuri. Iliamuliwa kuchukuliwa umeme kutoka Wilaya ya Same ambayo iko mashariki mwa Wilaya ya Simanjiro.

Kwa hiyo, umeme ule ulilazimika kutoka mashariki kwenda magharibi kupitia kijiji cha Muungano na ilipaswa kuvuka Mto Ruvu kupitia kijiji cha Darajani kuingia kijiji cha Ngage katika Wilaya ya Simanjiro na kuendelea kwenda kusini kwenye kijiji

kinachofuata cha Roborsoiti ili kujenga mazingira muafaka ya mradi wa maji unaotarajiwa kuvutwa kutoka katika kijiji cha Roborsoiti kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro ambayo ni Orkesmet. Hapa ndiko liko tatizo moja ambalo limejitokeza la ubinafsi na ambalo kwa kweli sina haja ya kulieleza maana lina sura la ukabila na ambalo ningependa Ofisi ya Waziri Mkuu iangalie vizuri na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi tangu mwaka 1968/1969 Bwawa la Nyumba ya Mungu lilipojengwa upande mmoja wa bwawa liko katika Wilaya ya Simanjiro na upande wa pili wa bwawa liko katika Wilaya ya Mwanga. Ukienda saa kama za usiku upande wa Mwanga kuna taa upande wa Simanjiro, ni nguzo tu zinazotoka Nyumba ya Mungu kuingia Kariet, Ngorika, Magadini, Kiruani, Msitu wa Tembo, hakuna *bulb* mpaka unaingia Kiwanda cha *TPC* katika Mkoa wa Kilimanjaro ndiyo taa inawaka.

Mwaka huu pamoja na fedha tulizopewa kwa mradi wa Simanjiro na Ukerewe uliofadhiliwa na Serikali ya Sweden, kitendo cha aibu ambacho kimefanyika badala ya umeme kutoka Muungano na kuvuka kuingia Wilaya ya Simanjiro imeendelea kuambaambaa na ng'ambo ya pili ya mto kuhudumia vijiji vitatu au vinne vya Wilaya ya Same bila kwenda katika eneo ambalo lilikusudiwa na wahisani na bila kuzingatia makubaliano ya kikao cha wadau kilichokutana *White Sand* tarehe 26 Agosti, 2006 ambayo Mheshimiwa Msabaha - Waziri wa Nishati na Madini (kwa wakati huo) baadaye aliniahidi kwamba maamuzi ya wadau yatazingatiwa.

Ningependa kuiomba Serikali katika hili kwa kweli ilifanyie kazi kwa kiwango kinachostahili ili kuwapa wananchi wa Simanjiro haki yao na sio kwamba ionekane Simanjiro ndiyo mahali panapostahili kukaa gizani lakini Wilaya za jirani zetu kwa ng'ambo ya pili wao wanaendelea kukaa kwenye mwanga na sisi huku tunaendelea kukaa kwenye giza, eti umeme unapita kwenye Kitongoji kimoja cha Oletibu na kwenda Makao Makuu ya Wilaya Simanjiro Orkesmet na huku tunaendelea kunyamaza eti hivyo ndio uungwana.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kusema, katika hili namwomba Waziri Mkuu aingilie kati. Nimemwandikia barua, nimemwandikia Waziri wa Nishati na Madini, nimempa nakala Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, hiki ndiyo kilio cha kwanza cha Wilaya ya Simanjiro kwa Serikali ya Awamu ya Nne kupitia Bunge hili Tukufu. Katika hili, ningependa kabla ya hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini wananchi wa Simanjiro wangependa kupata kauli ya huruma na ya haki kuhusiana na umeme huu.

Mheshimiwa Spika, kilio cha pili ni mgogoro wa wachimbaji wadogo wa madini ya *Tanzanite* pale Mererani baina yao na wachimbaji wakubwa. Kwa kweli, napenda tena nimpongeze Waziri Mkuu alimwagiza Waziri wa Nishati na Madini kulimaliza tatizo hili. Lakini tatizo halijaisha na haliishi kwa sababu watu hawapendi kwa wakweli. Mgogoro uliopo ni wa mpaka kati ya Kitalu 'B' na 'C' ambayo 'B' inamilikiwa na wachimbaji wadogo na Kitalu 'C' inamilikiwa na wachimbaji wakubwa. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba kulikuwepo na mgogoro wa mpaka huo tangu mwaka 1987 baada

ya Kampuni ya Graphitan kuondoka na baadaye eneo hilo kumilikiwa na Kampuni ya *Tanzanite One* ikitumia jina la *MML* na baadaye mipaka ile ikahamishwa.

Mheshimiwa Spika, ushahidi ulioko ya ripoti ya Tume iliyoundwa na Waziri wa Nishati na Madini iliyoongozwa na Jenerali Mstaafu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Jenerali Mboma. Moja kati ya mapendekezo ya Tume ya Jenerali Mboma, naomba kunukuu kwa ruhusa yako. Inasema hivi: "Ili kuleta na kuboresha mahusiano mema kati ya wachimbaji wadogo na mwekezaji mkubwa *MML* ambaye sasa ni *Tanzanite One,* ni vyema tatizo la mpaka kati ya *Block 'B'* na *'C'* litatuliwe. Mpaka huo wa mwanzo urejeshwe sehemu ulipokuwa. Jukumu la kufanikisha jambo hili ni la Wizara yenyewe ya Nishati na Madini kwa kuwahusisha pamoja na wahusika wengine." Mwisho wa kunukuu.

Ukiendelea utakuta kwamba majalada 110 yaliyokuwa yamepotea Wizara ya Nishati na Madini yanadaiwa ndiko liliko jalada lililokuwa linaonyesha mipaka kati ya Kitalu 'B' inayomilikiwa na wachimbaji wadogo na Kitalu 'C' inayomilikiwa na Kampuni kubwa ya *Tanzanite One.* Ningependa kumhakikishia kwamba mgogoro ule haujakwisha na namna ya pekee ya kulimaliza ni kuhakikisha kwamba mpaka ule wa awali unaheshimiwa bila ya kuangaliwa sura ya mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea kuweka hali hii kuwa hali mbaya zaidi ni pale ambapo wachimbaji wadogo wapatao 23 wanasimamishwa kwa mgogoro huo wa mpaka, lakini yule ambaye wanagombania mpaka nao anaendelea kuchimba na wale wengine wamesimamishwa na hili naliona kabisa ni suala la ubaguzi la kuendelea kuwagandamiza wachimbaji wadogo na kuwabeba wawekezaji wakubwa. Sijui ni kwa maslahi ya nani!

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu atusaidie tena katika hili.

Mheshimiwa Spika, liko jambo moja ambalo ningependa tena niligusie baada ya kuzungumza hilo, nalo ni suala la Mradi wa Maji kutoka Robostret kwenda Orkesmet. Ningependa tena kuiomba Serikali ijielekeze katika kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kuvuta maji kutoka Mto Ruvu ili kwenda Orkesmet kwa nia ya kuweza kuwasaidia wananchi wa Wilaya Simanjiro ambao wanaishi katika nyanda kame.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia sasa linahusu suala zima la ubadhirifu wa mali ya umma. sera ya kupambana na ubadhirifu wa mali ya umma ni sera ya Chama cha Mapinduzi na haikuanza sasa, ilianza tangu zamani. Nawahakikishieni kwamba hata viongozi wa zamani wa Chama chetu waliwahi kuonyesha msimamo juu ya jambo hili. Ningependa kunukuu maneno ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Edward Moringe Sokoine wakati akiendesha vita dhidi ya wahujumu uchumi na walanguzi. Marehemu Sokoine alisema hivi:

"Tumeruhusu walanguzi na wahujumu uchumi kuongoza nchi, wananchi wamefikia mahali ambapo wanashindwa kutofautisha kati ya viongozi wa Chama na

Serikali na walanguzi na wahujumu uchumi wa nchi. Walanguzi ni wahujumu uchumi, wote ni maadui wa Taifa, ni lazima kuwapiga vita vya kuwatokomeza".

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wetu wa sasa, Mheshimiwa Edward Lowassa katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka jana katika kudhihirisha dhamira ya Awamu ya Nne ya kupambana na watu ambao sio makini katika kuwaletea Watanzania maisha bora, naye alisema hivi:

"Serikali ya Awamu ya Nne haiwezi kuwaachia kila kiongozi wake au kila mtendaji kusikiliza na kucheza ngoma anayoipenda. Tumeahidi maisha bora kwa kila Mtanzania, tutekeleze ahadi hiyo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, asiyeweza kucheza ngoma kwa midundo inayopigwa na Serikali ya Awamu ya Nne itabidi atupishe."

Mheshimiwa Spika, ninasema nawanukuu viongozi hawa mahiri wote wawili ambao wamewahi kushika nafasi hii ya Uwaziri Mkuu. Nia yangu ni kuonyesha kwamba imefika wakati ambapo Serikali yetu lazima idhamirie kupambana na ubadhirifu wa mali ya umma. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaonyesha ubadhirifu mkubwa wa shilingi trilioni 1.2. Hatuwezi kuendelea kuwatazama watu hawa hivi hivi tu. Hapa tunasikia minong'ono mingine ambayo inahusisha Taasisi za umma na inakuwa mbaya zaidi zinapotajwa Taasisi ambazo hazina yetu ya nchi nzima ipo na hiyo ni Benki Kuu ya Tanzania. Hili linahitaji majibu, haliwezi kukwepwa.

Mheshimiwa Spika, tutoe ufafanuzi wa kutosha na ikibidi kuwaridhisha Watanzania kwa kuunda Kamati Teule ya Bunge ili Watanzania waendelee kuwa na imani na sisi wenyewe. Kuacha kufanya hivyo, haitaonyesha au itatia mashaka dhamira yetu ya kupambana na wabadhirifu wa mali ya umma na mimi ningetaka katika hili tujielekeze huko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika Halmashauri zetu za Wilaya na Wizara zetu pamoja na Mikoa, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaonyesha dhahiri kwamba liko tatizo la ubadhirifu wa fedha za wananchi. Hatuwezi kuwaletea Watanzania maisha bora wakati tunaendelea kubaki na wale wabadhirifu ndani ya Serikali yetu. Ni lazima tuwabaini ni akina nani? Wako wapi? Wameiba kiasi gani? Wametumia vibaya kiasi gani? Watupishe ili Serikali ya Kikwete iweze kutimiza ahadi ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hili halina itikadi na kama ni itikadi namba moja ni ya CCM na lazima tupambane kidete katika hili. Hatuwezi kuwaletea Watanzania maisha bora kwa kuwavumilia wabadhirifu wa mali ya umma. Hawa lazima tuwajue, tuwashughulikie ipasavyo na ndivyo tutatimiza wajibu wetu kama Bunge kwa mujibu wa ibara 63 ibara ndogo (1 – 3) kazi ya Bunge ya kuisimamia Serikali. Tupambane kulinda heshima ya Chama chetu kwa kuwashughulikia hao wote kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninalotaka kuzungumzia ni mifugo. Mifugo imeachwa, mabwawa mwaka jana hatujapata, majosho hatujapata, dawa za kuogesha hatujapata!

Mheshimiwa Spika, tunategemea kwamba Mheshimiwa Diallo atakapowasilisha bajeti yake hapa awape wafugaji matumaini juu ya majosho na malambo kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kusema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu inayohusu Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zote ambazo ziko chini ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitii utaratibu wa kanuni za Bunge na mimi kiufupi niseme tu naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza majukumu yake ipasavyo kulingana na Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Songea imetekeleza maagizo yote ambayo yamekuwa yakitolewa kupitia Ofisi mbalimbali zinazosimamia utekelezaji wa Ilani na ninaomba kusema hasa katika sekta ya elimu tumeweza kufanya vizuri sana na katika sekta nyinginezo kulingana na maagizo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, bila ya kupoteza muda, sasa naomba niendelee kujikita katika yale ambayo niliazimia kuyazungumza katika siku hii ya leo. Mkoa wa Ruvuma hususan Wilaya ya Songea, Jimbo la Peramiho, unapozungumza suala la pembejeo unagusa roho za wapiga kura wa Jimbo langu la Peramiho na unagusa uchumi wa wananchi wa Jimbo langu la Peramiho.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia taarifa ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nikasoma kipengele kinachohusiana na jinsi gani Sekta ya Kilimo inavyoweza kuchangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. *Composition* ya *labour force* katika nchi yetu ya Tanzania asilimia 81 inatokana na kilimo, asilimia 9.0 inatokana na *informal sector*, asilimia 4.0 inatokana na *private sector* na asilimia 3.6 inatokana na *Housework,* lakini asilimia 2.4 inatokana na *public sector*.

Mheshimiwa Spika, kiasi kikubwa cha nguvukazi kiko katika maeneo ya vijijini na kiasi hicho kikubwa cha nguvu kazi kinatumika kuanza kabisa katika kutekeleza shughuli za kilimo ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wazalishaji wakubwa na waongezaji wa pato la Taifa ni wakulima vijijini. Lakini unaona nguvu kazi hizo nyingi kule vijijini hazina tija na hazina ujira na hasa katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme kwamba imefika wakati nimshukuru Waziri Mkuu, leo ameniambia kwamba anaongeza fedha na anaongeza wigo wa matumizi wa ruzuku katika suala la kilimo hasa kwenye masuala ya madawa na

kadhalika. Lakini naomba niseme ni lini tatizo la ruzuku litapatiwa ufumbuzi? Ni lini? Tutakubali kwamba tumechoka kusikia hadithi za matumizi ya ruzuku katika kuwaneemesha wale ambao wameshatosheka badala ya wale walalahoi kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme kwamba mwaka jana wakati nachangia hotuba hii nilisema, jamani tusikilizane, tukubaliane kimsingi kwamba tatizo la ruzuku ya pembejeo limekuwa ni tatizo sugu ambalo linahitaji kabisa kufanyiwa kazi ya kina na ya kutosha. Jinsi tulivyolibebabeba mwaka jana limeleta matatizo makubwa mwaka huu tumepata shida kubwa sana kwa wakulima kule vijijini.

Mimi naomba nimshukuru sana Mkuu wangu wa Wilaya. Tuliamua kukubaliana kupitia katika Halmashauri yetu, Wilaya yetu na Mkoa baadaye lakini kwenye Wilaya yetu tulikubaliana ruzuku ipitishwe kupitia Vyama vya Akiba na Mikopo. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu angalau liliweza kufanikiwa vizuri. Sasa kama sisi kwenye Wilaya tunaweza, huko kwenye Wizara kuna tatizo gani? Ninaomba sana Waziri wa Kilimo atakapokuja na bajeti yake aje na mkakati huo wa kutatua kero ya ruzuku kwa wakulima na hasa wakulima wangu wa Jimbo la Peramiho wanaolima mahindi kama zao lao kuu la biashara na zao kuu la chakula.

Mheshimiwa Spika, niingie katika Vyama vya Akiba na Mikopo. Ninakushukuru umelizungumza sana kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, ana lengo zuri sana kwa Watanzania. Serikali ya Awamu ya Nne ina mipango mizuri sana ya kuondoa umaskini kwa Watanzania. Ninaomba nipongeze Mfuko wa Uwezeshaji na mifuko mingine yote ya *SELF, TASAF* na kadhalika katika kuwahudumia Watanzania ili waondokane na umaskini. Lakini nizungumzie Mfuko wa Uwezeshaji Jamii.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kimsingi kwamba Mfuko huu sasa ndio uangalie namna gani utaboresha kazi za wajasiriamali wadogo wadogo. Lakini sasa wajasiriamali wadogo wadogo wanajigawa katika sekta nyingi. Mimi ukiniambia wajasiriamali wadogo wadogo kwenye Jimbo langu kule Peramiho, Madaba, Wino na kadhalika ni wakulima. Ninaomba nikwambie kwamba, Mfuko huo haujawafikia wale walalahoi huko vijijini mpaka dakika hii!

Mheshimiwa Spika, kilichokuwa kinatakiwa, nafikiri ni kutengeneza utaratibu muafaka, tumetumia kipindi kirefu kutegemea sana hizi Benki tulizozipa majukumu ya kufikisha fedha hizi kwa wananchi. Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii ilifanya ziara ya makusudi katika Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha. Tulitembelea *SACCOS* ya Kaya, *SACCOS* pale Same: *SACCOS* ile ni nzuri, inafanya vizuri, lakini walitumbia wao kamwe hawatakwenda kukopa fedha *CRDB* kupitia Mfuko wa Ujasiriamali. Wakatupa sababu wakasema, sababu kubwa ya kimsingi, riba ya asilimia 12 ambayo asilimia 10 inatakiwa ibaki pale kwenye *NMB,* asilimia mbili ndiyo ichukuliwe na *SACCOS* kuwafikia wananchi walalahoi kule vijijini, *SACCOS* haitaweza.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kukuambia leo, tulipofika *NMB* pale Same walituambia bila ya kutuficha kwamba hawawezi wao waka-*guarantee* kufanya kazi kule

kwenye milima ya Same, kule juu kuwafuata wakulima kwa gharama kubwa halafu kwa kutumia hiyo riba ya asilimia 10 wakati wanapata labda wajasiriamali wawili. Hicho kitakuwa ni kitu ambacho hakiwezekani. Kwa hiyo walishawishi Vyama vya Akiba na Mikopo ndivyo vikafanye kazi kule, lakini Vyama vya Akiba na Mikopo, kwanza masharti magumu ya *CRDB* hawayawezi; pili riba ya asilimia mbili kuwafikia walalahoi kule Buhukulu mpakani mwa Msumbiji na Tanzania kwenye Jimbo langu ni kufanya mchezo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali kwa nia nzuri ya Mheshimiwa Rais, hebu tukae tujadiliane. Hatuwezi tukakubaliana namna gani *SACCOS* zetu zikaongezewa matumizi hayo ya riba kutoka asilimia mbili labda mpaka asilimia sita ili azma ya Chama cha Mapinduzi kuimarisha Vyama vya Akiba na Mikopo ikaweza kutimia sawa sawa. Wananchi wameelewa umuhimu wa kuweka akiba, wanajua hakuna maendeleo bila ya kukopa. Ninakwambia dhana hiyo imeeleweka, kinachotakiwa ni kufanya maamuzi na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hiyo, ninawashukuru sana *SIDO*. Nilipata shida baada ya kuanzisha hiyo mikakati na nilikuwa sina mahali pa kukimbilia kuwawezesha wajasiriamali wangu. Ninamshukuru sana Meneja wangu wa *SIDO* Mkoa wa Ruvuma. Mama Lucy Sarungi ni mwanamke imara, aliniambia tutafanya kazi. Mimi nitakwenda vijijini kama Benki zimeshindwa kuwafikia wajasiriamali vijijini. Nampongeza yule mama, naipongeza *SIDO* na nasema *SIDO* wanaweza kuwa wakombozi wakubwa sana kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niingie katika posho za Madiwani. Leo tumeambiwa kwamba Madiwani hawa wanaruhusiwa kujilipa posho zao mpaka Sh. 60,000/= kulingana na uwezo wa Halmashauri. Wiki nzima napigiwa simu kutoka kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songea, tunajikuna vichwa kuangalia, hivi Halmashauri yetu ilivyo maskini tunawezaje kupata mapato ya kupandisha hiyo posho ya Madiwani kwa kiwango hicho kinachokaribiana na kilicholetwa? Imekuwa kazi kubwa!

Mheshimiwa Spika, Madiwani wanafanya kazi kubwa sana kila siku asubuhi, mchana na jioni. Nilikuwa naomba Serikali, kwa nini isiamue kwa makusudi kutoa ruzuku ili kufidia posho hizo za Madiwani? Kama itagundulika kwamba kuna Halmashauri zitashindwa kuwalipa Madiwani kwa kiwango kilichowekwa, tofauti hiyo itakuwaje? Hawa wote ni watendaji na wanahitaji wahudumiwe kwa viwango vinavyolingana. Ninaomba Serikali ifikirie sana suala hilo.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana bajeti ya mwaka jana, tulikubaliana, Waziri alinionyesha mpango mkakati, nakumbuka mimi na Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu tukakutana naye tena na wataalamu wake tukakubaliana kwamba bajeti itazingatia kupeleka umeme Peramiho. Sasa nasikitika kusema kwamba mpaka sasa umeme Peramiho haujafika. Nimefuatilia, jibu nililolipata leo kwa Naibu Waziri, ananiambia Mheshimiwa Mbunge inaelekea mchakato wa kutafuta fedha hizo ndani na nje ya nchi unaendelea ili kupeleka umeme vijijini ikiwemo Peramiho. Inanisikitisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mudhihir amemwomba Naibu Waziri wa Maji, mimi namwomba Naibu Waziri wa Nishati na Madini aende akawajibu wananchi wa Peramiho majibu hayo na mimi sitakwenda kuyaeleza tena. Walinisikia Bunge la Bajeti la mwaka jana, sasa namwomba yeye aambatane na mimi na akajibu hoja hizo huko Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuomba Serikali, ninaishukuru kwa kuanzisha Wilaya mpya lakini ninaomba izingatie uanzishwaji wa Kata mpya. Hilo ni suala la msingi sana. Utawala bora unaanzia kwenye Kata ndipo unakuja kwenye Wilaya. Suala la Kata mpya bado ni kero kubwa sana huko katika maeneo tunayotoka.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, ameanza kazi nzuri. Fedha za kudhibiti UKIMWI zimekuwa zikifujwa sana Tanzania kuanzia ngazi ya juu mpaka chini. Ninaomba tumpe *support* mama yetu, hizi fedha ziweze kufanya kazi kweli ya kupambana na UKIMWI na sio kupambana na matatizo mengine mbadala badala ya UKIMWI wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kukubali kutoa mrahaba katika maeneo ya machimbo ya madini. Nitakuja na hoja.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la machimbo ya kokoto yanayojenga barabara za lami katika nchi yetu ya Tanzania. Machimbo hayo yamekuwa katika maeneo ya vijiji na katika Halmashauri zetu. Wananchi wanatuuliza, wao wanafikiriwa kwa namna gani kwa usumbufu mkubwa wanaopata kutokana na machimbo ya kokoto ambayo yamekuwa yakitumika katika ujenzi wa barabara katika nchi yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwaomba watendaji wa Serikali waheshimu maamuzi yanayopitishwa na vikao vya Halmashauri zetu. Kumekuwa na tabia ya maamuzi yanayopitishwa na vikao vya Halmashauri zetu, wengine wanakuja kuyatengua na kuona sio maamuzi muafaka. Tumeamua madaraka kupeleka kwenye Halmashauri na ninaomba Halmashauri ziheshimike katika maamuzi yake.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumwombea Mheshimiwa Waziri Mkuu afya njema na maisha bora katika nchi yetu ya Tanzania akisaidiana na Mheshimiwa Rais wetu katika kuiongoza Serikali ya Awamu ya Nne.

Ninawaombea Mawaziri wote waendelee kufanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya na ninawapongeza sana kwa kuwa wamefanya kazi yao vizuri katika kipindi cha mwaka wa kwanza uliopita tunaamini wataendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja na niseme nakushukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa ajali za

basi zilizotokea Mkoa wa Singida na Arusha. Napenda nitoe mkono wa pole kwa wafiwa wote na nawaombea Marehemu wapumzike mahali pema Peponi. *Amina!*

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana. Nimeisoma, inafafanua mambo mengi na mimi nitachangia maeneo machache tu ya yale ambayo amejaribu kuyafafanua katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni Maji. Mwaka jana nilipokuwa nachangia Wizara ya Fedha nilitamka kwamba Serikali haipeleki pesa kwenye miradi ambayo imeidhinishwa Wilayani; na nikatoa mfano wa mradi wa Ntomko. Mwaka 2005/2006 mradi huo ulitengewa shilingi milioni 30, kupitia Wizara ya Maji na nikalamika kwamba pesa hizo hazijafika. Leo nina malalamiko makubwa zaidi na masikitiko zaidi kwa sababu fedha ile milioni 30 ya mwaka 2005/2006 haijaletwa kwa mradi huo wa Ntomoko na mwaka huu unaoishia mwezi Juni mwaka huu zilitengewa shilingi milioni 100. Mpaka sasa mradi huu haujapata hata senti tano. Matokeo yake ni nini?

Matokeo yake, ule mradi umevurugika sana, hivi sasa hakuna huduma ya maji kwa wananchi 50,000 ambao wanategemea mtaro huo. Nami niungane na Mheshimiwa Jenista kusema kwamba Waziri wa Maji namwomba aende akawajibu wananchi wa kule kwa sababu mimi nimetoa maelezo nimeshindwa kuwaridhisha. *(Makofi)*

Waziri wa maji nimeshamweleza kwa kina kabisa, lakini naona ameshindwa kunielewa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi yako itumike tuweze kupata maji kwa sababu Kiangazi ndiyo kinaingia, wananchi hawana maji kabisa sasa. Baada ya kuzungumzia suala la maji, naomba nigusie tena mradi wa maji wa Benki ya Dunia. Wilaya ya Kondoa ni kati ya Wilaya 11 zinazotekeleza mradi huo, lakini nasikitika kusema kwamba mradi huo umekwama na sababu ni urasimu wa Wizara ya Maji. Mambo yote yameshikiliwa kule Wizarani.

Mheshimiwa Spika, tumepewa visima 10. Kati ya hivyo visima saba vimepata maji, lakini kazi haziendi, *pump* hazinunuliwi kwa sababu jukumu la kununua *pump* na mashine ni la Wizara, lakini hawafanyi kazi hiyo. Kwa hiyo, miradi imesimama na wananchi wanaendelea kupata taabu katika Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Waziri wa Maji apunguze urasimu kwa sababu pesa ipo, sioni sababu ya urasimu huu. Naomba basi hii miradi ambayo imekusudiwa kutekelezwa kupitia Mkopo wa Benki ya Dunia, basi isimamiwe kwa kasi na miradi iweze kutekelezwa kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kuifanya katika kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Barabara nyingi zinajengwa kwa kiwango cha lami, lakini nasikitika kusema kwamba baadhi ya barabara zetu zimepuuzwa. Moja ya barabara ambayo imepuuzwa mpaka sasa na Serikali hii ni barabara ya kutoka Iringa, Dodoma mpaka Babati. *(Makofi)*

Tumekuwa tukisema muda mrefu kwa zaidi ya miaka 20 hivi sasa. Lakini kila leo huwa tunaambiwa kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami. Lakini kwa kweli hata ukiangalia bajeti yake unaona kwamba Serikali kama vile haina nia ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Kwa mfano, mwaka huu fedha zilizotengwa kwa ajili ya barabara ya kutoka Iringa kuja Dodoma ni shilingi milioni 900, sijui ya kazi gani! Lakini mbaya zaidi ni barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati imetengewa shilingi milioni 10. Mimi nafikiri mngefuta tu hata hizo shilingi milioni 10 kwa sababu hazina kazi. *(Makofi)*

Hivi tutaendele kusema mpaka lini? Ndiyo maana Wabunge hapa wanasema jamani, inauma. Inauma kama tunazungumza kila siku lakini Serikali inaonekana kama haisikii. Mimi naomba basi mwakani, naomba kabisa barabara hii itengewe pesa za kutosha ili barabara ianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia barabara, sasa naomba niende kwenye sekta nyingine ya Elimu. Niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri na msukumo mkubwa uliotolewa katika Elimu na hasa sekta ya Elimu ya Sekondari. Naambiwa zaidi ya sekondari mpya 1000 zimejengwa na kufunguliwa mwaka huu. Kwa hiyo, naipongeza sana kwa kazi nzuri ambayo inafanyika. Lakini hata Waziri wa Mipango katika hotuba yake alikiri kwamba kuna matatizo makubwa katika kusimamia Elimu ya Sekondari. Moja ya matatizo ni upungufu wa Walimu; na mbaya zaidi ni kwamba hata hizi shule tulizofungua zaidi ya 1000 hazina viongozi. Viongozi maana yake nini? Wakuu wa Shule hawajateuliwa mpaka leo. Kwa hiyo, shule zina endeshwa kienyeji. Waratibu wa Elimu ndiyo Wakuu wa Shule. Mimi katika Wilaya yangu ndiyo wanaosimamia hizo shule. Sasa hawa waratibu kwa kweli hawana uwezo wa kuweza kuendesha Sekondari zetu.

Tunaomba haraka sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi teueni Wakuu wa Shule waweze kupelekwa katika shule hizi zianze kutoa elimu inayokusudiwa na uongozi unaotakiwa. Kwa hiyo, naomba basi hilo lifanyike, sambamba na hilo Walimu waongezwe kwa sababu sasa hivi shule zetu nyingi zina walimu mmoja mmoja, au wawili wawili. Kwa hiyo, hakuna elimu inayotolewa katika mazingira hayo. Wananfunzi wanakwenda shuleni na kurudi, labda wanaitwa majina na kurudi, lakini elimu inayotolewa ni kidogo sana.

Nyongeza ya hapo, kuna majengo muhimu kama mlivyoandika katika hotuba ya bajeti na pia katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Majengo kama nyumba za Walimu, maabara ni muhimu na pia vifaa vya kufundishia, vitabu ndiyo hakuna kabisa! Kwa kweli elimu haitolewi. Tunaomba kama Waziri Mkuu alivyoahidi katika hotuba yake, basi suala la kuimarisha Elimu ya Sekondari lifanyiwe kazi kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo, naomba sasa nihamie kwenye Sekta ya Afya. Pia niipongeze sana Serikali kwa kuja na sera mpya ya afya kwamba kuanzia mwaka kesho tutaanza kutekeleza sera mpya ya afya ya kujenga Zahanati katika kila kijiji na Kituo cha Afya katika kila Kata nchi nzima. Naipongeza sana kwa sera hiyo, lakini changamoto ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto yenyewe ni kwamba ukweli wenyewe hali ya sasa hivi ya Zahanati zetu na Vituo vya Afya ni mbaya sana. Hatuna watumishi, Zahanati nyingi zinaendeshwa na Manesi ama Wahudumu ambao hawana utaalam wowote. Sasa sambamba na kutekeleza sera hii, naomba basi Serikali ichukue hatua za dhati kabisa kuwafunza wataalam hasa Waganga waweze kuchukua nafasi zao katika Zahanati hizo mpya na Vituo vya Afya vipya vitakavyojengwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kondoa, zaidi ya Zahanati kumi hazina Waganga. Mbaya zaidi sasa hivi katika Wilaya ya Kondoa na hasa nizungumzie Jimbo la Kondoa Kusini, hivi sasa kuna Zahanati tano, zimejengwa na kukamilika miaka mitatu iliyopita, lakini bado hazijafunguliwa kutokana na ukosefu wa watalaam. Aidha, tuna Kituo cha Afya kimoja ambacho karibu kinakamilisha majengo yote, lakini mpaka leo hatujafungua kwa sababu hatuna watumishi.

Sasa najaribu kufikiria tutakapoanza kujenga Zahanati katika kila kijiji na Kituo cha Afya katika kila Kata, sijui hali itakuwa namna gani! Kwa hiyo, naomba kama Waziri Mkuu alivyoelezea katika hotuba yake ukurasa wa 34, basi jitihada zifanyike ili mapungufu hayo yaweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hayo, naomba niende kwenye eneo la mikopo ya Wajasiliamali. Naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 1.0 kwa kila Mkoa mwaka jana kwa ajili ya kuwawezesha Wajasiliamali wadogo wadogo. Lakini napenda niseme tu kwamba pesa hizi kwa kweli hazijasaidia sana kuondoa umaskini katika maeneo ya vijijini. Sababu ni nini? Sababu ni kwamba, masharti yanayotolewa na Benki hizi za Biashara ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Benki hizi zipo mbali sana na wananchi, kwa hiyo, wananchi wengi sana wameshindwa kunufaika na mikopo kutokana na mikopo kutokana na pesa zilizotengwa. Hivi karibuni tuliambiwa kwamba katika Mkoa wa Dodoma, kati ya zile shilingi bilioni 1.0 tulizopewa mpaka sasa ni shilingi milioni 240 tu ndizo zilizokopwa.

Lakini zaidi ya shilingi milioni 700 bado hazijatoka kwa sababu ya tatizo hili. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anaahirisha Bunge la mwaka jana la Bajeti, alisema hivi: twende tukashirikiane kwa maana ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuunda *SACCOS* na aliahidi kwamba pesa hizi zingepelekwa kwenye *SACCOS* ili wananchi waweze kukopa kwa urahisi. Sasa maamuzi yaliyotoka baadaye ni tofauti na yale ambayo Waziri Mkuu alituhimiza tufanye. Mimi naomba Serikali ichukue hatua za dhati kuimarisha *SACCOS* zetu ili pesa hii inayotoka Serikalini iweze kwenda moja kwa moja huko badala ya Mabenki hilo ndilo ombi langu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie juu ya Wilaya mpya. Napenda niikumbushe Serikali kwamba, Wilaya ya Kondoa ni kati ya Wilaya kongwe katika nchi hii. Wilaya hii iliundwa wakati wa enzi za Ujerumani na

mpaka sasa haijagawanywa, imekua, watu wameongezeka na eneo bado ni kubwa. Tulipeleka maombi yetu tusaidiwe kugawa Wilaya hii katika Wilaya mbili kwa lengo zuri tu. Lengo la kusogeza huduma kwa wananchi.

Nimejaribu kusoma hotuba ya Waziri Mkuu, sijaona mahali popote ilipozungumzia Wilaya ya Kondoa. Imezungumzia Wilaya nyingine tu. Naomba tusaidiwe, Wilaya hii ni kubwa mno na inakaribia watu 500,000 na zaidi ya eneo la hekta 13,000 ambayo yote inakaliwa na watu. Kwa hiyo, tunaomba kama imeshindikana leo katika Bajeti ijayo tufikiriwe na sisi kuweza kumpunguzia Mkuu wa Wilaya ili Wilaya ya Kondoa iweze kutawalika kama itagawanywa sehemu mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naomba nitamke kwamba naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kuendelea na lolote tena kwa jioni hii. Kwa hiyo, naomba nitangaze tu yafuatayo:-

Kwanza kwa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, jina la Kambi ya Upinzani litabaki hivyo hivyo kwa sababu hatuwezi katikati hapa tukaleta mambo mapya ambayo hayana mjadala wa kina. Kwa hiyo, bado mtaendelea Kambi ya Upinzani na mfurahi tu, kwanza mambo mengi mnayapinga; sio vibaya kupinga, unapinga unaweza na mbadala, basi sawa, kwani kuna ubaya gani? Kwa hiyo, hilo naliondoa lisituchukulie muda.

La pili, ni kwamba *Hansard* kwa hotuba ya Mheshimiwa Dr. Slaa kwa sababu ilikuwa na matatizo mengi, *Hansard* itarekodi yale yasiyo na matatizo.

Kwa hiyo, wenzetu wa Waandishi wa Habari wasichukue yale maneno kama nchi inateketea na nini ambayo yamo katika ile *printed speech* kwa sababu hiyo haitakuwa rasmi Kibunge. Hatuwezi tukasema nchi yetu inateketea. Yapo matatizo kama nchi nyingine lakini hakika haiteketei.

La tatu, ni kwamba, nimeletewa karatasi hapa, mgongano baina ya Kanuni ya 50 (6) na 49(7). Huu sio mgongano. Kanuni zozote zinakuwa na maelezo na wapi unaweka uzito. Kuhusu Mheshimiwa Dr. Mzindakaya angeweza akalindwa na Kanuni ya 50(6) inayokataza kusemana. Lakini kinga hiyo ipo tu kama Kanuni ile nyingine haikuonekana kuvunjwa. Nieleweke hivyo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kama ukisimama hapa na una jambo ambalo linaonekana kuwa una maslahi nalo kwa Kanuni ya 49(7) ni lazima uliseme. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huwezi ukaja kusema kwamba kwa sababu inakatazwa kumsema Mbunge mwingine, basi hata lile ulilioficha lisiweze kuumbuliwa. Sasa kilichopo hapa ni kwamba chini ya Kanuni ya 40, unaweza kutoa maelezo binafsi na hiyo ndiyo inaweza ikasahihisha. Ndiyo mwenendo wa Kanuni, moja inasema hivi, nyingine inasema hivi, zinakwenda zinasahihishana halafu tunafika pazuri. Kwa hiyo, nitatoa

nafasi kwa Mheshimiwa Mzindakaya sasa hivi chini ya *Adjournment Motion* kwa Kanuni ya 40.

Kabla ya kumwita Mheshimiwa Mzindakaya naomba kusema tu, nina maombi mengi sana ya kubadili badili na karibu kila mmoja wetu anajaribu dharura ambayo nyingine zinatia huruma, lakini sasa Kiti kitashindwa kabisa kuendesha shughuli hizi kama kila mtu atasema kesho mchana lazima aondoke.

Kwa hiyo, nasikitika sitazingatia hayo, wale ambao walikuwa wanaona wanala maana la kusema kwenye *Vote* ya Waziri Mkuu Wabaki wayaseme. Lakini kuuguliwa, wote tunauuguliwa tu, ndiyo hali halisi katika familia yote hakuna mgonjwa. Kwa hiyo nitazingatia tu dharura za kweli kweli zenye ushahidi ili kubadili.

Kwa maana hiyo basi wachangiaji wa kesho, ataanza Mheshimiwa Lucy Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Blandes anaumwa hayupo, kwa hiyo, atafuatia Mheshimiwa Galinoma. Halafu tutaendelea na utaratibu huo kwa namna hiyo.

Kwa hiyo, sasa hivi namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi awasilishe hoja ya kuahirisha Bunge.

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIANI):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umetoa nafasi kwa Mheshimiwa Mzindakaya kutoa maelezo yake kuhusu baadhi ya hoja zilizotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani; na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 40 umemruhusu; hivyo basi, naomba kwa mujibu wa Kananu ya 21(4) Bunge lako Tukufu likubali kuendelea kukaa ili tuweze kujadili hoja Mheshimiwa Mzindakaya.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

## HOJA BINAFSI YA MHESHIMIWA DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maelezo yangu chini ya kifungu cha Kanuni ya (40) na pia naomba sasa kwa sababu maelezo yamenihusisha, nihusishe pia kifungu cha 49(7). Kwa ajili ya kuokoa muda sina haja ya kusoma kwa sababu vifungu hivi Waheshimiwa Wabunge wengi wanavifahamu.

Lakini pia napenda nitumie nafasi hii vilevile kujieleza kwa kutumia kifungu namba 50(6), ambacho kinalinda na kinazuia Mbunge mmoja kusema au kumtaja Mbunge mwenzake binafsi. Pia kwa ajili ya kuokoa muda, sitaweza kukisoma kwa sababu kifungu hiki Waheshimiwa Wabunge wanakifahamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, niseme kwamba katika maneno ya Mheshimiwa Dr. Slaa aliyokuwa ameyasema leo hii; napenda kunukuu:

"Mheshimiwa Spika Kambi ya Upinzani imefarijika sana kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekiri kufahamu taarifa aliyoitoa hapa Bungeni kuhusu ubadhirifu mkubwa ndani ya *BoT*, unaomgusa Gavana wa Benki Kuu pamoja na Wafanyabiashara wengine wakubwa akiwemo Mbunge kupitia kampuni anayoimiliki."

Kwa maelezo haya maana yake ni kwamba, katika kashfa inayohusiana kule Benki na mimi nimehusishwa jambo ambalo nafikiri sio sahihi. Maneno hayo yanahitaji uthibitisho ikiwa Mbunge Mzindakaya ni sehemu ya ubadhirifu unaozungumzwa. Nakiri kukopa deni katika Benki ya Biashara kwa dhamana ya Serikali na sijakopa au kudhaminiwa na Benki Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikiri kuwa Mheshimiwa Dr. Slaa ni Mbunge mwenzangu sawa na binafsi, anafahamu jinsi mimi na yeye tunavyofahamiana na kuheshimiana. Kwa kweli naweza kusema tuko marafiki. Natambua pia Wabunge wote hapa Bungeni tuko sawa, hakuna Mbunge bora kuliko Mbunge mwingine. *(Makofi)*

Sasa napenda kutoa maelezo sahihi juu ya shutuma alizotoa Mheshimiwa Dr. Slaa katika maelezo yake. Mwaka 2004, Serikali ilianzisha Sera ya kuwawezesha Watanzania ambayo miradi yao inaonekana kuwa ina manufaa kwa uchumi wa nchi. Ingawa nia ya Serikali wakati ule ilikuwa ni kuitumia *TIB* kwa miradi ya kilimo na ile ya ufugaji, *TIB* ilikuwa bado haijajiandaa vikamilifu.

Kwa hiyo, Serikali ilitoa mwongozo kuwa kwa wakati ule wenye miradi waende katika Benki watakazokuwa wamechagua na Benki hizo kuwakubalia.

Mheshimiwa Spika, vilevile Benki husika ndiyo zitaandika barua Serikalini na kwa Benki Kuu na badala ya Serikali kutoa udhamini kwa Benki iliyotoa mkopo, Serikali ilitoa dhamana kwa Benki Kuu. Narudia, Serikali inatoa dhamana kwa Benki Kuu ili Benki Kuu nayo ndiyo iende ikamdhamini mkopoji kwa Benki husika. Kwa hiyo, mdhamini hapa ni Serikali na sio Benki Kuu.

Kwa utaratibu uliopo, ni kuwa Serikali pia haiwezi kutoa mkopo. Kwanza yule mwenye mradi lazima aende kwenye Benki yoyote aliyoichagua mwenyewe, Benki ile ndiyo iridhike kwamba ule mradi ni *viable* unafaa kiuchumi. Kama haufai wala hutakwenda Serikali kuomba mkopo.

Mheshimiwa Spika, mdhamini wa mkopo wangu narudia sio Benki Kuu, ni Serikali kupitia Wizara ya Fedha. Mkopo wa *Standard Chartered Bank* sio wa muda mrefu. Mara nyingi wanatoa mkopo wa muda mfupi usiozidi miaka mitano.

Mradi nilioombea mkopo ni ufugaji wa ng'ombe wa nyama na ujenzi wa machinjio na kiwanda cha kisasa ambacho ulipaji wake hauwezi kuwa wa muda mfupi, ni wa muda mrefu.

Lakini *Standard Chartered Bank* kwa kuwa waliridhika kwamba mradi huu ni mzuri, walikubali kutoa mkopo kwa mradi huo na kwa kuwa muda wao ni miaka mitano baada ya mradi wenyewe kuanza kutekelezwa na baada ya kuridhika kwamba mradi huu ni mzuri, wao wenyewe ndiyo waliotoa mapendekezo kwa Serikali Kuu kwamba mradi huu tumeridhika, ni mradi mzuri, lakini mkopaji hawezi kuulipa kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ufugaji na kilimo ni wa muda mrefu. Tunapendekeza Serikali mpeleke katika Benki nyingine ambayo muda wake utakuwa mrefu kwa mkopaji.

Baada ya hayo Benki niliyokopa ambayo sina haja ya kutoa maelezo mengi, ilipopeleka mapendekezo yake Serikali ilikubali kwa kuzingatia umuhimu na faida ya mradi huo. Baada ya kukubali, Serikali yenyewe ndiyo iliagiza Benki Kuu kwamba mimi sasa nihamie *TIB*. Kwa hiyo, mkopo niliokopa mimi na dhamana ni ya Serikali Kuu na sio ya Benki Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie tena, Serikali inatumia vyombo. Benki Kuu haikopeshi, duniani kote Benki Kuu hazitoi mikopo. Kwa hiyo, mimi sikukopeshwa na Benki Kuu kwa sababu haiwezi kukopesha mtu, haina hela ya kukopesha.

Fedha zote nilizokopeshwa mimi, mdhamini wake narudia ilikuwa ni Serikali Kuu na fedha ambazo ilionekana lazima nihamie Benki ya *TIB* Serikali ndiyo imelipa katika Benki niliyokopa mimi, siyo Benki Kuu kama ilivyoelezwa hapa. Narudia tena, Serikali Kuu ndiye mdhamini sio Benki Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kueleza kuhusu kiwango cha deni la kampuni kwa kuwa hiyo sio kazi yangu kueleza hapa. Deni la mkopaji ni siri kati yake na Benki yake. Kwa hiyo, takwimu zilizotolewa hapa, mimi siwezi kuzithibitisha kwa sababu ni siri ya mkopaji na mkopeshaji.

Mheshimiwa Spika, kiwanda tulichojenga kina faida nyingi. Kwanza kitatoa ajira kwa wafanyakazi 180 na wale wasiokuwa wa moja kwa moja watakuwa wafanyakazi 2,300, kitasaidia Taifa letu kupata fedha za kigeni, tutaokoa fedha za kigeni kwa kuzuia hoteli zetu za kitalii kuagiza nyama kutoka nje.

Vile vile, napenda kusema hapa kwamba Mkoa wa Rukwa tangu tumepata uhuru hiki ndicho kiwanda cha kwanza kujengwa katika Mkoa na kimejengwa kutokana na Sera za Chama chetu za uwezeshaji wa Watanzania Wazalendo. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana katika sera za Chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaweza sasa nikatambua kwamba mtu mweusi kufanya maendeleo ya aina hii tuliyofanya ni dhambi kabisa kwa sababu hakuna atakaye-*appriciate* jambo kama hilo na leo maelezo haya ni ushahidi.

Vile vile sio kweli kwamba Kampuni yangu imeomba mkopo mwingine wa mabilioni kutoka Benki Kuu. Kampuni yetu imeomba mkopo wa kuendeleza shughuli zake kutoka Benki ya *TIB,* sio Benki Kuu kwa sababu Benki Kuu haitoi mikopo.

Mheshimiwa Spika, mimi sikujua kama lengo la maelezo ya Mheshimiwa Dr. Slaa ni Gavana kwa jina Mr. Balali, mimi sikujua. Mimi nilisemea baadhi ya mambo mazuri ambayo Benki Kuu imeyafanya katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Mimi sijatetea maovu yoyote ambayo yanamlenga Gavana kwa sababu mimi sikujua hayo.

Mheshimiwa Spika, mimi niliisifu Serikali kwamba imekubali na itafanya ukaguzi yanayozungumzwa kuhusu Benki Kuu. Nimekuwa mtetezi na nimeendelea kuwa mtetezi wa wananchi kupitia sera za Chama changu, sijakuwa na sera yangu hata siku moja, nimekuwa natumia sera za Chama changu kuwatetea wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kazi hii nimeifanya katika kipindi kisichopungua miaka 40 ya uongozi wangu. Katika kipindi chote cha uongozi wangu, sijapata kuhusishwa na kashfa yoyote katika maisha yangu na hili ni deni. Deni ni deni na duniani kote huwezi kufanya maendeleo bila kukopa. Nimekopa katika Benki, sikuiba wala siku-*collude* na Benki Kuu. Benki Kuu haikopeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika baada ya hayo, ningependa niseme tena kwamba Watanzania wengi mnaotaka maendeleo, lazima mkope na mimi ningekuwa tajiri kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge katika maelezo yake nisingekwenda kukopa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nieleze kwamba kwa umri wangu mnavyoniona sikujenga kile kiwanda ili niwe tajiri, nimejenga kusaidia maendeleo ya nchi yangu. Kwa sababu ukishafikia miaka 65 hutafuti tena utajiri. Mimi nimejenga kwa ajili ya nchi yangu, kitasaidia wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kitatoa ajira. Mimi sina watoto wa kuajiri katika kile kiwanda, watafanya kazi Watanzania na kinaleta maendeleo kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mzindakaya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge baada ya maelezo hayo, nadhani hoja hii sasa inaweza ikaachwa hivyo ilivyo kwa sababu mmepata maelezo ya Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, nami naridhika kwamba kwa kuwa mkopo ulikuwa wa kibiashara, alikuwa hana haja yaku-*declare conflict of interest* yoyote kwa sababu hata *guarantee* yenyewe kumbe ni ya Serikali. Kwa hiyo, hakuathiri Kanuni ya 49 (7).

Nimekumbushwa hapa na Sekretarieti kwamba kwa kuwa tukio la leo sio la kila siku, inahitaji sasa niwahoji kuhusu kuahirishwa Bunge kwa sababu hoja ilitolewa na Waziri wa Nchi (Bunge) na kupita wakati wake na iliungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wasioafiki watabaki humu humu, kwa sababu walioafiki wameshinda na sasa naliahirisha Bunge hadi kesho asubuhi Saa Tatu.

*(Saa 02.04 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 26 Juni, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*